# Nipashe

Ijumaa Aprili 3, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580196

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US



## Latra yatangaza neema wenye mabasi kusafirisha abiria Dar

UKURASA 3


Asimulia safari iliyoanzia shule ya walimu wawili mume, mke
TRC inavyokabili janga kuu la corona
BUFE
IJUMAA APRILI 3, 2020
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA
MIKOPO SH.MIL.301 Halmashauri Shinyanga 'zajibu' kuelekezea kinamama na vijana
MWALIMU, MJASIRIAMALI...
Mtotoa vifaranga anayesimamia siri mafanikio, nyenzo nishati jua
UCHUMI
Habari katika picha
Mustakabali wa kuambukizana corona na kitendawili umaskini

UKURASA 13

# Corona yatawala mjadala bungeni

UKURASA 2



## BAA LA CORONA

**IDADI ya wananchi waliowekwa karantini Zanzibar imeongezeka na kufikia 324 wakiwamo madaktari 27 kwa ajili ya kufanyiwa uchunguzi wa maambukizi ya virusi vya corona.**

- **Epuka mikusanyiko ya watu**
- **Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka**
- **Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana**
- **Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo**

## Mbowe atangaza mabadiliko upinzani

UKURASA 4



Wafanyabiashara wa nyanya katika soko la Tasaf, eneo la Ilula, wilayani Kilolo, Mkoa wa Iringa, wakizipanga kwenye vifaa vya kusafirishia kwa ajili ya kuuza nje ya mkoa huo jana. Wanadai bei ya bidhaa hiyo imeshuka kutokana na wateja wao wengi ambao ni wafanyabiashara kutoka Kenya kufungiwa mipaka kutokana na tahadhari ya ugonjwa wa corona. Tenga limeshuka bei kutoka 80,000/- hadi 30,000/-. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

Scan Hapa



Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu
GET IT ON Google Play
Download on the App Store

# Watu 168 wawekwa karantini

• **Wamo** madaktari 27, Mbunge ataka udhibiti uongezwe, baadhi ya viongozi wadaiwa kugoma kupimwa, hofu yatanda Namanga, wachimbaji, wakulima nyanya wadai kuathirika...*Uk. 2, 3, 4, 7, 8, 23, 26*

**MICHEZO** **KASEJA ATAMBIA KIWANGO CHAKE** UK.32

**MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

# Watu 168 wawekwa karantini

**Na Manuel Kaminyoge,** SONGWE

KATIKA kutekeleza maagizo ya serikali ya kuhakikisha wasafiri wote nje ya nchi zikiwamo zenye maambukizi zaidi ya virusi vya corona wanatengwa, wasafiri 84 kutoka Afrika Kusini wamewekwa karantini kwa muda wa siku 14 mjini Tunduma.

Wakati wasafiri hao wakizuiwa, habari kutoka Zanzibar zinasema watu 84 wakiwamo madaktari 27 waliokuwa wakiwahudumia wagonjwa wa corona, nao wamewekwa karantini, hivyo kufanya idadi ya waliofanyiwa hivyo kuwa 168.

Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Brigedia Jenerali Nicodemus Mwangela, alisema hayo jana alipofanya ukaguzi wa maandalizi ya utayari wa kupambana na Corona kwa Mkoa wa Songwe hususani maeneo ya mipakani, kwenye halmashauri za Wilaya ya Ileje na Mji wa tunduma.

Alisema wasafiri hao ambao ni Watanzania 55 na raia wengine kutoka Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), Afrika Kusini, Kenya na Uganda, walipoingia nchini kupitia mpaka wa Tunduma, walipimwa na kukutwa hawana dalili za corona.

Licha ya kuwa hawakuwa na dalili, lakini alisema kwa kuwa wametoka katika nchi yenye maambukizi zaidi wamewekwa katika karantini.

Alisema utaratibu huo ni kwa ajili ya kuwaaangalia ndani ya siku 14 na kama watakuwa hawana dalili za virusi vya Corona, wataruhusiwa kuendelea na safari zao.

Jenerali Mwangela aliwaagiza viongozi katika sekta mbalimbali kuendelea kutoa elimu ya namna ya kujikinga na corona na pia katika ofisi na taasisi zote usafi uzingatiwe likiwamo suala la kunawa mikono kwa maji na sabuni.

Pia aliagiza Jeshi la Polisi Mkoa wa Songwe kufanya msako katika maeneo ya stendi za mabasi endapo kutakuwa na raia kutoka katika nchi zenye maambukizi zaidi ya corona na wamepitia njia zisizo rasmi ili wawekwe karantini.

"Mpaka sasa tumewaweka karantini wasafiri 84 katika mpaka wa Tanzania na Zambia ambao wengi ni raia wa Afrika Kusini na Congo na kazi hii inaendelea kusimamiwa vilivyo," alisema.

Naye Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, George Kyando, alisema jeshi hilo limepiga marufuku kwa mabasi kujaza abiria kuliko uwezo wa gari, kutokuwa na vitakasa mikono kwenye mabasi au maji na sabuni kwa ajili ya kunawa na marufuku ya mabasi kuanza safari bila kupuliziwa dawa.

Alisema yeyote atakayepuuzia marufuku hizo ambazo zimelenga kuweka tahadhari ya kutosambaza ugonjwa wa corona atakuwa anataka kusambaza ugonjwa kwa makusudi jambo ambalo ni kosa kisheria hivyo hatua kali zitachukuliwa dhidi yake.

"Nimewaagiza askali wangu wa usalama barabarani wasiruhusu basi kujaza abilia, bora izuiliwe kufanya hizo biashara na si kujaza abiria," alisema.

Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Mji wa Tunduma, Dk. Enock Mwambalaswa, alisema wasafiri wote waliowekwa karantini wanapimwa mara mbili kwa siku ili kufuatilia maendeleo ya afya zao.

Alisema endapo atatokea mwenye dalili za virusi vya corona, hatua za haraka zitachukuliwa lakini hadi sasa wote wanaendelea vizuri na hakuna aliyebainika kuwa na viashiria vya ugonjwa huo.



Sehemu ya wasafiri 84 kutoka nchi ya Afrika Kusini, wakiendelea kupimwa kabla ya kuwekwa karantini kwa muda wa siku 14, katika mpaka wa Tanzania na Zambia, katika Halmashauri ya Mji wa Tunduma, mkoani Songwe jana, kwa ajili ya tahadhari ya maambukizi ya Virusi vya Corona. **PICHA: MANUEL KAMINYOGE**

# Corona yateka mjadala wa Bunge

**Na Mwandishi Wetu**, DODOMA

MJADALA wa makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka ujao wa fedha, umetekwa na hoja ya kupambana na ugonjwa wa homa ya mapafu inayosababishwa na virusi vya corona (Covid 19), wabunge wengi wakitaka kuangaliwe athari za kiuchumi zitakazojitokeza.

Wakichangia mjadala huo juzi na jana bungeni jijini hapa, watunga sheria hao waliitaka serikali kueleza jitihada zaidi za kupambana na ugonjwa huo ili kuepuka athari ambazo tayari zimejitokeza kwenye mataifa makubwa.

Mbunge wa Moshi Mjini (Chadema), Jafari Michael, alishauri jitihada za kudhibiti ugonjwa huo ziendelee ikiwamo kupata fedha kupitia njia yoyote ya kibajeti na ambazo si za kibajeti kukabiliana na mlipuko wa virusi hivyo.

"Fedha hizi zinunue vipimo vya upimaji ili tujue kwa kiwango gani watu wameathirika kwa janga hili, mpaka sasa tunaamini tuna watu wachache sana ambao ni wagonjwa, hatuna uhakika kwa vipimo, inaonekana kuna wagonjwa bado wapo ndani, ni vyema tukapima ili kujua kiwango cha maambukizo na kukabiliana nacho kabla ya kuruhusu kuwa kubwa kwa jamii yetu.

"Vifaa vya kunawia mikono watu walio wengi bado havijawafikia zaidi ya kutumia maji na sabuni, serikali iangalie namna ya kutumia mamlaka za serikali za mitaa, ili wadau mbalimbali wachangie na kuwafikia watu wa chini kwa huduma ya vitakasa mikono," alisema.

Mbunge huyo pia alishauri serikali kuangalia athari za ugonjwa huo kiuchumi, akisema sekta ya utalii itaathirika zaidi kutokana na baa hilo.

"Tunapimaje hiyo hali? Slogan kubwa yetu ni kukusanya kodi, lakini tunatakiwa kukusanya kwa watu wenye uwezo wa kulipa kodi, sasa tunawapunguzie watu mzigo huo?" Alihoji.

Alisema ni vyema serikali ikakaa na wataalamu na kupima athari za kiuchumi, ili kusaidia watu kama ilivyofanyika katika nchi zingine zikiwamo Kenya na Rwanda.

"Na sisi tuangalie hatua za kuchukua ili wafanyabiashara wasiumie na wananchi wasiumie," alisema.

Akichangia mjadala huo, Mbunge wa Iramba Mashariki (CCM), Allan Kiula, alishauri fedha zilizotengwa kwa ajili ya matumizi ya Ofisi ya ya Waziri Mkuu na wizara nyingine, zitumiWe kwenye maeneo muhimu, akiamini kuwa ugonjwa huo utasababisha upatikanaji wa fedha usiwe mzuri.

"Kwa kuwa hatuna hakika kama 'flow' (mtiririko) itakuwa nzuri kama tunavyoona nchi zingine, ni vyema fedha zitakazopatikana, zielekezwe kwenye mambo muhimu, pia kwenye suala la kukaa kwa umbali bado linatupa shida kidogo," alisema.

Mbunge wa Mtambile (CUF), Masoud Abdalah Salim, alisema kuna haja Watanzania wakalitumia baa hilo kutafakari na kuacha dhambi kwa kuwa dunia sasa imesimama kutokana na corona.

"Ni vyema mkakati ukaongezwa zaidi kukabiliana na corona, vitakasa mikono bei zake zimekuwa zikiongezeka siku hadi siku, jambo hili ni kubwa, hakuna vitakasa mikono, elimu na wala barakoa vijijini, serikali iangalie jambo hili," alisema.

Mbunge huyo pia aliitaka serikali iongeze vipimo zaidi vya kuwatambua washukiwa wa ugonjwa huo badala ya kutumia maabara moja tu iliyoko Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

Mbunge wa Kalenga (CCM), Godfrey Mgimwa, alisema ugonjwa huo umesababisha athari za kiuchumi kwenye mataifa yenye uchumi mkubwa na yameshindwa kuuzuia.

"Je, serikali imejipangaje kukabiliana na ugonjwa huu? Ukipita maeneo ya starehe, vijana wapo kuanzia saa moja hadi saa nane usiku, tukishindwa kuzuia maeneo hayo, sijui tutakuwa na hali gani," alilalamika.

Mbunge wa Iringa Mjini (Chadema), Mchungaji Peter Msigwa, alionyesha kutoridhishwa na hotuba ya Waziri Mkuu kuhusu namna alivyozungumzia suala la corona, akisisitiza kuwa haikuelezwa kwa kina.

"Tulisema tupo vitani, lazima tujiandae kwa kiwango kikubwa sana, sipingani na hatua za serikali kwenye suala la kunawa mikono, wenzetu wazungu suala la kunawa mikono ni kawaida yao.

"Kama kukabiliana na corona ni kunawa mikono, tunajidanganya, kuna hatua za kuchukua kama nchi na wabunge tunapaswa kuibana serikali mipango tuliyochukua," alisema.

Waziri Kivuli huyo wa Mambo ya Nje, alisema hoja ya corona ni zaidi ya watu wanavyodhani, akidai hatua zilizochukuliwa na serikali haziendani na tatizo lililopo.

"Wakilipuka wagonjwa 100,000 tutawalaza wapi? Hatuna ICU (chumba cha wagonjwa wanaohitaji uangalizi maalum) za kutosha, serikali mnapaswa kuwa na majibu," alisema.

Mchungaji Msigwa alisema katika sekta ya utalii, zaidi ya watu milioni mbili nchini hawana kazi na kwamba visiwani Zanzibar, hoteli za kitalii 250 zimefungwa kutokana na baa la corona.

"Mapato mtakusanya kutoka wapi? Tunatakiwa kujadili, serikali iseme ina mpango gani ili tushauri, serikali waje na mpango wabunge tushauri, tunachokiona ni visabuni huko barabarani, kuna wafanyabiashara wamekopa benki tunaendaje?" alihoji.

HABARI KITAIFA

# Latra yafungua milango usafiri daladala

**Na Elizabeth Zaya**

MAMLAKA ya Udhibiti Usafiri Ardhini (Latra), imewataka watu binafsi, shule na taasisi zenye mabasi ambayo hayajapangiwa njia kwa ajili ya usafirishaji, kuomba leseni za muda mfupi kwa ajili ya kutoa huduma hiyo katika maeneo ya mijini.

Latra katika taarifa yake kwa umma jana, imeamua kufanya hivyo kwa sababu ya ongezeko la uhitaji wa vyombo vya usafiri wa abiria kutokana na utekekelezaji wa tahadhari dhidi ya ugonjwa wa corona.

"Latra inawataarifu wadau wa usafiri wa umma nchini kuwa kufuatia (kutokana na) utekelezaji wa tahadhari dhidi ya corona, kuna ongezeko la uhitaji wa vyombo vya usafiri wa abiria," ilisema taarifa hiyo.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa kwa wadau watakaoitikia wito huo, watapaswa kufika katika ofisi za Latra zilizo karibu yao wakiwa na kadi za magari.

Taarifa hiyo ya Latra imekuja ikiwa siku moja tu baada ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, kutoa kibali cha usafiri wa pikipiki za miguu mitatu (bajaji) na bodaboda kusafirisha abiria katikati ya jiji hilo.

Alisema lengo la kutoa kibali hicho ni kusaidia kusafirisha abiria ambao watakuwa na uwezo wa kutumia usafiri huo kuwahishwa kazini na kupunguza changamoto iliyopo kwa sasa usafiri inayosababishwa na hatua zinazochukuliwa juu ya tahadhari ya ugonjwa wa corona.

Jumatatu ya wiki hii, agizo la magari za umma kubeba abiria kulingana na idadi ya viti vyake, lilianza kutekelezwa rasmi, hivyo kuongeza changamoto ya usafiri kwa wakazi wa jiji la Dar es Salaam.

Katika vituo vingi vya mabasi vikiwamo vya mwendokasi, foleni ya watu katika dirisha za kukatia tiketi hadi mchakato wa kusafiri kwenda katika maeneo mbalimbali imekuwa kubwa.

Sambamba na hilo, kumekuwa na watu wengi vituoni huku baadhi ya daladala zikiwalazimisha watu kukaa chini na baadhi yao kutumia zaidi za saa tano kuhangaikia usafiri.

## Wachimbaji wadogo nao wadai kuathirika

**Na Anthony Ishengoma,** SHINYANGA

ATHARI za mlipuko wa ugonjwa wa corona zimeanza kuonekana kutokana na wanunuzi wa almasi kutoka vikundi vya wachimbaji wadogo vinavyoendelea na marudio ya makinikia ya mchanga wa madini hayo kuanza kupungua kwa kasi, hivyo wachimbaji hao kushindwa kuuza kwa wakati kama ilivyotarajiwa.

Katibu Mkuu wa Chama cha Wachimbaji Madini Mkoa wa Shinyanga (Shirema), Gregory Kibusi, alisema hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maendeleo ya uchenjuaji wa makinikia ya almasi katika Kijiji cha Msagala wilayani Kishapu, nje kidogo ya mgodi mkubwa wa almasi wa Mwadui.

Kibusi alisema kupungua kwa wanunuzi wa madini hayo kunatokana na wanunuzi wa almasi ndogondogo zenye ukubwa wa punje ya sukari kupatikana nchini India lakini kutokana na nchi hiyo kukumbwa na corona, wanunuzi kutoka nje hasa India hawaji tena.

Kuhusu malalamiko wachimbaji wadogo juu ya ubora wa mchanga huo, Kibusi alisema upatikanaji wa mchanga ambao ni takribani tani milioni moja, utaendelea kutolewa na mgodi kwa kuwashirikisha viongozi wa Shirema na kuwataka wachimbaji hao kuwa na subira.




# Madaktari sasa wapendekeza wagonjwa kupunguzwa vituoni

**Na Gwamaka Alipipi**

CHAMA cha Madaktari Tanzania (MAT), kimependekeza kupunguzwa kwa wagonjwa kwenye vituo vya afya kwa kutoa dawa za muda mrefu ili kupunguza mrundikano utakaosababisha kuenea kwa haraka ugonjwa wa virusi vya corona.

Kimesema wagonjwa wenye maradhi ya kisukari, shinikizo la damu, maumivu mgongo na misuli na mengineyo wanaweza kupewa dawa walau za miezi mitatu kwa sababu makundi hayo yako hatarini kupata ugonjwa huo.

Rais wa MAT, Dk. Elisha Osati, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu ugonjwa wa corona.

Dk. Osati alisema kwa utafiti mdogo walioufanya nchini, wamebaini asilimia 70 ya wagonjwa wanaokwenda kliniki wanafuata dawa, hivyo kuna haja ya kupewa dawa za muda mrefu ili wakae nyumbani, hali itakayosaidia kupunguza msongamano kwenye vituo vya afya.

Aliongeza kuwa hakuna haja kwa wagonjwa wanaohitaji dawa kwenda kliniki mara kwa mara wakati wanaweza kupewa dawa nyingi zitakazowawezesha kukaa nyumbani muda mrefu.

Aidha, aliwataka wananchi kutoa ushirikiano wa wahudumu wa sekta ya afya kwa kufuata maelekezo yanayotolewa, ikiwamo kunawa mikono wakati wote.

"Pia tunapendekeza kupunguza wagonjwa kwenye kliniki zetu kwa kutoa dawa za muda mrefu walau za miezi mitatu, ili kupunguza mrundikano wa wagonjwa kwenye kliniki zetu," alisema Dk. Osati.

Vilevile, aliiomba serikali kuhakikisha kunakuwapo na vifaa vya kujikinga dhidi ya maambukizi ya ugonjwa wa corona kwa wafanyakazi wa afya nchini.

Alisema vifaa kama v mask N95 ni muhimu kwa wafanyakazi wa sekta ya afya kwani wao ndiyo wanaowahudumia wagonjwa, hivyo wasipopata vifaa vya kujikinga, wakatakuwa katika hatari ya kuambukizwa ugonjwa huo.

"Serikali wahakikishe kunakuwapo na vifaa vya kujikingia kwa wafanyakazi, ni muhimu sana kwetu ukizingatia idadi ya wagonjwa na walio katika hatari ya kupata maambukizi ya ugonjwa wa corona inaongezeka siku hadi siku. Hivyo tahadhari ni muhimu sana," alisema Dk. Osati. Alipongeza serikali kwa namna inavyoongoza jitihada kupambana na ugonjwa huo.

Hadi kufikia juzi, taarifa iliyotolewa na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, ilieleza kuwa idadi ya watu walioambukizwa ugonjwa wa corona nchini imefikia 20.



Waombolezaji wakibeba jeneza lenye mwili wa aliyekuwa mtangazaji wa TBC1, Marin Hassan Marin, wakitoka nyumbani kwa marehemu kuelekea katika Msikiti wa Kibweni KMKM, kwa ajili ya kuombea dua na baadaye mazishi yaliyofanyika katika makaburi ya Mwanakwerekwe, mjini Zanzibar jana. **PICHA: OTHMAN MAULID**

# Mbowe apangua Baraza la Mawaziri Kivuli

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

KIONGOZI wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Freeman Mbowe, amefanya mabadiliko katika Baraza lake la Mawaziri ikiwa imebaki takribani miezi mitatu kufika ukomo wa Bunge la 11.

Bunge hilo linatarajiwa kuvunjwa na Rais John Magufuli Juni 30, mwaka huu.

Taarifa ambazo Nipashe ilizipata jana kutoka ndani ya Kambi Rasmi ya Upinzani na kuthibitishwa na baadhi ya mawaziri kivuli, zilieleza kuwa mabadiliko hayo yalifanywa juzi jijini Dodoma.

Baraza hilo lina mawaziri 21 na wote safari hii wametoka Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema).

Mawaziri kivuli ni pamoja na Jaffari Michael (Moshi Mjini) anayekuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Tamisemi, akisaidiwa na Mbunge wa Viti Maalum, Sophia Mwakagenda.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, anakuwa Ruth Mollel ambaye ni waziri pekee asiyekuwa na msaidizi (naibu waziri).

Tunza Malapo (Viti Maalum) atakuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) akisaidiwa na Zainabu Mussa Bakar wakati Esther Bulaya akiendelea kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Ajira na Vijana), akisaidiwa na Frank Mwakajoka, Mbunge wa Tunduma. Wizara ya Kilimo itakuwa chini ya Pascal Haonga, Mbunge wa Mbozi, akisaidiwa na Mbunge wa Viti Maalum, Anatropia Theonest, wakati Wizara ya Mifugo na Uvuvi ikiendelea kuwa chini ya Dk. Immaculate Sware anayesaidiwa na Lucy Mageleli. Katika baraza hilo, Qambalo Qulwi ni Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano akisaidiwa na Suzan Kiwanga, Mbunge Mlimba mkoani Morogoro.

Wizara ya Fedha na Mipango inaendelea kuwa chini ya Halima Mdee, Mbunge wa Kawe, akisaidiwa na Catherine Ruge wakati Wizara ya Nishati sasa inaongozwa na Grace Tendega na Naibu Waziri Jesca Kishoa.

Mbunge wa Tarime Vijijini, John Heche, sasa anakuwa Waziri wa Madini akisaidiwa na Joseph Haule 'Prof Jay' wakati Wizara ya Katiba na Sheria ikiwa chini ya Salome Makamba na Naibu Waziri, Sabrina Sungura.

Wizara ya Maliasili na Utalii inaongozwa na Mch. Peter Msigwa akisaidiwa na Joyce Mukya huku Wizara ya Ulinzi ikikabidhiwa kwa Gibson Meiseyeki na Naibu Waziri Peter Lijualikali.

Wizara ya Mambo ya Ndani na ile ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, zitakuwa chini ya mawaziri Godbless Lema (hajabadilishwa) na Esther Matiko (hajabadilishwa) wakisaidiwa na Rhoda Kunchela na Upendo Peneza, mtawalia.

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, inaongozwa na Wilfred Lwakatare na Naibu Waziri Grace Kiwelu wakati Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji itakuwa chini ya David Silinde aliyehamishwa kutoka Wizara ya Fedha na Mipango alikokuwa Naibu Waziri. Silinde atasaidiwa na Lucy Owenya.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, inaendelea kuwa chini ya Waziri Susan Lyimo akisaidiwa na Yosepher Komba, aliyechukua nafasi ya Birago Kasuku aliyefariki dunia.

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Waziri ni Cecilia Paresso na Naibu Waziri Hawa Mwaifunga wakati Wizara ya Maji ikiwa chini ya Zubeda Sakuru akisaidiwa na Lucy Mlowe huku Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Muchezo ikiendelea kuwa chini ya Joseph Mbilinyi 'Sugu' na Naibu Waziri yule yule Devotha Minja.

# Bunge lataka wasimamizi wa uchaguzi kuwajibishwa

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

BUNGE limeutaka uongozi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kuwawajibisha wasimamizi wa uchaguzi wanapobainika kufanya uzembe unaosababisha madhara katika uchaguzi.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, Mohamed Mchengerwa, alitoa rai hiyo bungeni jijini hapa juzi alipowasilisha taarifa na maoni ya kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka ujao wa fedha.

Alisema kuna haja tume hiyo kufuatilia mienendo ya wasimamizi wake wa uchaguzi na kuchukua hatua dhidi ya wanaobainikia kufanya uzembe na kutozingatia sheria, kanuni na taratibu.

"Kamati inaendelea kushauri kwamba, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ihakikishe inafuatilia wasimamizi wake wa uchaguzi na kuwawajibisha pale wanapofanya uzembe unaosababisha madhara ambayo yangeweza kudhibitiwa mapema na msimamizi aliye makini na anayetambua na kutekeleza wajibu wake kwa mujibu wa sheria," alisema.

Mbunge huyo wa Rufiji (CCM), pia alisema kamati yake imeridhishwa na utekelezaji wa ushauri wake kuhusu uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura kwa uangalifu mkubwa.

Hata hivyo, akasema kamati inaendelea kuishauri NEC kujitahidi kufanya kazi yake kwa weledi ili kuendelea kuaminika kwa wadau wake wa uchaguzi, na hasa kipindi hiki kuelekea Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu.

Alisema kamati yake pia imeridhishwa na jinsi Hazina ilivyotoa fedha kwa wakati kuiwezesha tume kuboresha Daftari la Kudumu la Wapigakura, lakini bado inaendelea kuishauri serikali kuhakikisha inatoa fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa wakati ili kuiwezesha tume hiyo kuratibu masuala mbalimbali ya uchaguzi kwa ufanisi mkubwa.

Amana Bank
*Pamoja, katika njia sahihi*

## Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014
## TAARIFA YA MAHESABU ZILIZOKAGULIWA

**WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 DESEMBA 2019**

| | TZS '000<br>Mwaka wa sasa<br>31 - 12 - 2019 | TZS '000<br>Mwaka uliopita<br>31 - 12 - 2018 |
|---|---|---|
| **A. MALI** | | |
| 1. Fedha Taslimu | 12,308,710 | 10,160,903 |
| 2. Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 18,756,238 | 25,939,729 |
| 3. Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 0 | 0 |
| 4. Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 5,854,327 | 6,405,995 |
| 5. Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 65,494 | 347,225 |
| 6. Miamala Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| 7. Bili Zilizoafikiwa | 0 | 0 |
| 8. Dhima za Wateja Zilizokubalika | 0 | 0 |
| 9. Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 19,223,998 | 17,317,390 |
| 10. Investment in Other securities | 0 | 0 |
| 11. Mikopo Halisi Iliyopo | 162,644,151 | 152,450,514 |
| 12. Mali Nyingine | 9,551,392 | 8,525,746 |
| 13. Uwekezaji wa Hisa | 0 | 0 |
| 14. Akaunti za udhamini | 0 | 0 |
| 15. Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 9,677,365 | 4,348,692 |
| **16. JUMLA YA MALI** | **238,081,675** | **225,496,194** |
| | | |
| **B. DHIMA** | | |
| 17. Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 0 | 0 |
| 18. Amana za Wateja | 190,383,867 | 181,716,729 |
| 19. Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | 0 | 0 |
| 20. Amana Maalumu | 13,170,304 | 14,588,970 |
| 21. Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 0 | 0 |
| 22. Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 110,250 | 136,971 |
| 23. Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 772,342 | 568,447 |
| 24. Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | 0 | 0 |
| 25. Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| 26. Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 97,441 | 296,213 |
| 27. Dhima Nyingine | 6,422,850 | 1,796,202 |
| 28. Madeni | 0 | 0 |
| 29. JUMLA YA DHIMA | 210,957,053 | 199,103,533 |
| **30.MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **27,124,622** | **26,392,661** |
| | | |
| **C. FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31. Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 39,697,089 | 39,697,089 |
| 32. Akiba ya Mtaji | 10,624,547 | 4,160,572 |
| 33. Mapato Yaliyobakizwa | (23,928,976) | (18,081,493) |
| 34.Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 731,962 | 616,493 |
| 35. Akaunti Nyingine za Mtaji | | 0 |
| 36. Stahiki ya Wenyehisa Chache | 0 | 0 |
| **37. JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **27,124,622** | **26,392,661** |
| | | |
| 38. Dhima Zisizo Dhahiri | 13,950,647 | 24,994,424 |
| 39. Mikopo Chechefu | 18,910,750 | 8,290,865 |
| 40. Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 2,167,030 | 1,758,824 |
| 41. Mali Nyingine Chechefu | 0 | 0 |
| | | |
| **D. BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 11.4% | 11.7% |
| (ii) Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 11.5% | 5.4% |
| (iii) Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 81.0% | 78.6% |
| (iv) Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 68.3% | 67.6% |
| (v) Ongezeko la Amana | 3.7% | 10.4% |
| (iv) Ongezeko la Mali | 5.6% | 10.5% |
| | | |

**TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI MWAKA UNAOISHIA 31 DESEMBA 2019**

| | TZS '000<br>Mwaka wa sasa<br>31 - 12 - 2019 | TZS '000<br>Mwaka uliopita<br>31 - 12 - 2018 |
|---|---|---|
| 1. Faida itokanayo na Mikopo | 19,567,061 | 19,430,994 |
| 2. Gawio la Faida kwa waweka Amana | (5,810,968) | (6,646,796) |
| **3. Mapato Halisi ya Faida (1kutoa 2)** | **13,756,093** | **12,784,198** |
| | | |
| 4. Madeni Viza Yaliyofutwa | 0 | 0 |
| 5. Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (208,367) | (339,820) |
| | | |
| **6. Faida isiyotokana na Mikopo:** | **7,273,804** | **7,138,710** |
| 6.1 Faida Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 1,725,884 | 965,903 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 5,528,330 | 6,095,528 |
| 6.3 Gawio | 0 | 0 |
| 6.4 Mapato Mengine | 19,590 | 77,279 |
| | | |
| **7. Gharama za uendeshaji** | **(19,893,488)** | **(18,556,881)** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | (9,256,536) | (8,240,581) |
| 7.2 Ada na Kamisheni | (157,549) | (59,359) |
| 7.3 Gharama Nyingine | (10,479,403) | (10,256,941) |
| | 0 | |
| **8. Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | 928,042 | 1,026,207 |
| 9. Tengo la Kodi ya Mapato | (196,080) | (409,714) |
| | | |
| **10. Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **731,962** | **616,493** |
| | | |
| 11. Idadi ya Waajiriwa | 239 | 218 |
| 12. Mapato kwa Hisa | 18 | 16 |
| 13. Idadi ya Matawi | 9 | 8 |
| | | |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | |
| Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 0.3% | 0.3% |
| Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 2.7% | 2.3% |
| Uwiano wa Gharama za uendeshaji na Mapato Ghafi | 74.1% | 69.8% |
| Uwiano wa Mapato Halisi yatokanayo na Mikopo na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 7.7% | 7.8% |
| | | |
| | | |

**TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA MWAKA UNAOISHIA 31 DESEMBA 2019**

| | TZS '000<br>Mwaka wa sasa<br>31 - 12 - 2019 | TZS '000<br>Mwaka uliopita<br>31 - 12 - 2018 |
|---|---|---|
| I. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji: | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | 928,042 | 1,026,207 |
| -Marekebisho kwa Ajili ya | | |
| Uchakavu Katika Mali | 2,248,697 | 1,244,658 |
| Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | 0 | 0 |
| Gharama za kifedha | 415,758 | 0 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (10,449,554) | (22,615,740) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 7,248,471 | 18,377,338 |
| - Mabadiliko ya kiwango kinachohitajika na banki kuu kisheria | 1,713,306 | (1,015,873) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (155,424) | 438,676 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 118,552 | (1,632,856) |
| - Kodi Iliyolipwa | (112,828) | (72,450) |
| - Mengineyo (bainisha) | 0 | 0 |
| **I: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | **1,955,020** | **(4,250,040)** |
| | | |
| **II: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji** | | |
| Gawio Lililopokewa | 0 | 0 |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (1,754,341) | (2,510,798) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | (1,107,000) | (370,048) |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | 0 | 0 |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | 0 | 0 |
| Marekebisho katika mali za Kudumu | 0 | 0 |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(2,861,341)** | **(2,880,846)** |
| | | |
| **III. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha** | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | 0 | 0 |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | 0 | 3,999,809 |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | 0 | 0 |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | 0 | 0 |
| Mengineyo (bainisha) | (1,061,117) | 0 |
| Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha | (1,061,117) | 3,999,809 |
| | | |
| **IV. Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu** | | |
| Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | (1,967,438) | (3,131,077) |
| | | |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu kwa Mwaka | 44,267,838 | 47,398,915 |
| | | |
| **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Mwaka** | **42,300,400** | **44,267,838** |
| | | |
| | | |
| | | |

**TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 DESEMBA 2019**

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mwaka wa sasa 2019 | | | | | | | |
| | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **39,697,089** | 0 | **(17,465,000)** | **2,843,597** | **1,316,975** | 0 | **26,392,661** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | 0 | 0 | 731,962 | 0 | 0 | 0 | 731,962 |
| Share zilizouzwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Miamala na wanahisa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Gawio lililolipwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Ziada ya Kisheria | 0 | 0 | (7,780,951) | 7,780,950 | - | 0 | (1) |
| Tengo la Ziada ya Jumla | 0 | 0 | 1,316,975 | 0 | (1,316,975) | 0 | 0 |
| Mengineyo | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Salio la mwisho wa mwaka wa sasa** | **39,697,089** | 0 | **(23,197,014)** | **10,624,547** | 0 | 0 | **27,124,622** |
| | | | | | | | |
| Mwaka Uliopita 2018 | | | | | | | |
| | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa Mwaka | | | | | | | |
| Tengo la Ziada ya kihuasibu (IFRS 9) | **35,697,280** | 0 | **(16,686,216)** | **3,451,838** | **1,263,376** | 0 | **23,726,278** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | | | (1,949,919) | 0 | 0 | 0 | (1,949,919) |
| Share zilizouzwa | 0 | 0 | 616,493 | 0 | 0 | 0 | 616,493 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | 3,999,809 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3,999,809 |
| Miamala na wanahisa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Gawio lililolipwa | 0 | 0 | - | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Ziada ya Kisheria | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Tengo la Ziada ya Jumla | 0 | 0 | 608,24 | (608,241) | 0 | 0 | 0 |
| Mengineyo | 0 | 0 | (53,599) | 0 | 53,599 | 0 | 0 |
| **Salio la mwisho wa mwaka uliopita** | **39,697,089** | 0 | **(17,465,000)** | **2,843,597** | **1,316,975** | 0 | **26,392,661** |

Dondoo za hapo juu zimetokana na Mahesabu ya Benki kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba 2019 ambazo zimetayarishwa kwa kuzingatia kanuni za kihasibu za IFRS, kanuni za kisharia pamoja na vifungu vya Sheria ya Makampuni ya Mwaka 2002. Mahesabu haya yalikaguliwa na kampuni ya Ukaguzi ya KPMG na kupata hati safi.

Taarifa za mahesabu hapo juu zimeidhinishwa na bodi ya wakurugenzi na kutiwa saini kwa niaba yao na wajumbe tajwa hapo chini:

**Abdallah Nahdi**
(Mkurugenzi) Machi 31, 2020

**Dr. Muhsin Salim Masoud**
(Mkurugenzi Mtendaji) Machi 31, 2020




215688102

Amana Bank
Pamoja, katika njia sahihi
Mobile Banking
Chukua tahadhari na virusi vya Corona
Epuka msongamano wa watu
Pata huduma za kibenki hapo ulipo
Kuhamisha pesa na Kufanya malipo ya huduma mbalimbali
Kwa Maelezo zaidi, wasiliana nasi kupitia Huduma kwa Wateja 0657 980 000 0657 980 000 /amanabanktz /amanabank

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Bodaboda, bajaji sawa katikati jiji Dar, lakini...

**JUZI** Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, alitangaza kutengua zuio la usafiri wa pikipiki za magurudumu matatu yaani bajaji na za magurudumu mawili yaani pikipiki kufika katikati ya Jiji, ili kuwezesha wananchi wengi kutumia huduma hiyo.

Uamuzi huyo ulikuja siku chache baada ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini (Latra), kuelekeza magari yote kupakia abiria kulingana na idadi ya viti vilivyopo.

Baada ya kuanza utekelezaji huo, abiria wengi walionekana kujaa vituoni, huku baadhi wakilazimishwa kukaa sehemu ya katikati na wengine wakisafiri kwa nauli mara mbili.

Aidha, baadhi ya wamiliki wa magari binafsi walipakiza abiria na kuwatoza fedha za nauli; yote hayo yakitokana na katazo la mikusanyiko na kubanana kwenye vyombo vya usafiri kama namna ya tahadhari ya kujikinga na maambukizi ya homa ya mapafu inayosababishwa na virusi vya corona.

Mabadiliko hayo yalikwenda hadi kwenye usafiri wa treni, ambapo abiria wametakiwa kukaa kulingana na idadi ya viti vilivyopo, huku kwenye mwendokasi abiria wakikaa kwenye viti na wengine kusimama kulingana na idadi ya viti vya kushikilia.

Uamuzi wa Makonda ni mzuri kwa kuwa unakwenda kuwapa watu ambao walikosa usafiri na kulazimika kutembea kwa miguu kwa umbali mrefu. Mbali ya kutembea umbari mrefu, pia walikuwa wakilazimishwa kulipa nauli ambayo ni zaidi kuliko elekezi pamoja na kuchelewa kufika kazini na sehemu za biashara.

Hata hivyo, pamoja na lengo hilo zuri la serikali, lakini tunatahadharisha kuwa suala hili lichukuliwe kwa tahadhari kubwa na waendeshaji wa pikipiki na bajaji, kwa kuwa wengi huwa ni wakaidi wa sheria, taratibu na kanuni za usalama wa barabarani, ikiwamo kufanya vurugu.

Mathalani, kwenye makutano ya barabara zenye taa wengi hukaidi kusubiri taa ziwaruhusu, badala yake hujiamulia kupita kwa kadri macho yao yanavyowaridhisha kisha hupita, jambo ambalo huwaingiza kwenye matatizo makubwa, ikiwamo kusababisha ajali au kugongwa. Matatizo wanayokumbana nayo ni ajali ambazo hugharimu maisha yao na ya abiria wanaowabeba.

Ni jambo lililo wazi kuwa waendeshaji wengi wa usafiri huo ni vijana, ambao wakati mwingine huwa na mihemko, ikiwamo matumizi ya vilevi kiasi cha kuendesha ovyo bila kujali sheria na alama za barabarani. Baadhi ya madereva hao wamekuwa wakituhumiwa kuhusika katika vitendo vya uhalifu vikiwamo kupora abiria wakiwa wamesimama kwenye vituo au wakiwa wanatembea barabarani, na wengine kutumia mbinu ya kugonga magari ya watu ili aliyepo ndani ateremke na akifanya hivyo basi huishia kumuibia.

Kwa ujumla, ni vitendo ambavyo vimeshusha hadhi na uaminifu wa madereva hao hususan wa bodaboda kiasi cha kutoaminika na kuonekana, wahalifu, wasumbufu na wanaosababisha majanga barabarani. Pia, tunatambua kuwa wapo madereva wa magari ambao huwaonea kwa kuwachomekea na kusababisha ajali, lakini matukio hayo si mengi ikilinganishwa na matukio ya ajali zinazosababishwa na pikipiki pamoja na bajaji.

Tunashauri madereva hao kuheshimu na kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za usalama barabarani ili katika siku za baadae mamlaka husika ziwape vibali vya kusafirisha abiria kwenda na kutoka katikati ya Jiji la Dar es Salaam.

Kwa upande mwingine, tunalishauri Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani kuhakikisha wanawasimamia vyema na kuchukua hatua kali dhidi ya watakaokaidi sheria na kuwa chanzo cha usumbufu.

Tunashauri hivyo kutokana na uzoefu wetu kuwa madereva bodaboda ni rahisi kupenya kokote wakati wowote, na ndiyo maana imekuwa ngumu sana kuwakamata kwa kuwa wao hawasimami kwenye taa, na wanapenya kokote ambako gari au bajaji haziwezi kupenya.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com





Na Beatrice Moses

## Muungwana Lazima Nilonge

# Corona itukumbushe malezi ya pembetatu

**SERIKALI** ilitangaza kufunga shule za awali, msingi na sekondari kwa siku 30 kuanzia Machi 17, ikiwa ni sehemu ya kuikabili Corona

Ni hatua ya ghafla, iliyotangazwa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa.

Ni uamuzi ambayo katika mazingira yake, haukuwa na muda wa kujiandaa, hata uongozi wa shule mbalimbali zikiwapo binafsi hawakumudu kutoa kazi za masomo kwa wanafunzi wawapo likizo.

Waziri Mkuu alitangaza hatua, siku moja baada ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kutangaza kubainika uwepo wa mgonjwa wa corona nchini hapa.

Ratiba ya kitaifa, ilionyesha wanafunzi wa kidato cha sita walipaswa kuanza mitihani Mei 4, mwaka huu, hivyo wameahidiwa kutangaziwa utaratibu mwingine, kulingana na hali iliyoko nchini.

Kwa kuwa ni hatua ya ghafla, ni wazi uongozi wa shule, wazazi na wanafunzi husika hawakuwa wamejiandaa, hakuna wa kumlaumu, Sote tuna ushuhuda kupitia vyombo vya habari, vikiwamo vya kimataifa, corona inavyoathiri hapa kwetu, hadi jana imeshawagusa watu 20, kati yao mmoja kishatangulia mbele ya haki na wawili wamepona.

Nakumbuka siku hiyo, walimu hasa wa shule za bweni, walihaha kuhakikisha wanafunzi wanaondoka kurejea nyumbani kwao wakiwa salama. Wazazi nao walijitahidi kuhakikisha wanatuma nauli kwa watoto wasafiri salama.

Walio hasa katika madarasa ya kujiandaa ana mitihani, kwa maana ya mitihani ya taifa, yaani la nne, saba, kidato cha pili, nne na sita walihitaji kujua hatma ya maandalizi yao.

Chama Cha Walimu Tanzania (CWT), kwa kushirikiana na asasi ya HakiElimu, walifanya utafiti kati ya Septemba 2003 na Desemba, mwaka 2003 kuhusu maisha na mazingira ya kazi ya walimu katika wilaya saba nchini na walipata mawazo na mtazamo wa walimu kuhusu uhalisia wa maisha yao.

Nikiwa ni miongoni wa wazazi, siku hiyo ya tangazo nilijikuta nakumbuka umuhimu wa malezi ya pembe tatu kwenye sekta ya elimu; mzazi au mlezi, mwalimu na mwanafunzi husika.

Kwani, hayo yote niliyotaja hapo juu yalifanikiwa kwa wazazi walikuwa na ushirikiano mzuri wa walimu, kwa kuwasiliana nao ili kutuma nauli.

Pia, baadhi ya walimu walitambua umuhimu wa kutoa maelekezo kwa wazazi jinsi ya kuwasaidia wanafunzi waliopo kwenye maandalizi ya mitihani ya taifa.

Kutokana na teknolojia ya mawasiliano, baadhi ya shule zina makundi ya mitandao ya kijamii (whatsApp) ilitumika katika kuweka mambo sawa.

Baadhi ya walimu walikumbuka kuhamasisha watoto kujisomea vitabu vya masomo mbalimbali kwa mujibu wa mwongozo wa shule husika, wakizingatia mtaala iliyotolewa na Wizara ya Elimu.

Kuna wazazi au walezi walioupuuza malezi ya pembe tatu, hali inayosababisha usumbufu kwa watoto, kutokana na likizo hiyo ya ghafla.

Wapo ambao hawazingatii maagizo yanayotolewa na walimu, ikiwamo kununua vitabu vinavyohitajika, ambavyo sasa ndiyo vinatumiwa na watoto kujisomea nyumbani.

Wapo ambao wamekuwa na visingizio vya kutokuwa na uwezo (fedha) kununua vitabu hivyo, lakini baadhi yao wakiwafuatilia, ni hodari wa matumizi ya mengine uasiyio na tija. Wazazi kukwepa malezi ya pembe tatu, ni jambo linalolipigiwa kelele na viongoni wa serikali, hata taasisi binafsi kama CWT na wadau wenza, HakiElimu.

Matokeo ya utafiti yalilenga kuchangia mijadala mbalimbali ya serikali, kuhusu uboreshaji hali ya walimu kwa lengo la kuinua kiwango cha elimu kinachotolewa nchini.

Utafiti huo, pamoja na mambo mengine uliangalia nyanja zinazochangia ama kuboresha au kudidimiza hali ya maisha na kazi ya walimu, pia mzigo wa kazi ya ufundishaji.

Mengine ni uwiano stahiki wa wanafunzi kwa mwalimu kila mmoja, maendeleo ya walimu kitaalamu katika kufundisha na kujifunza, maisha na walimu maslahi yao,

Ni utafiti huo uliobainisha kuwepo kwa umuhimu wa ushirikiano kati ya shule na wazazi, ni muhimu sana katika kujenga misingi bora ya maendeleo kwa watoto.

Ilibainishwa kuwa, muungano mzuri wa wazazi na walimu, umeweza kukuza maendeleo ya shule kitaaluma katika shule zilizo na ushirikiano wa karibu na wazazi na pale penye wazazi wenye mtazamo tofauti, zimekuwa zikilega kwa miaka mingi.

Kwa hiyo kupitia likizo hii iliyotokana na janga la ugonjwa corona, iwashitue wazazi na walezi waliokuwa mbali na majukumu yao kutoa ushirikiano, wakumbuke majukumu ya msingi, kama vile kununua vitabu vya watoto na kuwasiliana na walimu, wapate taarifa za maendeleo ya watoto zao.

# Kubenea ataka hatua zaidi kudhibiti corona

**Na Romana Mallya**

MBUNGE wa Ubungo, Said Kubenea, amesema tahadhari zinazochukuliwa dhidi ya mikusanyiko hazitoshi na kupendekeza kama maambukizi yataongezeka hata Bunge lisimamishe kwa muda vikao vinavyoendelea.

Kubenea alitoa mapendekezo hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu tahadhari zinazotolewa huku mitaani kukiendelea kuwako kwa mikusanyiko.

“Mikusanyiko yote ya ibada na mazishi ni muhimu ikapunguzwa.

Hii marufuku itatusaidia ili kupunguza maambukizi na tusijione sisi ni kisiwa. Bunge linaendelea Dodoma, ninamshukuru Spika wa Bunge, Job Ndugai kwa hatua alizochukua.

“Amefanya Bunge tushiriki wachache ili kupunguza maambukizi. Spika ametumia mamlaka aliyonayo kikatiba kulinda wabunge na wafanyakazi,” alisema.

Hata hivyo, alisema hiyo haitoshi kwa sababu mbunge anaweza akawa ametoka kwenye shughuli za kijamii, akaingia bungeni na kusababisha kuenea maambukizi.

“Kama huu ugonjwa utaendelea ni vizuri bunge likafungwa. Tusione shida kusitisha shughuli za Bunge kwa ajili ya kuokoa maisha ya watu.

“Tuangalie hali tuliyonayo sasa. Kama maambukizi yatakuwa makubwa ni vyema Bunge likajitazama, kujitafakari na hiki ndicho chombo kikuu kwa Jamhuri ya Muungano kwa niaba ya wananchi,” alisisitiza.

Kubenea alisema Bunge linaweza kutafuta njia bora zaidi ya kupitisha bajeti na shughuli za serikali zikaendelea na kulisimamisha kwa muda na baadaye wabunge wakaitwa kwenda kuangalia mambo mengine.

Pia alisema Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) anayo mamlaka ya kuagiza fedha zitumike bila Bunge kukutana halafu baadaye wakaenda kuidhinisha.

Alisema licha ya corona kuendelea kuua maelfu ya watu duniani, juzi ameshuhudia jimboni kwake wananchi katika kituo cha Kimara wakiwa kwenye mkusanyiko mkubwa wakisubiri daladala.

“Marekani jana (juzi) wamesema wanategemea kufikia vifo 100,000 hadi 240,000 kwa wiki tatu zinazokuja. Mkurugenzi (Mkuu) wa Shirika la Afya Duniani (WHO) amesema vifo vinatarajia kufikia hadi watu milioni moja katika wa wiki chache zijazo.

“Kuna hatari ya kiafya katika nchi zilizoendelea duniani, sisi hapa tunazembea. Likilipuka hapa tutakuaje? kufanya mzaa bila kuwa makini hapana,” alisema.

**AWEKA MSIMAMO**

Kuhusu Mbunge wa Moshi vijijini, Anthony Komu, kutangaza kujiondoa Chama cha Demokrasia Maendeleo (Chadema) huku kukiwako maneno na yeye atafanya hivyo, Kubenea alisema wao ni marafiki lakini si kila anachokifanya Komu na yeye atakifanya.

“Bado ni mbunge wa chadema na ninadhani ninahitaji kutumikia wananchi wangu mpaka nitakapoondoka. Bado nipo watu waache kupiga ramli, waache tufanye kazi. Muda ukifika tutayazungumza haya mambo kwa ujumla wake,” alisema.

Kuhusu madai ya vijana wa Chadema kumshambulia mtandaoni, alisema hiyo ni mihemko na kueleza kuwa yawezekana ni makundi yanayoibuka kwenye chama hasa kipindi cha kuelekea uchaguzi.


**Canara Bank (Tanzania) Ltd.**
(Together we can build a better life)

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA ZILIZOKAGULIWA KWA UMMA

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

### WARAKA MIZANIA ULIOKAGULIWA KWA TAREHE 31 DESEMBA 2019 *(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | | Mwaka wa Sasa 31 Desemba 2019 | Mwaka Uliopita 31 Desemba 2018 |
|---|---|---|---|
| A | **ASSETS** | | |
| | 1 Fedha Taslimu | 405.33 | 719.43 |
| | 2 Salio katika Benki kuu ya Tanzania | 6,601.31 | 4,527.67 |
| | 3 Uwekezaji katika Amana za serikali | 25,371.80 | 22,747.45 |
| | 4 Salio katika Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 668.44 | 753.75 |
| | 5 Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 67.32 | 93.33 |
| | 6 Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| | 7 Bili zilizoafikiwa | - | - |
| | 8 Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| | 9 Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 36,866.46 | 36,081.44 |
| | 10 Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| | 11 Mikopo Halisi Iliyopo | 35,634.01 | 34,855.70 |
| | 12 Mali Nyingine | 838.23 | 1,553.62 |
| | 13 Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| | 14 Akaunti za udhamini | - | - |
| | 15 Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 1,556.18 | 946.37 |
| | **16 JUMLA YA MALI** | **108,009.07** | **102,278.77** |
| B | **DHIMA** | | |
| | 17 Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 32,500.00 | 37,602.23 |
| | 18 Amana za Wateja | 37,399.46 | 28,960.70 |
| | 19 Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| | 20 Amana Maalumu | - | - |
| | 21 Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| | 22 Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | 7.51 |
| | 23 Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 1,302.99 | 1,099.74 |
| | 24 Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| | 25 Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| | 26 Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | - |
| | 27 Dhima Nyingine | 839.34 | 113.62 |
| | 28 Madeni | - | - |
| | **29 JUMLA YA DHIMA** | **72,041.79** | **67,783.80** |
| | **30 MALI/(DHIMA) HALISI** *(16 kutoa 29* | **35,967.28** | **34,494.97** |
| C | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| | 31 Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 32,830.00 | 32,830.00 |
| | 32 Akiba ya Mtaji | 828.58 | 539.29 |
| | 33 Mapato Yaliyobakizwa | 836.39 | 234.14 |
| | 34 Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 1,472.31 | 891.54 |
| | 35 Akaunti Nyingine za Mtaji | - | - |
| | 36 Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| | **37 JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **35,967.28** | **34,494.97** |
| | 38 Dhima Zisizo Dhahiri | 10,781.42 | 4,495.24 |
| | 39 Mikopo Chechefu | 4,125.84 | - |
| | 40 Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 162.90 | 101.27 |
| | 41 Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| D | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| | (i) Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 33.30% | 33.73% |
| | (ii) Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 11.49% | 0.00% |
| | (iii) Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 51.14% | 52.49% |
| | (iv) Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 33.24% | 34.16% |
| | (v) Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 91.23% | 92.33% |
| | (vi) Ongezeko la Amana | 5.01% | 47.04% |
| | (vii) Ongezeko la Mali | 5.60% | 28.70% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI ILIYOKAGULIWA KWA MWAKA UNAYOISHIA TAREHE 31 DESEMBA 2019

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | Mwaka wa Sasa 31 Desemba 2019 | Mwaka Uliopita 31 Desemba 2018 |
|---|---|---|
| 1 Mapato ya Riba | 8,167.40 | 6,724.39 |
| 2 Gharama za Riba | 2,802.03 | 2,125.40 |
| **3 Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **5,365.37** | **4,598.99** |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 61.62 | 64.74 |
| **6 Mapato Yasiyo ya Riba** | **895.68** | **672.27** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 137.86 | 80.74 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 757.82 | 591.53 |
| 6.3 Gawio | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | - | - |
| **7 Gharama Zisizo za Riba:** | **4,048.32** | **3,930.59** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | 1,447.60 | 1,263.13 |
| 7.2 Ada na Kamisheni | - | - |
| 7.3 Gharama Nyingine | 2,600.71 | 2,667.46 |
| **8 Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **2,151.12** | **1,275.93** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | 678.81 | 384.39 |
| **10 Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **1,472.31** | **891.54** |
| 11 Idadi ya Waajiriwa | 23 | 19 |
| 12 Mapato kwa Hisa | 45 | 27 |
| 13 Mapato kwa Hisa | 45 | 27 |
| **14 Idadi ya Matawi** | 1 | 1 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | |
| (I) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 1.40% | 0.98% |
| (II) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 4.18% | 2.62% |
| (III) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 44.24% | 53.14% |
| (IV) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 5.56% | 5.55% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA ILIYOKAGULIWA KWA MWAKA 31 Desemba 2019 *(Kiasi kwa shilingi milioni )*

| | | Mwaka wa Sasa 31 Desemba 2019 | Mwaka Uliopita 31 Desemba 2018 |
|---|---|---|---|
| I | **Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za uendeshaji:** | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | 1,472.31 | 891.54 |
| | Marekebisho kwa ajili ya: | | - |
| | Hasara katika mali | 1,300.77 | 1,125.57 |
| | -Badiliko halisi katika Mikopo | (842.93) | (16,071.01) |
| | Faida/Hasara kwenye mauzo ya Mali | - | 3.38 |
| | Mabadiliko halisi katika Amana | 3,336.53 | 21,294.79 |
| | Mabadiliko halisi katika Amana za muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - |
| | Mabadiliko halisi katika dhima nyingine | 794.93 | 1,025.35 |
| | Mabadiliko Halisi katika mali nyingine | (931.66) | (451.09) |
| | Kodi iliyolipwa | (612.79) | (390.00) |
| | Mengineyo(bainisha) | - | - |
| | **Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **4,517.15** | **7,428.52** |
| II | **Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za uwekezaji:** | | |
| | Gawio lililopokewa | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za kudumu | (19.39) | (97.93) |
| | Mapato kutokana na mauzo ya mali za kudumu | - | - |
| | Ununuzi wa Amana zilizoshughulikiwa na Mawakala | 978.16 | (1,571.24) |
| | Mapato kutokana na mauzo ya Amana zilizoshugulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Mengineyo(bainisha) | - | - |
| | **Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uwekezaji** | **958.77** | **(1,669.18)** |
| III | **Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za kifedha:** | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato kutokana na utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha taslimu | - | - |
| | Mabadiliko halisi katika Madeni Mengine | - | - |
| | Mengineyo(Malipo ya dhima za kukodishwa-IFRS 16) | (346.31) | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za kifedha** | **(346.31)** | **-** |
| IV | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha taslimu** | | |
| | Ongezeko/Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | 5,129.61 | 5,759.35 |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa mwaka | 43,240.26 | 37,480.91 |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa mwaka** | **48,369.87** | **43,240.25** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI ILIYOKAGULIWA KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 DESEMBA 2019

(Kiasi kwa shilingi milioni )

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya kisheria | Tengo la Ziada ya jumla | Mengineyo (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 2019** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka wa sasa** | **32,830.00** | - | **1,125.67** | **45.93** | **493.37** | - | **34,494.97** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | **1,472.31** | - | - | - | **1,472.31** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (782.65) | 782.65 | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | 493.37 | - | (493.37) | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka wa sasa** | **32,830.00** | - | **2,308.69** | **828.58** | - | - | **35,967.28** |
| **Mwaka Uliopita 2018** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka uliopita** | **32,830.00** | - | **289.00** | - | **510.00** | - | **33,629.00** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 891.54 | - | - | - | 891.54 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (45.93) | 45.93 | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | 16.63 | - | (16.63) | - | - |
| Mengineyo | - | - | (25.57) | - | - | - | (25.57) |
| **Salio la mwisho wa mwaka uliopita** | **32,830.00** | - | **1,125.67** | 45.93 | **493.37** | - | **34,494.97** |

**BAADHI YA MAELEZO**
**KWA MWAKA UNAOISHIA 31 DISEMBA 2019**

Katika kuandaa taarifa za hizi za fedha,sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita(kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha mwaka wa sasa,mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8)

| Jina | Cheo | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|
| T R BALAJI RAO | Ofisa Mtendaji mkuu | (Imesainiwa) | 30-03-2020 |
| FADHILI PETRO SANGA | Mkuu wa fedha | (Imesainiwa) | 30-03-2020 |
| FREDRICK HIPPOLITE | Mkaguzi mkuu wa ndani | (Imesainiwa) | 30-03-2020 |

**Sisi tuliotajwa hapo chini wajumbe wa bodi ya wakurugenzi tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu,tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 na zinaonesha hali halisi.**

| Jina | Cheo | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|
| 1. M VENKATA RAO | MWENYEKITI WA BODI | (Imesainiwa) | 30-03-2020 |
| 2. RAJABU SELEMANI KAKUSA | MJUMBE WA BODI | (Imesainiwa) | 30-03-2020 |

**Canara Bank (T) Ltd**
**Head Office Dar Es Salaam Branch**
**Elia Complex P.O. Box 491, Dar Es Salaam, Tanzania**
**E:mail ctbl@canarabank.co.tz, T +255 222112530 (D) +255 222112532**
**www.canarabank.co.tz**

215688701



Fundi akimwagilia maji kwenye linta ya moja ya majengo ya hospitali ya kijiji cha Mkirira, Kata ya Nyegina, Musoma Vijijini mkoani Mara jana, ambayo inapanuliwa ili kuweka wodi ya mama na mtoto, huku Mbunge Prof. Sospeter Muhongo akiwa amechangia mifuko 200 ya saruji. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Viongozi wadaiwa kugoma kupimwa corona

**Na Ashton Balaigwa,** KIGOMA

WAKATI serikali ikiendelea kupambana na ugonjwa wa homa ya mapafu nchini inayosababishwa na virusi vya corona (Covid 19), baadhi ya viongozi wa vyama na serikali wamelalamikiwa kugoma kushuka kwenye magari wanaposimamishwa kwa ajili ya kupimwa joto la mwili.

Mhudumu wa Afya ngazi ya Jamii, Issa Lukangamila, alisema hayo kwenye barabara kuu inayounganisha kati Tanzania, Burundi, Rwanda wakati akizungumza kwenye kizuizi cha barabara ya Wilaya ya Uvinza, kilichowekwa kwa ajili ya kupima joto na kunawa mikono kwa sabuni na vitakasa mikono kabla ya kuingia Mkoa wa Kigoma.

Kutokana na hali hiyo alishauri elimu iendelee kutolewa kwa viongozi hao ambao hawako tayari kupimwa mpaka walazimishwe kufanya hivyo na watumishi mwingine huondoa magari yao kwa nguvu.

"Magari ya serikali yanapita hapa, maofisa wanakataa kushuka na kupima kwetu hiyo ni changamoto tunaomba serikali wahamasishane ili watu hao wasimame na kupima badala ya kuamrishwa kupimwa. Ni vizuri kutekeleza agizo la rais," alisema. Alisema tangu alivyoanza kupima Machi 22, mwaka huu, hajapatikana mgonjwa hata mmoja na kazi hiyo inaendelea kwa kuwa magari yanayotokea Mpanda, Kigoma, Kasulu, Mwanza na Dar es Salaam, pia yanayoanzia Uvinza kwenda Kigoma yote yanapimwa.

Wakati viongozi wengine wakigoma kupimwa joto la mwili ili kujua kama wana maambukizi hayo, Mwenyekiti wa Chama cha NCCR-Mageuzi, James Mbatia, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), Dk. Yohana Budeba pamoja na Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dk. Geoffrey Mkamilo walipimwa na kuendelea na safari zao.Mbatia alisema ugonjwa huo ni kati ya majanga ambayo yamesababishwa na kiburi cha wanadamu kwa kutokutekeleza masharti na maelekezo yanayotolewa na wataalamu.

"Shirika la Afya Duniani lilipotangaza ni janga la kidunia Machi 11, mwaka huu hatua mbalimbali zinazoendelea kuchukuliwa zimeleta tija ili maambukizi haya yasizidi na kuna taarifa virusi vinaweza kukaa hewani kwa muda wa saa nane, tuangalie namna ya kuweka dawa na watu kutekeleza ya msingi wanayoelekezwa kabla hatujazembea ikawa kubwa zaidi," alisema Mbatia.

Alisema vijana wana jeuri ya kusema kuwa wao ni rika ambalo haliwezi kupata maradhi hayo jambo ambalo sio kweli kwa kuwa maradhi hayo yanaweza kumpata yoyote.

Mwenyekiti TARI, Dk. Budeba, alisisitiza kwa vituo vyote 17 vya utafiti nchini kuzingatia kanuni za afya kwa kuwa wanahitaji wakulima na watafiti wawe na afya bora ili waendeleze shughuli za kiuchumi. Alisema bila kuwa na afya bora watafiti watashindwa kuendeleza shughuli za kitafiti na kilimo katika nchi.

Alisema hayo wakati akiendelea na ziara anayoifanya mkoani Kigoma ya kutembelea maeneo ya uzalishaji na usambazaji wa mbegu na miche ya michikichi mkoani humo.

Alitaka Watanzania wasifanye mzaha katika kutekeleza kanuni hizo kwa kuwa janga ni kubwa halihitaji mzaha.

Naye Dk. Mkamilo, aliwataka Watanzania kujihadhari na ugojwa huo ambao viongozi wameendelea kuhamasisha jamii.


## NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kampuni ya **WANGWANA AUCTION MART,KOTI BROTHERS LTD NA ADILI AUCTION MART** kwa niaba ya AccessBank Tanzania Limited watauza kwa njia ya mnada wa hadhara, Nyumba, na Viwanja vilivyowekwa kama dhamana ya mikopo ambapo wateja husika wameshindwa kulipa mikopo yao kwa mujibu wa mikataba husika. Hivyo basi ifahamike kuwa utakapopita muda wa siku kumi na nne tangu kutoka kwa gazeti hili,Dhamana husika zitauzwa kwa njia ya mnada . Mnada utafanyika sehemu nyumba na viwanja husika vilipo siku na tarehe kama vilivyotajwa kwenye jedwali hapo chini.

| S/N | TAWI HUSIKA | KAMPUNI INAYO HUSIKA | JINA LA MTEJA | JINA LA MWENYE DHAMANA | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | KIJITONYAMA | WAUNGWA NA AUCTION MART | MASAIGANAH/S,MWAJUMA | MASAIGANAH/S,MWAJUMA | NYUMBA NA KIWANJA | MLINGOTINI | 16/04/2020 SAA 4:ASUBUHI |
| 2 | KIJITONYAMA | WAUNGWA NA AUCTION MART | TARAZO/S, MOHAMED | TARAZO/S,MOHAMED | NYUMBA | VISIGA | 16/04/2020 SAA 4:00ASUBUHI |
| 3 | KIJITONYAMA | WAUNGWA NA AUCTION MART | KIGODA/ABBASS,KIGODA | KIGODA/ABBASS, KIGODA | GUEST HOUSE | VIGWAZA | 18/04/2020 SAA 4:00 ASUBUHI |
| 4 | KIJITONYAMA | WAUNGWA NA AUCTION MART | SANGA/LAMECK,JOVIN | SANGA/LAMECK,JOVIN | KIWANJA | CHANIKA | 17/04/2020 SAA 4:00 ASUBUHI |
| 5 | KIJITONYAMA | WAUNGWA NA AUCTION MART | MAGENDO/JOHN,DOROPHINA | MAGENDO/ JOHN,DOROPHINA | NYUMBA | KIMARA KILUNGULE | 20/04/2020 SAA 4:00 ASUBUHI |
| 6 | KIJITONYAMA | WAUNGWA NA AUCTION MART | DACHI/J,SOPHIA | DACHI/J,SOPHIA | NYUMBA | KILUVYA | 21/04/2020 SAA 4:00 ASUBUHI |
| 7 | KIJITONYAMA | WAUNGWA NA AUCTION MART | MASONU/JOSEN,JUDICA | MASONU/JOSEN,JUDICA | NYUMBA | KIMARA | 22/4/2020 SAA 4:00 ASUBUHI |
| 8 | LUMUMBA | ADILI AUCTION MART | MATORO/ ORERO,DENNIS | MATORO/ORERO, DENNIS | NYUMBA | KIGAMBONI | 18/04/2020 SAA 04:00 ASUBUHI |
| 9 | TEMEKE | KOTI BROTHERS | BEBWA/LUDOVICK,ANECTUS | BEBWA/LUDOVICK,ANECTUS | KIWANJA | SALASALA | 17/04/2020 SAA 4:00 ASUBUHI |
| 10 | LUMUMBA | WAUNGWA NA AUCTION MART | KIWILE/ALLY,NEEMA | KIWILE/ALLY,NEEMA | NYUMBA | BUGURUNI | 18/04/2020 SAA 04:00 ASUBUHI |
| 11 | LUMUMBA | WAUNGWA NA AUCTION MART | MOHAMED /ABDALLAH,SALUMU | MOHAMED/ABDALLAH,SALUMU | NYUMBA | KIMARA SARANGA | 21/04/2020 SAA 04:00 ASUBUHI |
| 12 | LUMUMBA | WAUNGWA NA AUCTION MART | MUOMBWA/MOHAMEDI,RAJABU | MUOMBWA/MOHAMEDI,RAJABU | NYUMBA | TEMEKE | 23/04/2020 SAA 04:00 ASUBUHI |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Ukaguzi unaruhusiwa mara usomapo tangazo hili.
2. Mnunuzi atalazimika kulipa malipo ya 25% ya fedha taslimu papo hapo na 75% baada ya siku 14 toka siku ya mnada kufanyika na ukishindwa kulipa malipo yaliyobaki mnada utarudiwa na fedha ulizo lipa hazitarudishwa
3. Gharama za kubadilisha umiliki ni za mnunuzi mwenyewe, kumbuka vigezo na masharti kuzingatiwa

**MAWASILIANO**
**WAUNGWANA AUCTION MART 0713077474**
**ADILI AUCTION MART 0716651103**
**KOTI BROTHERS 0713235517**

215689102


# Shahidi wa Zitto aanza kutoa ushahidi

**Na Hellen Mwango**

SHAHIDI Gerald Ibrahim (32), maarufu kama 'serikali' wa utetezi katika kesi ya uchochezi inayomkabili, Kiongozi wa chama cha ACT- Wazalendo Zitto Kabwe, amedai mahakamani alipewa kazi ya kurejesha amani na kutafuta silaha mbili za Jeshi la Polisi, alishuhudia miili ya watu kati ya 18 mpaka 20 waliokufa ikiwa msituni katika kijiji cha Mpeta, mkoani Kigoma.

Kadhalika, shahidi huyo amedai aliisaidia serikali kutuliza ghasia, kupata silaha mbili ikiwamo bunduki na bastola moja za Jeshi la Polisi, kupatikana na mwili wa Inspekta Ramadhani katika msitu wa Mwandubandu, mkoani humo.

Serikali alitoa madai hayo jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi, dhidi ya kesi ya uchochezi inayomkabili Mbunge wa Kigoma mjini, Zitto Kabwe.

Akiongozwa na Wakili wa Utetezi, Peter Kibatala, shahidi huyo wa sita akiongozwa na Kibatala, alidai mapigano baina ya Polisi na wananchi hao yalisababishwa na mgogoro wa ardhi. Alidai kuwa katika mapigano hayo alishuhudia watu wanne wakiwa wamekufa na alishiriki mazishi yao na kuongeza kuwa Oktoba 16, 2018, saa 10:00 alfajiri, alisikia bunduki zikirindima katika Kijiji cha Mpeta, Wilaya ya Uvinza, Kigoma na wananchi walikimbia na kutawanyika mahali tofauti.

Alidai kuwa tukio hilo lilileta maafa kwa watu mbalimbali na alishiriki mazishi ya watu wanne, huku wawili akiwa amewashuhudia majeraha yao ya risasi mmoja alipigwa ya mgongoni ikatokea mbele na mwingine alipigwa kwenye paja.

"Niliiona miili ya watu wawili waliouawa kwa kufumuliwa kwa risasi, lakini wengine nilihudhuria mazishi sikufanikiwa kuyaona majeraha yao kwa sababu nilikuwa wameshafunikwa sanda," alidai.

Pia, alidai kuwa madhara mengine yaliyosababishwa na Polisi katika mapigano hayo ni kuchoma nyumba moto iliyokuwa na watoto wawili ndani ambao walifariki.

Aliendelea kudai kuwa katika tukio hilo askari wawili walifariki na kuwataja kuwa ni Inspekta Ramadhani na Koplo Mudy, ambao walinyanganywa silaha zao.

Alidai kuwa Kamati ya Ulinzi na Usalama mkoa wa Kigoma ilifika Kijiji cha Mpeta na baada ya kikao wakafikia muafaka wa kutafuta upatikanaji wa miili ya askari hao na silaha walizonyanganywa kwenye tukio hilo la mauaji pamoja na kurudisha amani.

Shahidi huyo alidai kipindi cha msako cha kutafuta silaha hizo alifika katika kichaka kimoja akakuta watu 18 hadi 20 wamekufa na kwamba walifanikiwa kupata mwili wa Inspekta Ramadhani na bunduki mbili.

Alidai kuwa, aliteuliwa tena kumpeleka Naibu Waziri wa Uvuvi na Mifugo, Abdallah Ulega, kwenye eneo la tukio na kuongea na wananchi kuwa amepeleka salamu kutoka kwa Rais Magufuli na kuwataka watoke walikojificha na kurudi kwenye makazi yao kuendelea kufanya kazi na kuzaana.

Kadhali shahidi huyo alidai, baada ya kikao hicho, walirudi na yeye akapewa kazi ya kurudisha amani iliyopotea, kutawanya vikosi vya vurugu.

Katika kesi ya msingi, Zitto anadaiwa Oktoba 28, 2018 akiwa katika mkutano na waandishi wa habari, uliyofanyika katika Makao Mkuu ya ofisi ya Chama cha ACT- Wazalendo alitoa maneno ya uchochezi yenye kuleta hisia ya hofu na chuki.

# Wajasiriamali wanufaika mikopo TPB

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

BENKI ya Posta (TPB) tawi la Shinyanga, imetoa mikopo kwa wajasiriamali ya Sh. bilioni 3.9 kwa vikundi 330, ili wajishughulishe na biashara mbalimbali za kuwaingizia kipato na kuinuka kiuchumi.

Meneja wa benki hiyo, Jumanne Wagana, alisema hayo jana wakati akizungumza na Nipashe kuhusu changamoto wanazokabilia nazo katika urejeshaji wa mikopo kwenye vikundi ambavyo wanavikopesha, hasa kwenye kipindi hiki cha Janga la maambukizi ya virusi vya corona.

Alisema katika kipindi cha mwaka mmoja benki hiyo imekopesha vikundi 330, Sh. bilioni 3.9 na wajasiriamali wadogo wamekopesha vikundi 89, Sh. milioni 56, wakati vikundi 208, Sh. bilioni 1.2, pamoja na wakubwa vikundi 33, Sh. bilioni 2.6.

"Changamoto ambazo tunakumbana nazo kwa sasa ni urejeshaji wa mikopo umekuwa siyo mzuri, sababu ya janga hili la maambukizi ya virusi vya corona, biashara nyingi zimeyumba hasa zile zenye mikusanyiko ya watu zinakosa wateja, na kusababisha kupata mapato kidogo," alisema Wagana.

"Hali hii ya maambikizi ya virusi hivi vya corona ikiendelea kuwa mbaya, uongozi wetu ngazi ya juu umeshaanza kulifanyia kazi, na ikiwa tete kabisa itatoa utaratibu au kusitisha kabisa kuleta marejesho hadi hali itakapokuwa nzuri au kuondoa riba, kwa ujumla hali ya kiuchumi sasa hivi siyo nzuri kabisa," aliongeza.

Pia alisema mikopo hiyo wanaitoa kwa watumishi wa serikali na wazee wastaafu, na ndani ya miaka mitano wameshakopesha watumishi 409, Sh. bilioni 2.2, na marejesho yao hukatwa kwenye mishahara kila mwisho wa mwezi.

Alisema kwa kipindi hicho cha miaka mitano wameshakopesha wazee wastaafu 834 Sh. bilioni 4.3, na marejesho yao hukatwa kwenye pensheni na kutoa wito kwa wajasiriamali waendelee kuchapa kazi kama alivyosema Rais John Magufuli, huku wakichukua tahadhari ya kujikinga na virusi vya corona.

Mmoja wa wajasiriamali wadogo ambaye ni mnufaika na mikopo hiyo ya benki hiyo, Evarist Kabalo, alisema alianza kukopa tangu mwaka 2013, kwa sasa amejenga nyumba pamoja na kukuza mtaji wake wa ushonaji nguo, huku akibainisha kwa sasa biashara siyo nzuri sababu ya janga la virusi vya ugonjwa huo.



Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Brigedia Jenerali Nicodemus Mwangela, akipanda mti katika chanzo cha maji cha Ilolo, wilayani Mbozi, katika maadhimisho ya siku ya kitaifa ya upandaji miti ambapo kimkoa yamefanyika wilayani humo jana. **PICHA: MANUEL KAMINYOGE**

# Shule yaleta suluhisho kwa wanafunzi

**Na Elizabeth Zaya**

BAADA ya serikali kusimamisha masomo katika shule za msingi, sekondari na vyuo kwa ajili ya tahadhari ya tishio la ugonjwa wa corona, taasisi isiyo ya kiserikali ya Shule Direct, imeanzisha mpango wa kutoa nyenzo kwa ajili ya kujengea uwezo wazazi na walezi kuwasaidia watoto wao katika kipindi hiki.

Ofisa Mwendeshaji Mkuu wa taasisi hiyo, Mwanjisi, alisema kupitia majukwaa hayo ya shule Direct wazazi na walezi wanafursa ya kufuatilia maendeleo ya watoto wao kwa njia ya kidijitali.

"Pia kupitia majukwaa ya kidijiti ya Shule Direct, tunatoa mtaala wote wa elimu ya Sekondary kwa masomo 13 ya kidato cha kwanza hadi cha nne, mwanafunzi anaweza kujisomea hayo, kufanya maswali na mazoezi ya majaribio, pia anapata nafasi ya kupitia mitihani iliyopita ya Baraza la Mitihani la Taifa (Necta)," alisema Mwanjisi na kuongeza:

"Mwanafunzi ana fursa ya kufanya majadiliano na wanafunzi wenzake na pia kupata msaada wa mwalimu wa kidijitali wa Shule Direct anayepatikana kwa kutumia teknolojia ya Akili Bandia (Artificial Intelligence) na kupata nyenzo za kujifunza stadi za maisha, uongozi na ufahamu wa mambo ya fedha."

Mwanjisi alisema hivi karibuni taasisi hiyo iliingia makubaliano na shirika la Kimataifa linalohudumia Watoto (Unicef) upande wa Tanzania ili kusaidia upatikanaji wa huduma ya kujifunza kwa njia ujumbe mfupi wa maneno kupitia mpango maalum unaojulikana kama Makini SMS.

"Huduma ya Makini SMS inamwezesha mwanafunzi kujipima uelewa kwa kufanya maswali ya majaribio kwa kutumia simu yoyote ya kawaida. Huduma hii ambayo inapatikana bure kwenye mtandao wowote wa simu Tanzania, inampa mwanafunzi nafasi ya kufanya maswali ya majaribio katika masomo tisa ya kidato cha kwanza hadi cha nne, pia inampa nafasi ya kutafuta taarifa zaidi kupitia Wikipedia na Google kwa mfumo usiohitaji Internet," alisema Mwanjisi.

Aliongeza: "Shule Direct inahakikisha kuwa majukwaa yake ya kidijitali yanapatikana kutoa fursa kwa wanafunzi kujifunza kutoka kwa walimu takribani 40,000 waliojisajili kwenye jukwaa hili. Lengo ni kuhakikisha kuwa kila mtoto anapata nafasi ya kujifunza bila kujali jinsia yake, uwezo wake au mazingira yake. Tunafanya kazi na walimu wabobezi kutengeneza nyenzo za masomo ya Historia, Jiografia, Uraia, Kiingereza, Kiswahili, Fizikia, Kemia, Baiolojia, Hisabati, Biashara, na Tehama."

Mwanjili alisema tangu kuanzishwa kwa teknolojia hiyo mwaka 2013 mpaka kufika Machi mwaka huu ilikuwa imewafikia watumiaji 2,092,153 wakiwamo walimu 39,249 waliojisajili, watumiaji wa SMS zaidi ya 180,000 na shule za sekondari 90 zote za Tanzania ambazo zimewekewa mfumo maalum kutoka kwa taasisi hiyo.

# RC Malima aonya mzaha dhidi ya corona

**Na Sabato Kasika**

MKUU wa Mkoa wa Mara, Adam Malima, amewataka wakazi wa mkoa huo kutofanyia mzaha salamu za kugongeshana miguu, bali wazingatie maelekezo ya serikali ili kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona.

Alisema hayo alipokuwa akizungumzia jana kuhusu moja ya mikakati ya mkoa wake ya kukabiliana na maambukizi ya virusi hivyo, ambayo utoaji wa elimu kuanzia ngazi ya chini ili wananchi wajue namna ya kujikinga.

Alisema, moja ya silaha kubwa na muhimu ya kupambana na maambukizi ya ugonjwa huo ni utoaji wa elimu kwa umma ili wananchi wajue madhara yake na jinsi wanavyoweza kujikinga wasipate maambukizi.

"Bado kuna watu wanachukulia hizi salamu za kugongesha miguu kama fasheni au masihara, yote hayo yanatokana na ukosefu wa elimu kwa umma, hivyo ni jukumu letu kuhakikisha tunawafikia na kuwaelimisha kuhusu madhara ya ugonjwa huu na jinsi ya kujikinga, " alisema Malima.

Mkuu huyo wa mkoa alisema katika kufanikisha hilo, amewaagiza wakuu wa wilaya kuhakikisha elimu sahihi inatolewa kuanzia ngazi za vijiji ili kila mtu aipate na kujua jinsi kujikinga kuliko ilivyo sasa.

"Kwa sasa baadhi ya watu bado wanachukulia ugonjwa huo kama utani hali ambayo ni hatari, hivyo ni muhimu wote hao wafikiwe na kupewa elimu sahihi ya kuwawezesha kujikinga na virusi vya corona," alisema.

Alisema, serikali mkoani humo pamoja na mambo mengine imeweka elimu kama njia muhimu na sahihi ya kupambana na ugonjwa huo kwa vile elimu ikitolewa vizuri kila mmoja ataelewa na kuwa mstari wa mbele kujikinga na kuwakinga wengine ili kuepuka maambukizi.



Naibu Spika Dk. Tulia Ackson, akipokea tuzo maalum ya kuthamini mchango wake katika kupambana na Ukimwi na Kifua kikuu nchini iliyotolewa na Chama cha Watu wanaoishi na Virusi vya Ukimwi nchini (NACOPHA) na kukabidhiwa kwake na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya masuala ya Ukimwi, Oscar Mukasa, jijini Dodoma jana. **PICHA: BUNGE**

# Wakulima mboga walalamikia maji yasiyo salama kumwagilia

MBUNGE wa Viti Maalum (CUF), Zainab Mndolwa Amiri, amesema wakulima wengi wa mboga hasa jijini Dar es Salaam, wanatumia maji yasiyo salama kwa ajili ya kumwagilia.

Akiuliza swali bungeni jana, Mbunge huyo alisema huenda maji hayo yanayotumika yana kemikali ambazo zinaweza kudhuru afya za wananchi badala ya kuziimarisha.

"Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia maji safi na salama wakulima hao wa mbogamboga?" alihoji.

Katika majibu yaliyotolewa na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, wakulima wengi wa mboga hizo waliopo Jiji la Dar es Salaam hutegemea bonde la Mto Msimbazi.

Hata hivyo, Ofisi hiyo ilisema Mto Msimbazi unakabiliwa na tatizo la uharibifu wa mazingira unaosababishwa na shughuli za kiuchumi na kijamii ikiwamo kilimo hicho kando ya mto huo. Aidha, ilisema Serikali kwa kushirikiana na wadau imeendelea kutoa elimu kuhusu hifadhi ya vyanzo vya maji na kutekeleza mipango na shughuli mbalimbali kwa ajili ya kulinda mazingira ya mto huo yasiharibiwe.

Pia, ilisema Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeandaa mradi wa kuboresha bonde la Mto Msimbazi ili kukabiliana na tatizo la uharibifu wa mazingira katika mto huo.

"Mradi huu unalenga kupunguza athari za mafuriko, kudhibiti mmonyoko wa udongo unaosababishwa na shughuli za binadamu kando ya mto huo, kujenga uwezo wa jamii inayozunguka mto msimbazi kuendelea na shughuli za kiuchumi pasipo kuathiri mto," Ilisema.

Kadhalika, ilisema kupanda miti kwa ajili ya hifadhi ya mazingira ya mto, kuweka mkakati wa udhibiti wa taka ngumu katika mazingira ya Mto Msimbazi na kujenga mazingira wezeshi kwa wajasiriamali wadogo kuendeleza shughuli zao bila kuathiri mazingira ya mto huo.

"Kwa kuboresha mazingira ya bonde la mto msimbazi, tunategemea kwamba uchafuzi wa mazingira katika mto huo utapungua," alisema.

Vile vile, Ofisi hiyo ilisema Kifungu cha 57 cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 kinazuia shughuli za kudumu na ambazo kwa asili yake inaweza kuhatarisha au kuathiri vibaya utunzaji wa bahari au kingo za mto na mabwawa katika eneo la hifadhi mita 60 kutoka vyanzo vya maji.

"Aidha, Sheria hii inampa mamlaka Waziri mwenye dhamana ya usimamizi wa mazingira kuandaa mwongozo wa matumizi endelevu wa eneo hilo," ilisema.

Ilibainisha kuwa imeandaa rasimu ya Mwongozo wa mita 60 wa kuhifadhi vyanzo vya maji na inaainisha matumizi endelevu ya eneo la mita 60 kutoka vyanzo vya maji ikiwamo shughuli za kilimo kando na vyanzo vya maji. Katika hatua nyingine, Ofisi hiyo imesema chanzo cha uchafuzi wa Mto Kanoni ni kuwapo kwa shughuli za kibinadamu pembezoni na ndani ya mto.

Majibu hayo yalitolewa na Mbunge wa Viti Maalum, Bernadetha Mushashu (CCM), ambaye alisema Mafuriko yanayotokea katika Mji wa Bukoba husababisha uharibifu mkubwa wa chakula, mali, barabara na hata kusababisha vifo kwa watu na mifugo, mafuriko hayo husababishwa na Mto Kanoni kujaa mchanga na takataka.

Ofisi hiyo ikitoa majibu ya swali hilo, Ilisema Halmashauri ya Manispaa ya Mji wa Bukoba imeanza kuchukua hatua za muda mfupi kwa kupiga marufuku na kuondoa shughuli zote za kibinadamu zinazofanyika ndani ya mto kama zilivyobainishwa hapo juu, pamoja na kuhakikisha eneo la hifadhi ya mto kisheria linasafishwa.

## TCRA kukagua ubora wa huduma

IMEELEZWA kuwa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) itafanya ukaguzi wa ubora wa huduma za mawasiliano kwa kushirikiana na watoa huduma kulingana na viwango vya ubora.

Lengo ni kuhakikisha wananchi wanapata mawasiliano ya uhakika kwa maeneo yenye usikivu hafifu.

Hayo yalielezwa kwenye majibu ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, katika swali la Mbunge wa Sikonge (CCM), Joseph Kakunda, ambaye alihoji kuhusu hitaji la mawasiliano ya simu ya uhakika katika eneo hilo.

Katika swali lake, Kakunda alisema baadhi ya minara ya simu ya Vodacom, Airtel, Tigo na Halotel katika Kata za Kipili, Kilumbi, Kiloli, Kitunda, Kisanga, Mole, Kiloleli na Ipole haifanyi kazi vizuri kwani mtandao katika Kata hizo ni mdogo sana na hivyo wananchi hawapati huduma nzuri ya Mawasiliano licha ya uwepo wa minara hiyo.

Aidha, katika Kata za Nyahua, Igigwa na Ngonjwa hakuna kabisa mawasiliano ya simu na kuhoji ni lini Serikali itawapatia mawasiliano ya uhakika wakazi wa Sikonge wanaoishi kwenye kata zenye minara ya simu lakini isiyokamata mtandao vizuri.

"Je, Serikali itawapatia lini mawasiliano ya simu wananchi wa Sikonge ambao wanaishi kwenye kata ambazo hazina kabisa minara ya mawasiliano ya simu?"alihoji.

Wizara hiyo ikitoa majibu kwa maswali hayo, Ilisema Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote imetoa ruzuku kwa ajili ya ujenzi wa minara ya mawasiliano katika Wilaya ya Sikonge katika kata za Kiloli, Igigwa, Kipanga, Kipili na Kitunda kwa kushirikiana na TTCL na VODACOM kupitia miradi ya mawasiliano ya awamu ya kwanza na awamu ya tatu.

Ilisema katika Kata ya Igigwa, Serikali kupitia Mfuko huo ilitangaza zabuni na kupata mtoa huduma TTCL ambaye ameanza maandalizi ya ujenzi wa mnara katika kata hiyo.

Kwa upande wa kata za Nyahua na Ngonjwa, ilisema kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote itazijumuisha kata hizi katika mradi wa Mawasiliano vijijini awamu ya tano ndani ya mwaka wa fedha 2020/21.

# Mto Kalambo sasa kuwa wa utalii

SERIKALI imesema ili kuboresha mazingira ya utalii katika eneo la maporomoko ya Mto Kalambo itahamasisha sekta binafsi ili zijengwe nyumba za kulala wageni, kumbi za mikutano na eneo la kuhifadhi wanyamapori hai (zoo).

Majibu hayo yalitolewa bungeni na Wizara ya Maliasili na Utalii katika swali la Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Aida Khenan, ambaye alihoji Serikali ina mpango gani wa kupeleka fedha kwenye kivutio cha maporomoko hayo.

Katika majibu ya Wizara hiyo, ilisema maporomoko ya Mto Kalambo yapo katika Msitu wa Hifadhi ya Mazingira Asilia Kalambo yenye ukubwa wa hekta 41,958.

Ilieleza Hifadhi hiyo ni muunganiko wa misitu miwili, Msitu wa Mto Kalambo na Msitu wa Hifadhi wa Maporomoko ya Mto Kalambo.

"Kutokana na kuwapo kwa maporomoko hayo, eneo hili lina bioanuai nyingi na kwa kuzingatia umuhimu wa eneo hilo, mwaka 2019, Serikali ilipandisha hadhi Msitu huo kwa Tangazo Na. 127 kuwa Msitu wa Mazingira Asilia,"ilisema.

Wizara kupitia Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), mwaka 2016 ilianza kuboresha miundombinu katika maporomoko ya Kalambo ili kuwezesha watalii kuvifikia kivutio husika kwa urahisi.

Ilisema ni pamoja na kujenga ofisi sita, kutengeneza njia za kutembelea wageni (walk trail) na kujenga ngazi katika maporomoko ya Mto Kalambo ambapo hadi sasa takribani ngazi zenye urefu wa mita 450 zimekamilika.

Aidha, ilisema kazi ya ujenzi ilianza mwaka 2018 ambayo inahusisha ujenzi wa jengo la ofisi, ngazi zenye urefu wa mita 514, vyoo na geti inayofanywa na kampuni iitwayo Green Construction Limited inaendelea kufanyika katika maporomoko hayo.

"Kazi hii inatarajiwa kukamilika ndani ya mwaka huu wa




**Habari zote na Augusta Njoji,** DODOMA

# Wadau wa madini watakiwa kuchangamkia fursa tanzanite

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

WADAU wa madini ya Tanzanite wa Mji Mdogo wa Mirerani wilayani Simanjiro mkoani Manyara, wametakiwa kuchangamkia fursa ya madini hayo, kwa kuwa serikali imeondoa kodi zilizokuwa zikilalamikiwa.

Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Zephania Chaula, aliyasema hayo wakati akizindua soko na mnada wa madini ndani ya ukuta unaozunguka migodi ya madini ya tanzanite.

Chaula alisema baada ya wadau wa madini kulalamikia kodi ya asilimia tano ya zuio na asilimia 18 ya ongezeko la thamani, wadau wachangamkie fursa hiyo kwa kuwa serikali imeondoa kodi hizo.

Alisema serikali ina mpango sekta ya madini iwe miongoni mwa sekta zinazochangia kwa wingi pato la taifa.

"Changamkieni fursa hizi kwa kuuza na kununua madini kwa kuwa na soko hapa Mirerani na Orkesumet, na soko lingine litafunguliwa hivi karibuni," alisema Chaula.

Mwenyekiti wa Chama cha Wanunuzi wa Madini Tanzania (Tamida), Sam Mollel, aliishukuru tozo hizo kutolewa kwa kuwa zimekuwa tatizo kwa wadau wa madini.

Mollel alisema hali hiyo imehamasisha wachimbaji wadogo kuuza madini kwenye masoko ya madini kwa kuwa wana imani kuwa kodi zilizokuwa na usumbufu kwa wadau wa madini zimeondolewa na Rais John Magufuli.

Katibu wa Chama cha Wachimbaji Madini Mkoa wa Manyara, (Marema), Tariq Kibwe, alisema wadau wa madini wanaendelea kupewa elimu ya ulipaji kodi .

Mdau wa madini ya tanzanite, Shifonya Solomon, alisema ukuta unaozunguka migodi ya madini ya tanzanite umekuwa na manufaa kwao.

Dalali wa madini, Elisha Laizer, alisema uwapo wa masoko ya madini ya vito ni nafuu kwao kwa kuwa watapambana na matatizo mbalimbali yanayowakabili, ikiwamo bei ya tanzanite.

Salome Mnyawi, muuzaji wa magonga ya tanzanite, alisema baadhi ya wanawake wa eneo hilo watachangamkia soko hilo kupitia umoja wao.

Mkoa wa kimadini wa Simanjiro una madini mbalimbali ikiwamo tanzanite, ruby, green tomarine, green gainet, ross, rafite umezindua masoko mawili ya Orkesumet na Mirerani.




Mkurugenzi wa kampuni ya Ngoma Auto spare ya Mji mdogo wa Mirerani, Wilayani Simanjiro, Khalifa Ngoma (wapili kulia), akimkabidhi kadi ya pikipiki Athanas Joseph, baada ya kushinda bahati nasibu aliponunua pikipiki kwenye duka hilo juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# NHIF yajipanga kufikisha huduma kwa wananchi

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

MFUKO wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) Mkoa wa Manyara, umeandaa mpango maalumu wa kuwafikia wananchi na makundi mbalimbali ili kurahisisha upatikanaji wa huduma za afya.

Hayo yalisemwa mjini Babati na Meneja wa NHIF mkoani Manyara, Hance Mwankenja, wakati wa hafla ya ugawaji wa kadi za bima ya afya kwa wananchi.

Mwankenja alisema ili makundi hayo, yasajiliwe kwenye mfuko huo, wahusika wanatakiwa kuwa kwenye vikundi na siyo mtu mmoja.

Alisema endapo wananchi watajiunga katika vikundi, itawapunguzia gharama ya kupata matibabu.

Hata hivyo, mfuko huo una mpango maalumu wa kuwafikia wananchi mbalimbali hususani madereva.

Alisema huduma ya kukata bima ya afya ya mfuko huo ni Sh. 100,000 kwa mtu mmoja.

"Tutaanza na madereva na baadaye tutakwenda kwa mama lishe na waandishi wa habari," alisema Mwankenja.

Aidha, alisema wanapaswa kujisajili hata kupitia katika vyama vya ushirika ili kuwarahisishia upatikanaji wa matibabu.

Aliwataka wananchi wasisubiri kupata maradhi ndio wakate bima za afya, badala yake wakate mapema ili wawe na uhakika wa matibabu wakati wakiendelea na shughuli za uzalihaji mali.

Mkazi wa Babati, Revocatus Festo, alisema kuna umuhimu kwa wananchi kukata bima za afya na kuwashauri wataalamu kutoa elimu bila kuchoka.

Mkazi wa Daghailoy, John Zacharia, alisema wananchi wanapenda kuwa na bima ya afya, lakini hawana uwezo wa kulipia kutokana na gharama kuwa kubwa.

Renatha Daudi alishauri

# Arumeru yapitisha bajeti bil. 55.4/-

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WAJUMBE wa Baraza la Madiwani Halmashauri ya Arusha wilayani Arumeru, wamepitisha rasimu ya mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/21.

Mpango huo una makadirio ya mapato na matumizi ya Sh. bilioni 55.4, na ulipitishwa wakati wa mkutano maalum wa baraza la madiwani.

Akiwasilisha rasimu hiyo, kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Mchumi Albert Mahoo, alisema kwa mwaka wa fedha 2020/21, halmashauri hiyo imepanga kukusanya na kutumia kiasi hicho cha fedha kutokana na ukomo wa bajeti uliotolewa na ofisi ya hazina.

Mchanganuo wa mpango wa bajeti ya Sh. bilioni 55.4, ni Sh. bilioni 4.9 kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na asilimia 8.86, Sh. bilioni 8.9 kutekeleza miradi ya maendeleo sawa na asilimia 16.8 na Sh. bilioni 41.6 ikiwa ruzuku ya kulipa mishahara ya watumishi sawa na asilimia 75.06.

Katika kutekeleza miradi ya maendeleo, halmashauri hiyo itatumia mapato ya ndani Sh. milioni 832.5 na Sh. bilioni 3.5, ambazo ni za ruzuku kutoka Serikali Kuu pamoja na Sh. bilioni 4.5 kutoka kwa wadau mbalimbali wa maendeleo.

Halmashauri hiyo imepanga kushirikiana na wananchi katika utekelezaji wa majukumu ya msingi ili kufikia malengo ya dira ya taifa ya kutoa huduma bora kwa wananchi na kuondoa umaskini.

Vipaumbele vya halmashauri hiyo kwa mwaka wa fedha 2020/21, ni uwekezaji katika sekta ya elimu, kilimo na umwagiliaji, Mifugo na uvuvi, afya, ardhi, mipango miji, maliasili, fedha na biashara, rasilimali watu na utawala, tehama na maeneo mtambuka.

Hata hivyo, wajumbe wa baraza hilo, licha ya kupitisha mpango wa bajeti hiyo, walisema kama bajeti hiyo itatekelezwa kwa ufanisi, itakuwa na mafanikio makubwa, kwa kuwa imepanga kutekeleza miradi inayowagusa wananchi moja kwa moja.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya hiyo, Baraka Simon, alisema mpango huo, utatekelezwa kwa ufanisi, lakini ameitaka halmashauri kubuni miradi ya kimkakati, ambayo itatekelezwa na itailetea halmashauri mapato na kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa bajeti hiyo.

Diwani wa Viti Maalum, Jasmin Bachu, aliishauri Halmashauri kufanya tathmini ya wafanyabiashara ambao siyo waaminifu wenye vitambulisho vya wajasiriamali kwa kuwa wanaikosesha mapato halmashauri.





# Wataalamu wanyooshewa kidole migogoro ardhi

**Na Mary Mosha,** SAME

SERIKALI mkoani wa Kilimanjaro imesema migogoro kati ya wakulima na wafugaji inachangiwa na baadhi ya wataalamu wa ardhi kushindwa kuweka na kusimamia mgawanyo sahihi wa matumizi bora ya ardhi.

Akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Marwa, Wilaya ya Same, Mkuu wa Mkoa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, alisema kwamba serikali haitasita kuwachukulia hatua wataalamu katika idara mbali mbali ikiwamo ya ardhi ikiwa watashindwa kuwa chachu ya kumaliza migogoro ya wakulima na wafugaji.

Alisema katika halmashauri wapo baadhi ya wataalamu ambao sio waaminifu wamekuwa chanzo cha migogoro kutokana na kushindwa kuweka matumizi bora ya ardhi pamoja na kutoa elimu kwa wakulima ya madhara hayo ili kuepusha migogoro isiyo ya lazima.

"Baada ya kuongea na kuwasikiliza wakulima na wafugaji tumebaini kuwa wapo baadhi ya wataalamu wetu ambao ni chanzo cha migogoro kutokana na kushindwa kusimamia sheria na taratibu zilizowekwa pamoja na kupokea rushwa ili kupindisha ukweli hasa wanapofika vijijini," alisema.

"Nawaagiza watendaji wote katika halmashauri zote mkoani hapa kuhakikisha wanalitazama suala la wakulima na wafugaji katika kuweka sawa matumizi bora ya kwa ardhi wakionyesha eneo la malisho na la wakulima ili kupunguza migogoro," alisema.

Katika hatua nyingine Dk. Mghwira aliwataka viongozi wa vitongoji na vijiji, kuainisha njia kwaajili ya mifugo pamoja na kuchimba mabwawa ambayo yatatumika kwa ajili ya majosho ya mifugo.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Same, Majid Kabyemela, ambaye ni Ofisa kilimo na mifugo wilayani humo, alisema halmashauri hiyo imetenga kiasi cha Sh. milioni 25 kwaajili ya kufanya mipango ya matumizi bora ya ardhi katika vijiji vinne vya Kata ya Ruvu.

Alisema migogoro kati ya wakulima na wafugaji inachangiwa kwa kiasi kikubwa na uwepo wa mifugo mingi katika eneo hilo, na kwamba kata ya Ruvu pekee inaongoza kwa kuwa na mifugo mingi katika Wilaya ya Same.

Kwa upande wake katibu wa Baraza la Usuluhishi migogoro ya ardhi Kata ya Ruvu Nangala, Koole Mollel, alisema kutokuwapo kwa maeneo yaliyotengwa kwaajili ya wafugaji inasababisha migogoro hiyo kuwapo.

"Watendaji wamekuwa wakifika kwenye maeneo haya bila kuleta suluhu la kudumu kwa kuwa wamekuwa wakitoa majibu ya serikali imelichukuwa, lakini ukweli ni kwamba hakuna matumizi sahihi ya ardhi katika eneo hili hivyo tunaomba mpango huo usimamiwe ili kutokomeza migogoro kati ya pande hizo mbili.

# Sabaya atoa siku 14 kujengwa uzio

**Na Godfrey Mushi,** HAI

KUCHELEWA kuanza kwa mradi wa ujenzi wa uzio wa eneo la uwekezaji la Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco), lililopo katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Hai mkoani Kilimanjaro, umemkasirisha Mkuu wa wilaya hiyo, Lengai Ole Sabaya.

Ameagiza ujenzi huo uwe umeanza kutekelezwa baada ya siku 14 kuanzia sasa ili kuzuia wavamizi kuliingilia tena eneo hilo ambalo awali lilikuwa likimilikiwa isivyo halali na mmoja wa wafanyabiashara, kwa madai kuwa ni mali yake.

Ole Sabaya alieleza jana kushangazwa na Shirika hilo kushindwa kutekeleza mradi huo tangu mwezi Januari mwaka huu, licha ya serikali kuipatia kiasi cha Sh. milioni 50.

"Hili neno mchakato unaendelea, unafanyika, mara tunafuatilia, linakwamisha kasi ya serikali kutekeleza miradi yake, ni mlolongo usio na matokeo chanya. Kukaa na fedha za umma miezi miwili, halafu hamzifanyii chochote kwenye eneo la serikali maana yake ninyi mnakaribisha wavamizi waje kwenye maeneo haya.

"Utaratibu wa kupata mchoro unachukua siku ngapi? Kwa hiyo mnazo pesa kwenye akaunti, halafu hamzifanyii chochote kwenye eneo la serikali maana yake ninyi mnakaribisha wavamizi waje kwenye maeneo haya kwa kutofanya jambo lolote."

Akijibu maswali hayo, Ofisa Rasilimali Watu wa Tanesco Mkoa wa Kilimanjaro, George Severine, alisema kulingana na utaratibu, wanawatumia watu wao wa makao makuu kutengeneza michoro ya majengo ili kukidhi vigezo vya majengo ya serikali.

Desemba 2, mwaka jana, Mkuu huyo wa wilaya aliamuru kukamatwa na kuhojiwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), mfanyabiashara mmoja baada ya kudaiwa kujimilikisha isivyo halali eneo la Tanesco kwa kipindi cha miaka 35.

Wakati mfanyabiashara huyo akiwa anamiliki kiwanja hicho kilichopo eneo la Bomang'ombe, Tanesco ilikuwa inalipa kodi ya pango la ardhi kwa kipindi chote iliyofikia Sh. milioni 20.



Mkuu wa Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya (katikati), akikagua mashimo makubwa yaliyochimbika katika barabara ya kuingia Kituo cha mabasi cha Bomang'ombe jana, kabla hajaifuta zabuni ya ukarabati wake iliyotangazwa na Halmashauri ya wilaya hiyo. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Wahoji fedha zao kutowasilishwa NSSF

**Na Mary Mosha,** SIHA

CHAMA cha wafanyakazi wa mashambani na kilimo Tanzania (TPAWU), kimeiomba serikali kuingilia kati tatizo la kukatwa fedha na waajiri wao za Shirika la hifadhi ya jamii (NSSF), ambazo haziwasilishwi kwa wakati kwenye mifuko hiyo.

Akizungumza kwa niaba ya wafanyakazi wenzake kwenye mkutano mkuu wa kamati ya utendaji kanda ya Kilimanjaro, Mwenyekiti wa TPAWU, tawi la Relongo Estate lililoko wilaya ya Siha, Rashid Mswaki, alisema waajiri hao wanawakata fedha hizo kwaajili ya mifuko mbalimbali ya kijamii ikiwamo NSSF, ilhal waajiri wao hawaziwasilishi fedha hizo kwa wakati.

"Sisi wafanyakazi wa mashambani na kilimo, tumekuwa tukikatwa fedha za mifuko mbalimbali ya kijamii kama NSSF na waajiri wetu, lakini wao (waajiri), hawawasilishi michango hiyo kwa wakati jambo ambalo limetujengea usumbufu mkubwa," alisema Mswaki.

Mswaki aliiomba serikali na uongozi wa TPAWU, iwasaidie kutatua tatizo hilo ambalo limegeuka kuwa mwiba kwa ustawi wa kiuchumi kwa kazi zao na familia zao pia.

Elius Mashmba, Mwenyekiti wa TPAWU, tawi la TPC alisema changamoto kubwa iliyoko kwa wafanyakazi wakati wanapoumwa wakienda kutibiwa hospitalini hawapati huduma hiyo kutokana na fedha wanazokatwa kutokuwasilishwa na waajiri wao.

"NSSF ni wadau wakubwa kwa wafanyakazi wa mashambani, wanapata mapato mengi kupitia kwa wafanyakazi hawa, mfanyakazi anapokuwa anaumwa anastahili na yeye apate fao la matibabu, miongoni mwa mafao wanayotoa NSSF ni pamoja na fao la matibabu, lakini mfanyakazi anapoenda kupata huduma hiyo ambayo ni stahili yake anaambiwa mchango haujatosha kwa kweli inakatisha tamaa,"alisema Mashamba.



Ukurasa 14

Asimulia safari iliyoanzia shule ya walimu wawili mume, mke



Ukurasa 15

TRC inavyokabili janga kuu la corona



Ukurasa 18

## MIKOPO SH.MIL 301 Halmashauri Shinyanga 'zajibu' kuelekezea kinamama na vijana


# BUFE

IJUMAA APRILI 3, 2020

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA




### MWALIMU, MJASIRIAMALI...

# Mtotoa vifaranga anayesimamia siri mafanikio, nyenzo nishati jua

**Na Beatrice Shayo**

"KUKU anapokuwa katika hali ya kutamia, huwa ninamchukua na kumloweka katika maji kati ya dakika 20 hadi 30 na kumtoa, halafu kesho yake namuweka tena katika maji. Lengo ni kumuondolea lile joto la kutamia na kumfanya asiwe na mawazo hayo na kuanza kutaga," anatamka Mama Rehema Kabuti.

Huyo ni mjasiriamali wa kutotolesha vifaranga vya kuku kwa kutumia umeme wa jua pamoja na gesi, ikiwa njia ya kuhudumia kuku anaowafuga kwa ajili ya kumpatia mayai ya kutotoa.Rehema anasema, pindi wanapotaka kutamia mayai, inamlazimu kuwaloweka katika maji waendelee kutaga na anasema huwa anatotolesha vifaranga, ili kuku wake waendelee na utagaji.

Anarejea mchakato kuwa anaanza na joto la kutaka kutamia na kisha anaomuondoa kuku na kumuweka katika maji.


INAENDELEA UK.16


UCHUMI

## Habari katika picha



Ukurasa 17

## Mustakabali wa kuambukizana corona na kitendawili umaskini


Ukurasa 20

BIASHARA

UBOSI WA MASELE WA NYANZA...

# Asimulia safari iliyoanzia shule ya walimu wawili mume, mke

• Ugomvi nyumbani, mke anasusa • Umbali Km.5, akichelewa viboko • Safari shule na maziwa ya walimu • Makazi ya darasa 5 alilipia 'jembe' • Matunda; mtaalamu kitaifa, bosi mkuu Ushirika



Jengo la mashine kongwe ya kuchakata pamba, lililopo Magu, ambako ni maeneo alikoanzia kazi Mzee Masele, takriban miaka 60 iliyopita. **PICHA: MAKTABA**

**Na Anthony Gervas,** MWANZA

KUNA usemi maisha ni safari ndefu. Unapomuona mtu katika wajihi wa leo, si ajabu alikotoka ana simulizi na mzizi wa kufikia sasa, una muonekano tofauti sana.

Ni kawaida, kila binadamu ana simulizi yenye safari ndefu na iliyojaa historia ya kipekee, tangu ujana hadi uzee wake, ikiwa atabahatika kufikia umri huo; kuna magumu, milima na mabonde, yanayobeba ama ya kufurahi au kusikitisha na kushangaza zaidi.

Hapo ndipo Mzee Enock Masele, jina kubwa na gwiji katika fani ya ushirika nchini, na hususan, Nyanza Mkoa wa Mwanza. Kama alivyowahi kuhojiwa na Nipashe na makala yake kuchapishwa, hapana shaka ni mtu wa kumuuliza chochote katika ushirika huo atakujibu.

Leo hii akiwa na umri wa miaka 78, mtanashati ana mantinki ya jibu lolote utakalomuuliza, mara moja inatoa jibu kwa mantiki 'shule ipo' tena kwa msingi imara tangu darasa la kwanza. Naam! Hapo ndipo kuna mzizi mkuu wa kilichojificha.

> **"Hata mumewe alikuwa hawezi kumuamuru afundishe, kwa sababu anakuwa bado ana hasira za ugomvi wake na mumewe.**

Unaweza kuamini, alishasoma katika shule iliyo umbali wa kilomita tano kutoka nyumbani kwao, ikiwa na walimu wawili tu, mke na mume? Unajua kila safari ya shule alikuwa anaharakisha mwendo kwa staili ya 'mbio mbio' awahi kuepuka viboko vya uchelewaji, mkononi ana zawadi ambayo kila siku ni lazima amfikishie mwalimu mkuu?

Hiyo ni jambo moja. Pale aliopofaulu na kuhamia kwingineko mbali zaidi nako kuna simulizi yake. Kwa kifupi, huko alipata hifadhi ya makazi alikolipia huduma hiyo kwa kulimishwa shamba.

Hizo ndizo dondoo, zenye simulizi zinazoanzia miaka 70 iliyopita, leo hii zimemuibua bingwa huyo msomi na gwiji wa sekta ushirika.

Ni wasifu unaoheshimika, hata Rais Dk. John Magufuli, aliyewahi kutumika naye Ushirika Nyanza, alimpatia jukumu la kitaifa, kusaidia kuongoza tume maalum 'iliyofukua' mali za Ushirika Nyanza kwa mafanikio makubwa. Sasa mfuatilie kwa hatua.

**ALIKOTOKA**

Gazeti la Nipashe katika kudodosa ukweli huo, iliandaa safari na kuwa na faragha na mzaliwa huyo wilatani Magu, ambaye sasa ni mkazi mkongwe wa jijini hapa kujua nini 'kilimkokotoa' hadi akawa jina kubwa katika ushirika, leo amestaafu lakini bado amekuwa wa kuhitajika.

Ni mazumgumzo ambayo yalijibu mtazazmo toka tamathali kuwepo 'milima na mabonde' katika mifumo ya maisha ya mwanadamu, hadi kumuumba leo kuwa Meneja Mkuu Mstaafu. Hapo msamiati mkuu umejificha katika dhana; kusaka fursa ya elimu na taaluma.'

Mzee Masele, anaanza simulizi yake, alizaliwa katika familia ya kifugaji kijijini Nyamatala wilayani Magu, Mwanza mwaka 1942, akimtaja baba yake Mzee Yaled Masele, aliyekuwa Mchungaji wa kanisa linaloitwa African Inland Church (AICT)

Anasimulia safari ya masomo, alianza mwaka 1949 akiwa na miaka saba. Hiyo ilikuwa katika shule kanisa la AICT, kijijini Magu na baadaye alihamia shule ya msingi anayoitaja ya Kitongo, alikosoma darasa la pili hadi la nne alikohitimu mwaka 1952.

Maisha mapya ya kuhamia shule ya Kitongo iliyoko umbali wa kilomita tano kutoka nyumbani kwao, ndiko alikoanza kuona maisha mapya na ya kipekee kitaaluma, iliyoambatana na 'joto ya jiwe' masomoni.

Anasema, shule hiyo iliyokuwa na walimu wawili tu, ambao ni mume na mke, ikiwa ni historia inatinga miaka 70 sasa, Mzee Masele anawataja kuwa Mwalimu Mkuu, Sylvester Ngoyeji, aliyefundisha darasa la tatu na nne na mkewe ambaye pia ndiye Mwalimu Mkuu Msaidizi, Rodofica Bugumba, alifundisha madarasa ya kwanza na la pili.

Kwa mujibu wa Mzee Masele, wanandoa hao wawili walifanikisha kufundisha kwa ufanisi na daima hajawahi kushuhudia pengo la kitaluma.

Pia, anajisifu daima hakukata tamaa masomoni, kwani licha safari ndefu kutembea jumla ya kilimita 10 kila siku, kwenda shule na kurudi nyumbani, daima hakukata tamaa ya masomo.

Mzee Masele anaendelea kusimulia:"Pamoja na yote, sitasahau walimu hao, kwanl siku wakiwa wamegombana nyumbani mke na mume, mwalimu Rodifica (mke) akija shuleni anakataa kufundisha darasani.

"Hata mumewe alikuwa hawezi kumuamuru afundishe, kwa sababu anakuwa bado ana hasira za ugomvi wake na mumewe."

Kingine kinachobaki kumbukumbu, anasimulia safari zake zilivyokuwa sehemu ya ratiba binafsi, kwamba kabla ya kuondoka nyumbani Buhi, alilazimika akamue maziwa ya ng'ombe kuwapelekea walimu waliomlipa baba yake fedha kidogo kila mwezi, kujikimu na maisha ya kifamilia.

"Pamoja na kuwapelekea maziwa, lakini nikichelewa wananichapa viboko viwili vya uchelewaji, wakati wa kuingia darasani. Hivyo, nilizoea adhabu hiyo," anasimulia na anaendelea:

"Sikuweza kuchukia, kwa sababu wakati huo ndivyo ulivyokuwa wa utii. Maadili na nidhamu shuleni na nyumbani kwa wazazi.'

Mzee Masele, ambaye leo ni mtu mzima anayetembea kwa hatua za mahesabu, anakumbuka wakati huo mwendo wa asubuhi kuwahi shule ulitawaliwa na mchakamchaka, ili awahi masomo na kuk-



Mzee Enock Masele, akiwa katika ofisi yake binafsi, jijini Mwanza. **PICHA: ANTHONY GERVAS.**

wepa viboko.

Pia, anaeleza ratiba yake siku ya mapumziko, ambazo ni Jumamosi na Jumapili ambayo baba yake alihuburi kanisani, alikuwa na jukumu la kulima na kuchunga ng'ombe.

Ni aina ya majukumu ambayo Mzee Masele, anakumbuka yalitawala likizo zake za masomo, akisema ni tofauti sana na ratiba za wasomi wa sasa walio huru zaidi.

**MASOMONI UKEREWE**

Anasema baada ya kumaliza darasa la nne, hakubahatika kufaulu. Hata hivyo, mwaka 1955 katika zama harakati za siasa za chama cha TANU zilikuwa zimeanza, alibahatika kupata nafasi ya kujinga darasa la tano na sita, katika shule iliyomilikiwa na kanisa la AICT, wilayani Ukerewe.

"Niliendelea kusoma Shule ya Middle School (Shule ya Kati) Kazirankanda darasa la saba na nane wilayani, humo hadi kuhitimu darasa la nane, wakati huo nikiwa natokea nyumbani Magu kwenda Ukerewe shuleni, nilikuwa napitia mjini Mwanza kupitia Ziwa Victoria kwa kutumia kivuko cha Mv. Tilapia hadi Ukerewe," anasimulia Masele.

Anaeleza akiwa Ukerewe, aliishi katika makazi ya mtu huko Ukerewe, anayemtambulisha hakuwa ndugu yake na alikuwa na utaratibu, kila shule inapofungwa, aliyepewa jukumu la kulima kwa wiki moja katika shamba la familia hiyo na kisha walimruhusu kwenda likizo nyumbani.

**AJIRIWA USHIRIKA**

Mzee Masele anasimulia, baada ya kuhitimu masomo ya darasa la nane, mwaka 1960 ukiwa ni mwaka mmoja kabla ya uhuru wa Tanganyika, alipata ajira katika kiwanda cha kuchambua pamba Magu (ginnery).

Hicho kilikuwa, chini ya Muungano wa Chama cha Ushirika cha Wakulima wa Pamba Kanda ya Ziwa (Victoria Federation Cooperative Unions Limitd -V.F.C.U), ambako Masele akitumika katika nafasi ya Kalani wa Kupima Pamba ya Wakulima kutoka katika vyama vya msingi, hadi mwaka 1964.

Anasema alipoendelea na utumishi ndani ya chama cha ushirika, baadaye alijiendeleza kimasomo hadi alipohitimu katika kilichokuwa Chuo cha Ushirika Moshi (sasa chuo kikuu), akitunukiwa stashahada mwaka 1973.

Masele anasema, baada ya hapo aliendelea kutumikia ushirika huo, uliopitia mabadiliko na kuundwa Ushirika wa Nyanza, alistaafu mwaka 1999, akiwa katika nafasi ya Meneja Mkuu.

Mzee huyo anahitimisha simulizi yake kwamba, baada ya kustaafu amejiajiri jijini Mwanza, kwa biashara ndogo zinazokimu mahitaji yake ya kila siku, huku hajatupia kisogo ushirika, kwamba amefungua mlango kuwashauri wanaushirika au kutoa ushirikiano wa lolote wanapomhitaji.

Ni hatua kama hiyo, ndio iliimuingiza katika kuongoza tume maalum ya kufuatilia za ushirika wa Nyanza, akionyesha mafanikio makubwa ya kurejesha.

Huyo ni Mzee Masele, ambaye umri wake 'jua limekuchwa' na simulisi mzizi wake inaanza robo tatu ya karne sasa.Je, wanafunzi wa sasa wana yepi?

***Mwandishi wa makala hii anapatikana kwa barua pepe: anthonygervas@yahoo.com na simu (+225)0682 86 92 44, Kanda ya Ziwa.***

> **"Baada ya hapo aliendelea kutumikia ushirika huo, uliopitia mabadiliko na kuundwa Ushirika wa Nyanza, alistaafu mwaka 1999, akiwa katika nafasi ya Meneja Mkuu.**

# TRC inavyokabili janga kuu la corona



Abiria wa treni za TRC, katika stesheni ya Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Mwandishi Wetu**

MAPAMBANO dhidi kuambukizana maradhi corona ni makubwa. Katika sekta ya usafiri, tayari kuna hatua kubwa zimeshachukuliwa ikiwamo kudhibiti abiria wanaosukumana.

Katika kukabili hilo, Shirika la Reli Tanzania (TRC), limechukua hatua kubwa, hasa katika kipengele cha kusafisha mikono na mingineyo kwa abiria.

Baada ya tamko hilo, maofisa TRC walianza kuendesha mafunzo kuhusu namna ya kuzuia maambukizi ya virusi vya corona, kwa kutoa elimu kuhusu mambo ya kuzingatia, ili kujikinga na maambukizi katika stesheni kuu eneo la Kamata Kariakoo, jijini Dar es Salaam.

Ni kazi iliyoanza wiki mbili ziliopita, ikitoa mafunzo kwa wataalamu wa afya kutoka Zahanati ya Reli Makao Makuu, yakiongozwa na Mganga Mkuu wa Zahanati, Dk. Peter Mathew.

Awali, mafunzo yaliendeshwa kwa pamoja, wafanyakazi na uongozi wa TRC makao makuu, lengo ni kuhakikisha abiria wa treni za mjini (daladala) na mikoani, wanapata uelewa wa kutosha kuhusu namna bora ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona, vilivyoingia nchini.

Hadi sasa, TRC inaendelea kutekeleza maagizo ya serikali kudhibiti kuenea kwa maambukizi ya ugonjwa huo, ikihudumia hilo katika maeneo yote nchini yaliyopitiwa na reli, hasa katika stesheni za reli zenye idadi kubwa ya wasafiri.

Hapo zinatajwa Reli ya Kati, kuanzia Dar es Salaam, Morogoro, Dodoma, Tabora, Kigoma, Mpanda na Mwanza, pamoja na reli ya Kaskazini kuanzia Ruvu, Tanga, Moshi hadi Arusha.

TRC ineleza kuwa, sambamba na hilo, hivi sasa linaendelea kutoa elimu kwa wafanyakazi kupitia hospitali za Shirika zilizopo katika maeneo hayo.

"Shirika lilianza kutoa elimu ya afya kwa wafanyakazi wake pamoja na wananchi wanaoishi pembezoni mwa reli, tunatoa vipeperushi na matangazo, ili kuhakikisha ugonjwa hauingii kupitia sisi, ndani ya treni zetu kuna vyumba vya huduma pamoja na mtaalamu wa afya" anasema

Mganga huyo anaendelea: "Anapotokea mgonjwa wa Corona tutampatia huduma zote kwenye chumba cha huduma kwa kumtenga na tutamshusha katika vituo vyetu vya afya vilivyopo njiani, Morogoro, Dodoma, Itigi, Tabora, Kigoma, Mwanza, Tanga pamoja na Moshi"

Miongoni mwa hatua TRC imeshachukua mpaka sasa, ni kuhakikisha abiria wanaosafiri kwa treni zote za mjini na mikoani, wanakaa kulingana na idadi ya viti vilivyopo maarufu 'level seat' ili kuondoa msongamano wa abiria unaoweza kuongeza maambukizi.

Sambamba na hilo, TRC imeweka maji na dawa ya kuosha mikono kwa ajili ya kuua virusi vya corona katika maeneo ya kazi na stesheni zote nchini.

Mkuu wa Habari na Uhusiano wa TRC, Jamila Mbarouk, anaeleza kinachofanyika ni kuunga mkono jitihada za serikali, kupambana na maambukizi mapya, ikizingatiwa shirika linadumaa usafiri wa abiria.

Anasema shirika linaendelea kutoa elimu kupitia vyombo vya habari, mitandao ya kijamii, vipeperushi na mikutano ya ana kwa ana na abiria, wananchi na wafanyakazi katika maeneo ya stesheni, kambi za ujenzi na maeneo ya pembezoni mwa reli.

**Kwa mujibu wa tovuti ya TRC.**

BIASHARA

MWALIMU NA MJASIRIAMALI...

# Mtotoa vifaranga anayesimamia siri mafanikio, nyenzo nishati

## • Adokeza keki yumo, huko anaegemea mkaa

INATOKA UK.13

Ni biashara aliyoifanya kwa miaka mitano iliyopita na awali alikuwa anatotolesha kwenye mashine za watu wengine, lakini badaaye aliguswa na gharama kubwa, pia kuna wakati anaambulia vifaranga wachache. Kabuti anasema, kipindi hicho alikuwa ana tenda mbalimbali za vifaranga na akaona njia ya kupunguza gharama anazotumia, ni kanunua mashine binfasi ya kutotoa vifaranga.

"Nilivyoona ni gharama kutotolesha kwa watu, ilinibidi nikanunue mashine ya kutotolesha na mimi nawatotoleshea kwa Sh 10,000 kwa kila trei," anasema na kuongeza: "Kama atatumia mayai yangu atalipa Sh. 25,000 kwa kila trei akija na maya yake nitamtotoleshea kwa Sh. 10,000."

Pia, anasifu mashine hiyo kwamba hata ikikaa asipopata wateja, hakuna hasara.



Mashine anayotumia kutotoa vifaranga. **PICHA ZOTE: BEATRICE SHAYO**

### MAANDALIZI

Rehema anazungumzia mashine hiyo jinsi inavyofanya kazi, kwamba huwa anakusanya mayai yaliyotagwa kuanzia siku moja hadi sita na kuyaweka katika trei.

"Ile siku ya sita nayaweka katika mashine. Hii mashine inauwezo wa kuweka mayai 528. huwa naweka trei sita ambazo zinabebaba mayai 88 kwa kila moja," anasema na kuendeleza simulizi: "Huwa najaza mitungi yangu miwili ya gesi kwa ajili ya kusaidia na umeme jua katika uzalishaji wa vifaranga."

Anasema ameunganisha umeme jua na wa gesi, hivyo vina uwezo wa kufanya kazi kwa pamoja, endapo umeme wa jua umepungua nguvu, mbadala wa gesi unafanya kazi.

Kabuti anaeleza:"Kama kitu kimoja kikipungua kuna alama itatoa ambayo ni kelele tutaenda kuangalia na kurekebisha kile ambacho kinaonyesha katika mashine. Mwanga ukiwa mkali wa jua moto wa gesi unatakiwa kupungua

"Kuna kipindi joto likiwa kubwa 38.1 kama likiendelea kuongezeka vifaranga vinakufa ni muhimu kufuatilia kwa ukaribu."

Kwa mujibu wa rehema, ili kutotoa vifaranga kinachotakiwa ni nyuzi joto 37.8 kiwango kinachosimamiwa na mashine yenyewe hata pale joto linapoongezeka. Kimsingi, haitakiwi ama joto kuongezeka au kupungua katika mashine.

Anaeleza kuwa mayai hayo hukaa kwenye mashine kati ya siku 19 na 23 na ndipo yanaanza kutoa vifaranga.

> **"Kuna kipindi joto likiwa kubwa 38.1 kama likiendelea kuongezeka vifaranga vinakufa ni muhimu kufuatilia kwa ukaribu.**

Rehema anasema utaratibu wake wa matunzo ni kwamba iwapo kuna vifaranga vimebaki, huwa anavifuga na anapomtolea mteja ndipo anamuuzia, apake haikuwa ameshawapatia chanjo.

"Kuna wale wateja ambao hupiga simu na kuulizia kama Kabuti una vifaranga, Huwa nawapatia, najitahidi kuweka na vya akiba," anaeleza.

Mjariamali huyo ambaye pia ni mwalimu katika Shule ya Msingi Malamba Mawili, anasema kifaranga kimoja anauza kwa bei ya Sh. 1,500 wakiwa na siku moja hadi mbili na baada ya hapo wanapanda hadi kati ya Sh. 2000 na Sh. 3,000.

Anasema sababu iliyomfanya kutumia teknolojia ya umeme jua na gesi, ni changamoto inayompata ya kukatika kwa umeme kila wakati, kilimchomfanya mara nyingi ashindwe kutotolesha vifaranga na kujikuta anapata hasara.

"Embu fikiria, umeweka mayai yako katika mashine kwa ajili ya kutotolesha wakati wote linahitajika joto halafu umeme unakatika, haujui unarudi saa ngapi," anaanika picha ya tatizo.

Anaendelea: "Kitendo hicho huwezi kutotolesha, utakuwa unaharibu mayai, maana joto linahitajika umeme hakuna na ndio maana nikaona nitumie umeme jua hata unapopungua naunganisha na gesi."



Kazi yake katika kutengeneza keki.



Rehema kabuti, akiwa na kuku alimtotoa kwa mashine yake .

Rehema anasema kila mwezi amekuwa akizalisha vifaranga 500 katika mashine hiyo na changamoto inayompata ni wasaidizi wake wa kazi wanatakiwa kuwa wasafi na mabanda ya kuku yanatakiwa usafi wakati wote, endapo asipofanya hivyo utagaji unakuwa hafifu.

"Kuku wanataka amzoee mtu usipomjali utagaji unakuwa hafifu. Kama mtu hafanyi usafi na wewe si msafi utamfanya kuku asitage," anasema.

### ANATENGENEZA KEKI

Mwalimu huyo mbali na biashara hiyo, anasema ana eneo lingine la ujasiriamali wa kutengeneza keki kwenye sherehe mbalimbali kwa kutumia 'oven' ya mkaa.

Anakiri kuipenda teknolojia hiyo, kwani inamgharimu fedha kidogo, kupitia nishati mkaa, akilinganisha na umeme huku akieleza kuwa upikaji keki una changamoto, kwani wengi wao wanapika 'ili mradi' pasipo kufuata taratibu zinazotakiwa.

"Utakuta mtu kanunua keki dukani inanata, ina maana upishi wake ni tofauti, japo utakuta inauzwa kwa bei rahisi dukani," anaibua siri na anaendelea:

"Lazima auze bei rahisi, kwa sababu katika keki anaweka maziwa kwa hali ya kawaida. Maziwa katika keki sio nzuri, ndio maana unakuta keki inanata, lakini ukichukua keki kama hizi ninazozitengeneza hata wiki nzima, utaikuta bado ipo vizuri."

Rehema anatahadharisha kuwa, upishi wa keki hautakiwi kuongeza chochote zaidi ya mayai, siagi na sukari akihimiza ufafanuzi:

"Wengine wanaona gharama kubwa katika kuweka mayai mengi na kuamua kuongeza maziwa. Nikichukua keki ya kilo moja, naweka 'blue band' ya kilo moja, sukari nusu (kilo) na mayai 16. Hapa ndio ninaanza kutengeneza keki yangu,"

Ni shughuli anazosema zinafanyika baada ya kutoka kazini, akiwa na ufafanuzi wake: "Huwa sipendi kupoteza muda kabisa ninapotoka kazini nahakikisha nafanya shughuli zangu za ujasiriamali.

"Nikisema nitegemee mshahara nitashindwa kuendesha majukumu mengine. Hivyo, akili yangu huwa inawaza ubunifu kila wakati. Hapa kwangu nauza na maua ukapendezeshe nyumba yako na hata asali nauza," anaeleza Rehema.

### MRATIBU NISHATI KIJANI

Mratibu wa Mradi wa Nishati Kijani na Usawa wa Kijinsia (Tangsen), Thabiti Mikidadi, anasema wamegundua sekta ya nishati haina wawakilishi katika ngazi za wilaya, tofauti na nyinginezo.

"Kutokana na hali hiyo, masuala ya nishati hayajulikani katika ngazi za wilaya na watu wengi wanajua nishati ni umeme na umeme unachukua asilimia kubwa ya nishati," anasema Thabit.

Anasema wao kama wataalamu wa nishati ya jinsia, wanatambua matatizo mengi ya kijinsia, yanasababishwa na ukosefu wa nishati.

Hivyo wameona watoe elimu katika ngazi ya wilaya, ili watambue fursa zilizopo katika nishati, pamoja na kutambua matatizo yaliyopo ya kijinsia katika masuala ya nishati ili wapange mipango ya maendeleo.

Mikidadi anasema, matunda mengi yanaharibika hasa katika Mkoa wa Dar es Salaam, licha ya kuwepo soko la usindikaji.

"Tunataka maofisa wa wilaya wajue namna ya kutatua matatizo ya watu kupitia teknolojia mbalimbali za nishati na tumeanza mafunzo kwa Wilaya ya Pwani itakapofanikiwa tutakwenda kutoa elimu katika wilaya nyingine," anasema.

# Biashara katika picha



Mchuuzi wa matunda akisubiri wateja katika soko kuu la Majengo, jijini Dodoma juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**



Mchimbaji mdogo wa madini Makomba Faustine, akiangalia kwa makini kama atafanikiwa kupata almasi wakati zoezi la uchenjuaji wa makinikia ya almasi linaloendelea nje kidogo ya mgodi mkubwa wa almasi wa Mwadui, mkoani Shinyanga jana. **PICHA: ANTHONY ISHENGOMA**



Mchuuzi wa miwani (kushoto), akiwahudumia wateja wake katika gulio la Tangamano, jijini Tanga mapema wiki hii. **PICHA: DEGE MASOLI**

BIASHARA

MIKOPO SH.MIL 301

# Halmashauri Shinyanga 'zajibu' kuelekezea kinamama na vijana

• DC na angalizo 'michezo pool'

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

MSIMAMO wa serikali, unajikita katika kusimamia kila Mtanzania anafanya kazi, ili aweze kujiingizia kipato kwa njia halali na asiwe tegemezi katika familia yake.

Ni katika msimamo huo, serikali imeamua kutoa fedha kupitia halmashauri zote nchini, asilimia ya kipato chao kinalenga kuwakopesha vijana, wanawake na wenye ulemavu,

Wahitaji walijitokeza kwa wingi, sehemu kubwa wakiwa ni wanawake, hasa kupitia vikundi vyao na wanarejesha kupitia njia hizohizo.

Nia ya serikali kupitia halmashauri zake, zilizopewa mwongozo wa kuhakikisha katika mapato yao ya ndani wanatenga asilimia 10 ya bajeti yanaelekezwa kwa makundi ya walemavu, vijana na wanawake.

Katika Wilaya ya Kahama yenye Halmashauri tatu; Ushetu, Halmashauri ya Mji Kahama na Msalala, tayari zimeweza kuitikia wito wa serikali kwa ajili ya kutoa mikopo kwa makundi hayo matatu yaliyoainishwa.

Ushetu haiko nyuma. Imekuwa ikitenga fedha kupitia mapato yake ya ndani kila robo ya makusanyo yake, ikitenga fedha za mikopo ya makundi ya vijana, wanawake na walemavu.

Tangu mwaka wa fedha wa 2015/2016 mpaka wa sasa 2019/2020, Halmashauri ya Ushetu inasema meshatoa zaidi ya asilimia 68 ya mikopo katika vikundi vya kinamama, vijana na watu wenye ulemavu, sehemu kubwa ya wanufaika ni kinamama.

Ni kikundi kinachonufaika zaidi, kutokana na hamasa ya kunufaika na mpaka sasa, ndio vinaongoza kutokana na hali ya urejeshaji bila ya usumbufu, kuliko makundi mengine.

**OFISA MAENDELEO JAMII**

Minaeli Ngomoi, ni Ofisa Maendeleo ya Jamii, katika Dawati la Uwezeshaji Wananchi kiuchumi, anasema, Halmashauri ya Ushetu imeshafanikiwa kutoa mikopo kwa vikundi vya kinamama, vijana na wenye ulemavu jumla Sh. milioni 301.1

Anasema, katika mwaka wa fedha 2015/2016 halmashauri ilishatoa mikopo kwenye vikundi saba vyenye wanachama 35 kwa thamani ya Sh. milioni nane.

Ngomoi pia anasema, katika mwaka wa fedha 2016/2017, halmashauri hiyo ilitoa mikopo kwa vikundi 21 na wanachama 105 waliopata jumla ya Sh. milioni 51 za kujiinua kiuchumi na kuongeza mitaji yao.

Hata hivyo, anasema katika mwaka wa fedha 2018/19, Halmashauri ya Ushetu, ilikopesha vikundi 16 vyenye wananchama 80 na ikapata jumla ya Sh. milioni 75.1.

Anafafanua kuwa, katika mwaka wa fedha 2019/2020 vikundi vya kinamama 35 vyenye wanachama 175 vilipata mkopo wa Sh. milioni 176, ikiondokana na adha ya riba kubwa za kitaasisi.



Diwani Viti Maalumu Kata ya Ulowa, Gabriela Kimaro na Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Elias kwandikwa, wakiwa ndani ya bajaji baada ya kukabidhi kwa kikundi.

> **Niwaombe kinamama mnaoishi na vijana wetu huko majumbani kuwaelimisha matumizi ya fedha na wazielekeze kwenye shughuli ambazo waliombea fedha hizo ili kujiinua kimtaji na kiuchumi.**



Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri ya Ushetu, Minaeli Ngomoi, akisoma taarifa ya miaka minne ya utoaji mikopo kwa vikundi vya kinamama, vijana. **PICHA ZOTE: SHABAN NJIA.**

**WAZIRI UJENZI**

Elias Kwandika, ni Mbunge wa Ushetu na Naibu Waziri wa Ujenzi, anawasifu wanawake katika Jimbo hilo ni hodari katika ufanyaji biashara ndogo na wanapowekewa misingi mizuri, wana uwezo wa kuinuka kibiashara katika siku zijazo.

Anarejea zama zilizopita, kuwa, mifumo ya kuwawezesha wanawake, vijana na walemavu haikuwa mizuri, lakini kwa sasa ni jambo linalotekelezwa na halmashauri zote nchini, kwa kupitia mapato yake ya ndani, lengo ni kujiinua kiuchumi.

"Nimpongeze Mkurugenzi wangu, Michael Matomora, kwa kutekeleza agizo la kutenga asilimia kumi ya mapato ya ndani kwa vitendo," anasema Kwandikwa.

Naibu Waziri Kwandikwa anawataka maofisa maendeleo ya jamii wanakotoa mikopo katika vikundi hivyo, iendane na utoaji elimu ya matumizi ya fedha hizo, hasa vikundi vya vijana wanaodaiwa walichukua fedha kwenda kujihusisha katika michezo ya kubahatisha na ubashiri.

Pia, anawataka kinamama kuhakikisha wanawafuatilia watoto wao wa kike shuleni, ili wasome kwa bidii na kujitambua, kwani ndio watakaokuwa msaada mkubwa katika kata zao na familia wanazotoka.

Anawapa angalizo kwamba hadi sasa kuna vijana wengi walioko katika vyuo vikuu wanatoka, Halmashauri ya Ushetu baada ya kusimamiwa na wazazi wao vizuri.

**DIWANI ULOWA**

Diwani Viti Maalumu kutoka Kata ya Ulowa, Gabriela Kimaro, anampongeza Mkurugenzi wa Hamashauri ya Ushetu, Michael Matomora, kwa kuviwezesha vikundi vya kinamama, vijana na walemavu wa mikopo isiyokuwa na riba kwa kuinua mitaji yao na kupunguza wimbi la vijana mitaani.

"Awali kata zetu kulikuwa na vikundi vingi vya kinamama, vijana na walemavu waliokuwa na shughuli zao za kufanya, lakini mitaji yao ilikuwa haitoshi kukua kibiashara.

"Sasa hivi wametoka kuwa wafanyabiashara wadogo hadi wa kati baada ya Halmashauri yangu kuwawezesha mikopo isiyokuwa na riba," Gabriela.

Anasema katika kila robo ya kwanza ya makusanyo ya fedha za mapato ya ndani, Halmashauri Ushetu imeshatenga asilimia 10 kwa ajili ya vikundi hivyo, katika mgawanyo vijana na kinamama, kila kundi linapata asilimia nne ya fedha zilizotengwa na asilimia mbili zinaenda kwa walemavu.

Rai yake, vikundi vya kinamama viendelee kuwa mfano wa kuigwa katika urejeshaji mapema mikopo na kuhamasisha vikundi vya vijana kutumia fedha hizo kwa busara.

**DC KAHAMA**

Mkuu wa Wilaya Kahama, Anamringi Macha, anasema vijana wamekuwa na matumizi mabaya ya fedha, kwani fedha wanazopata wamekuwa wakielekeza katika michezo ya kubashiri na wanashindwa kuzirejesha kwa wakati.

Anasema, Kahama ina michezo mingi ya kubashiri na bonanza na vijana wengi wamekimbilia huko, wakidhani wanaweza kupata fedha nyingi.

"Niwaombe kinamama mnaoishi na vijana wetu huko majumbani kuwaelimisha matumizi ya fedha na wazielekeze kwenye shughuli ambazo waliombea fedha hizo ili kujiinua kimtaji na kiuchumi," anasema.

BIASHARA

# Wanahabari Nyanda za Juu Kusini walipotua Hifadhi Serengeti kutalii

- Dereva watalii: Trafiki watusaidie biashara
- DED Serengeti: Maboresho zaidi yanakuja

**Na Francis Godwin,** aliyekuwapo Serengeti

HIFADHI ya Serengeti inapatikana katika mikoa ya Mara na Arusha, ikipakana na nchi ya Kenya. Ni eneo pekee duniani lenye kundi kubwa la wanyama wanaohama katika mfumo mzima wa msafara.

Hifadhi ya Taifa ya Serengeti yenye ukubwa wa kilomita za mraba 14,763 ilianzishwa mwaka 1951 na iko maarufu kuvutia watalii kutoka nje ya nchi, kushuhudia makundi ya wanyama wa aina na mandhari tofauti.

Umaarufu wa Serengeti, pia unatokana na misururu mirefu ya wanyama nyumbu wanaohama, hata kuna wakati wanavuka mpaka kuingia hifadhi jirani ya Maasai Mara nchini Kenya.

Takwimu za Mamlaka ya Hifadhi Tanzania (Tanapa), zinaonyesha zaidi ya nyumbu milioni moja, huunga misafara ya kutafuta malisho na maji.

Ujangili katika kipindi cha nyuma, ilikuwa changamoto kubwa hifadhini Serengeti, lakini hatua mbalimbali zilichukuliwa kukomesha hilo na taarifa za sasa, uhalifu huo umepungua sana, sababu mojawapo ni kuwa na sera ya ujirani mwema na vijiji jirani vinavyozunguka eneo hilo.



Msafara wa nyumbu wakiwa katika Hifadhi ya Taifa Serengeti. **PICHA: MTANDAO.**

### ZIARA HIFADHINI

Waandishi wa habari kutoka mikoa ya Iringa na Mbeya, wamefanya utalii wa ndani katika hifadhi hiyo kujifunza changamoto na mafanikio ya yake, ili kutia chachu ukuaji wa sekta ya Utalii kwa mikoa ya Nyanda za juu Kusini.

Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, kunakopatikana mikoa ya Mbeya na Iringa, nako kuna hifadhi kadhaa, ikiwamo ya pili kwa ukubwa kitaifa -Ruaha, Ziwa Ngosi wilayani Rungwe, katika milima ya Uporoto na Daraja la Mungu lililopo mkoani Songwe.

Mkuu wa kitengo cha Ujirani Mwema, hifadhini Serengeti, Zabron Mtweve, anasema ujangili katika hifadhi hiyo umepungua kwa kiasi kikubwa, hasa kutokana na mchango wa ujirani mwema kutoka kwa wananchi.

Mtweve anasema walitoa elimu kwa wananchi na sasa wanajua umuhimu wa hifadhi na sasa wanaendelea kushirikiana na wadau hao kwa elimu zaidi mpaka shuleni.

Anasema, kuanzishwa miradi mbalimbali kumesaidia jamii kujikwamua kiuchumi, kama vile ufugaji nyuki wilayani ya Ngorongoro na kuhamasisha kuanzishwa vikundi vya fedha za kukopeshana katika wilaya jirani kama vile ya Bunda, Tarime na Bariadi.

Akizungumzia mafanikio ya Idara ya ujirani mwema alisema TANAPA imeanzisha mpango wa matumizi bora ya ardhi ambao utasaidia kutatua migogoro ya mipaka baina ya wananchi na vijiji jirani na hifadhi yenyewe.

> **“Ujangili katika hifadhi hiyo umepungua kwa kiasi kikubwa, hasa kutokana na mchango wa ujirani mwema kutoka kwa wananchi.**




Baadhi ya wanahabari walipokuwa katika ziara hifadhini Serengeti, hivi karibuni. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

### DEREVA WATALII

Johnson Ndilakwe, dereva wa magari ya kubeba watalii, anaitaja Serengeti ni hifadhi bora zaidi kwa wananchi kunufaika kiuchumi na katika sura ya pili ana malalamiko kuwa baadhi ya askari wa usalama barabarani wanasumbua magari ya watalii katika barabara kuu.

Anashauri polisi wa usalama barabarani, kujenga mazingira ya kirafiki na misafara ya watalii, ikiwa ni namna mojawapo ya mchango katika kuvutia sekta hiyo, akitoa mfano hai wa wananchi askari trafiki wa mikoa ya Kaskazini.

Ndilakwe anasema, kwa sasa serikali kupitia wizara ya Maliasili na Utalii, imekuwa akielekeza nguvu nyingi katika kutangaza vivutio vya utalii na hifadhi mbalimbali, zikiwamo za mikoa ya Kusini kufanikisha mvuto wa utalii kitaifa.

Anasema Hifadhi ya Taifa Serengeti, ina mvuto mkubwa hata watalii wengi kitaifa kutaka kweda huko, lakini kuna walakini wa kukwazwa na miundombinu duni inayofanya baadhi ya maeneo yasifikike katika hifadhi hiyo

Dereva Ndalikawe katika maoni yake, anashauri halmashauri zinazozunguka hifadhi kutenga bajeti ya uboreshaji miundo mbinu, kwani kupitia watalii hao, mapato yake ya ndani yamekuwa yakiongezeka kila wakati

### WANAHABARI

Mwenyekiti wa chama cha Waandishi wa Habari Mkoa wa Iringa (IPC), Frank Leonard, anasema sekta ya utalii ikisimamiwa vizuri na kujitangaza ndani na nje nchi, ni moja ya chanzo kikubwa sana cha pato la nchi.

Leonard anaitaka Serikali kuwekeza zaidi katika sekta ya utalii hasa katika miundombinu ya Barabara, ujenzi wa Hotel za hadhi ya kitalii ndani ya hifadhi na uboreshaji wa makusanyo katika sekta hiyo ili mapato hayo yatumike katika kukuza pato la Taifa.

Mwanahabari, Laundence Simkonda. kutoka Mkoa wa Mbeya anaelezea ziara hiyo ya utalii kwenye Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, imekuwa na tija kubwa kwao kwani wataitumia ziara hiyo kufikisha kwa umma jinsi ambavyo wanaweza kunufaika moja kwa moja na Hifadhi za Taifa kwa kujikita katika shughuli za bidhaa za Kitalii .

Anasema, mji wa Serengeti na maeneo mengine yamezungukwa na Hifadhi za Taifa na zina nafasi ya kutumia fursa ya kuwa karibu na kwa kufanya shughuli za biashara za kitalii.

Tukuswiga Mwaisumbe, Katibu Mtendaji wa IPC, anaesema wao wanahabari wana nafasi kubwa ya kukuza uchumi wa utalii, hivyo anaiomba serikali kuwaongezea wigo wa kutangaza utalii ndani.

### DED SERENGETI

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti, Rebeca Msambuse, anasema kuwa halmashauri hiyo ipo katika mkakati wa uboreshaji wa miundombinu inayozunguka Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, ili kuwavutia watalii zaidi kuendelea kutembelea, ikiwa ni hifadhi yenye watalii wengi zaidi nchini.

Pasipo kutaja kiwango cha fedha zilizotengwa na urefu wa barabara zitakazojengwa kwa kiwango cha lami na changarawe, Rebecca anasema mpango wa uboreshaji wa miundombinu unategemewa kuanza kutekelezwa mwaka huu.

UCHUMI

# Mustakabali wa kuambukizana corona na kitendawili umaskini




Utekelezaji wa agizo la serikali, abiria kunawa kabla, kuepuka kuambukizana maradhi corona, kabla ya kupanda basi mjini Musoma. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**Na Nimi Mweta**

HOFU ya kuenea kwa kasi ugonjwa wa homa ya mapafu au corona ilikuwa kubwa, wakati idadi ya matukio ya kuambukizwa ilipofikia siku chache zilizopita.

Katika hali hiyo ilijenga mazingira watu wasitoke nje, ila kwa sababu za lazima kabisa. Katika nchi zilizoendelea haikuwa vigumu wao kuchukua hatua hizo. Kukaa nyumbani ndiyo hitaji la kwanza, kuzuia maambukizi yanayochukua kasi duniani.

Je, tunaliweza hilo na itakuwaje kiuchumi? Kuna hatua nchini kama serikali kuzipa nafasi yao, nyumba za ibada kupanga taratibu zao za udhibiti, wakati masoko na maeneo ya wazi na biashara yakiendelea na kazi.

Sababu iko kazi, kuna watu wengi zaidi jijini Dar es Salaam na miji mingi mikubwa na kwingineko nchini, hawana ajira halisi/rasmi za uzalishaji au utoaji huduma, ila kutegemea ubangaizaji.

Hapo inamaanisha hufanya uamuzi mchana kutoka ili wakapate nafasi za kutoa huduma hii na ile kama kushusha mizigo kwenye magari, kuchota maji na kusaidia ujenzi. Ni lazima na ndivyo wanavyotafuta riziki.

Umuhimu wa kubaki nyumbani umesisitizwa katika nchi kadhaa, kwa mfano watazamaji wa televisheni moja ya kigeni wakiwa nchini, walishtushwa kuona polisi wakiwa na fimbo ndefu kuwapiga waliokutwa wanapita barabarani au wamepanda vespa kwenda huku au kule.

> **Kuna mwanamke nchini Marekani ambaye taarifa zilisema hakuwa na bima, akaingia hospitalini kutibiwa alipoambukizwa, halafu akakabiliana na bili ya Dola za Marekani 35,000 (Sh. milioni 80.5).**



Abiria wa daladala wakigombea kuingia katika basi, hali iliyo hatari kiafya, hasa dhidi ya ugonjwa corona. Hivi sasa kuna agizo mabasi yote yasizidishe abiria waliokaa kwenye viti.

Nchini India, ambako wemeshaguswa wao siyo matajiri kwa kiwango cha kipato cha wastani wa mtu mmoja mmoja, licha ya kuwa na uchumi wa kati.

Bila shaka sehemu yake kubwa ni viwanda na haikuwa kazi rahisi sehemu kubwa ya watu kubaki tu nyumbani.

Bado hakuna ufafanuzi wa kina kuhusu namna wanayomudu chakula, lakini nchini Marekani hali ilikuwa tofauti, kwani baadhi ya maduka ya kisasa makubwa au maarufu 'supermarkets' yalianza kuajiri wafanyakazi zaidi kupeleka bidhaa katika makazi ya watu wanapotoa orodha ya wanachohitaji, halafu wanalipa kwa kadi, vitu vinapofikishwa.

Benki Kuu ya Marekani (Federal Reserve), ilipunguza viwango vya riba vikaribie sifuri, ili kuchochea uchumi.

Iyalia nako, mwanzo iliifuata China kwa kuwa na idadi kubwa ya wagonjwa wa corona. Ilijaribu kufuata mwelekeo huo, ikawa inakwama, kwani viwango vya kipato chenye uhakika hata kama mtu hana ajira ni kidogo.

Kwa mfano, kuna upinzani mkubwa kuhusu wahamiaji wanaoopolewa baharini wakikaribia kuzama, wanapoingia katika ardhi ya Italia, inabidi serikali iwajali na siyo kuwaacha waingie mitaani kivyao.

Ugumu wa kutekeleza sera ya kutotoka nyumbani unajionyesha katika viwango vya homa ya corona nchini Marekani, ambako jiji tajiri la New York kwa wiki kadhaa sasa, limekuwa mbadala wa Wuhan huko China, eneo ambako corona inapiga kwa nguvu zaidi duniani.

Kuna jiji la Bergamo Kaskazini mwa Italia, pia nchini Hispania, lakini kutokana na ukubwa wa New York katika uchumi wa Marekani na dunia nzima, hali yake imekuwa ikitikisa dunia kupitia televisheni tofauti za Marekani na nchi nyinginezo.

Pia, ilikuwa kielelezo cha ugumu wa kuzuia homa ya corona, kwani kimsingi New York ina kila kitu - ila vifaa vya tiba inapopiga.

Katika eneo hilo, pia baadhi ya watu au wafuatiliaji wa habari kimataifa walikuwa wanapata kigugumizi kuwa hali ya corona itakuwaje nchini Tanzania na kwingineko Afrika, ikiwa uambukizaji utachukua sura ya Italia au Marekani na tunaishi kwa ubangaizaji, tutakabili vipi haya?

Kuna mwanamke nchini Marekani ambaye taarifa zilisema hakuwa na bima, akaingia hospitalini kutibiwa alipoambukizwa, halafu akakabiliana na bili ya Dola za Marekani 35,000 (Sh. milioni 80.5).

Ni changamoto kokote kule aendako mtu, anamudu vipi gharama ya namna hiyo, kama hana bima?

Hakuna mjadala wa kina mchini kuhusu namna ya kukaa umbali wa kutoka mtu mmoja na mwingine, kuku kinachotawala ni usafi mikononi na mfumo wa kuambukizana kwa namna nyingi, ikiwamo kupakana jasho na mgonjwa.

Hadi sasa kuna msisitizo wa kujihami kiafya, ikiwamo kunawa mikono au vizuizi usoni (mdomo na pua) hasa kwa wanaohudumia wagonjwa hospitalini na kukwepa msongamano wa kijumuia, ikiwamo katika vyombo vya usafiri.

Ndiyo maana kuu ya vita dhidi ya ugonjwa tumaini pekee la Tanzania na Afrika kwa jumla, ni huruma ya mbinguni kuwa umaskini nchini, unabeba magonjwa ya corona,

Hilio ni jambo lisilofikirika, kuitaka Afrika iingie katika hali ya jiji la New York, halafu ibaki imesimama baada ya miezi miwili, kwani maeneo karibu na Dar es Salaam ni wazi yangeambukizwa.

Corona inaacha maisha ya vitendawili, walio maarufu kama Waziri Mkuu wa Uingereza, Boris Johnson wa Kiongozi Mkuu wa Ujerumani, Angela Merkel kunasa katika maambukizi ya ugonjwa huo.





Baadhi ya wanawake wakiendelea na shughuli za ujenzi wa vyoo katika Shule ya Msingi Chalangwa, iliyoko Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, mkoani Mbeya, ikiwa ni sehemu ya kujiingizia kipato cha kujikimu kimaisha. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Agizo la JPM kumsaidia mgonjwa latekelezwa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

SERIKALI mkoani Mbeya, imekabidhi Sh.milioni moja na utekelezaji wa agizo la Rais John Magufuli la kumpeleka Elizabeth Sanga (35), mkazi wa Mwasanga katika Hospitali ya Taifa Muhimbili kitengo cha Mifupa (Moi), kufanyiwa uchunguzi wa kitabibu.

Elizabeth amekuwa akikabiliwa na maradhi kwa zaidi ya miaka minne sasa.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, ndiye alikabidhi fedha hizo nyumbani kwa Sanga, ambazo zilitokana na michango ya wadau mbalimbali. Chalamila alisema kupitia vyombo vya habari kuwa Rais Magufuli alimuona mwanamke huyo akielezea madhila anayopitia kutokana na ugonjwa unaomsumbua na kuhitaji msaada wa fedha na huduma za afya ili aweze kupona. Alisema Sanga alikaa ndani kwa zaidi ya miaka minne kutokana na kusumbuliwa na maradhi ya mfumo wa njia ya haja kubwa kuziba na kusababisha kujisaidia kupitia sehemu ya uke, hivyo kuwalazimu wataalamu wa afya kumwekea kifaa maalum sehemu ya utumbo ili kutoa haja hiyo.

"Nimeagizwa na Rais Magufuli kumsaidia huyu mama fedha na kumsafirisha hadi Muhimbili akapate matibabu haraka...Rais alimuona mama huyu kupitia vyombo vya habari, akielezea namna anavyoteseka na kuomba msaada wa matibabu kwa Watanzania," alisema Chalamila.

Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya, James Kasusura, alisema kuwa usafiri umeandaliwa na muuguzi ambaye atamsafirisha kutoka Mbeya hadi Dar es Salaam. Akizungumza kwa uchungu, Elizabeth aliishukuru Serikali chini ya Rais Magufuli kutoa maagizo ya kumsafirisha hadi Dar es Saalam kupata matibabu, na kuwaomba Watanzania wamuombee ili apone.

# Waiomba serikali bei elekezi ngano

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAKULIMA wa ngano mkoani Mbeya, wameomba Serikali kutoa bei elekezi ya zao hilo ili kuwanusuru na unyonyaji wanaofanywa na walanguzi.

Walanguzi hao wanalalamikiwa kununua bidhaa hiyo kwa bei ya chini ikilinganishwa na gharama za uzalishaji.

Wakizungumza kwenye uhamasishaji wa kilimo cha zao hilo ulioandaliwa na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Uyole Tari- Uyole, kwenye Kijiji cha Usoha Kata ya

Muungano wilayani Mbeya, walisema wamekuwa wakilazimishwa kuuza mazao yao kwa bei ya kati ya Sh. 8,000 na 15,000 kwa ndoo ya plastiki yenye ujazo lita 20.

Mmoja wa wakulima hao, Michael Mbugu, aliiomba serikali kutafuta mbinu za kuwasaidia wakulima wasidhulumiwe na walanguzi hao kwa kununua ngano kwa bei ya kutupa, kwani wamekuwa wakitumia nguvu na gharama kubwa katika uzalishaji wa zao hilo na kwamba bei hiyo haiwanufaishi.

"Tunaomba Serikali isikie kilio chetu kwamba tunatumia nguvu kubwa kuzalisha ngano, lakini kutokana na walanguzi kununua mazao yetu kwa bei ndogo hatuwezi kunufaika na mazao yetu, hivyo tunaiomba Serikali iingilie kati kwa kupanga bei elekezi ambayo itazingatia gharama za uzalishaji," alisema Mbungu.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika, alisema kuwa ipo changamoto ya maofisa kilimo kutofika kwa wakulima kusikiliza vikwazo vinavyowakabili na kuagiza kuwa kuanzia sasa wafike katika kijiji hicho kuzungumza na wakulima na kutatua tatizo hilo.

"Mkoa wa Mbeya una ardhi yenye rutuba nzuri ya kilimo, lakini tatizo lipo kwa maofisa kilimo kutowatembelea wakulima na kuwashauri mbinu bora za kilimo ikiwamo namna ya kupunguza gharama za uzalishaji, hivyo kuanzia sasa nawaagiza maofisa ughani kuwatembelea wakulima kila walipo na kutatua changamoto zao," alisema Ntinika.

Kuhusu changamoto ya bei ndogo ya zao la ngano, Ntinika aliwataka wakulima kuzingatia maelekezo ya wataalam ili wazalishe mazao yaliyo bora ambayo yatajiuza yenyewe kwa bei nzuri yakifika sokoni.

Mtafiti wa ngano, Dk. Rose Mongi, alisema wamezalisha mbegu za kutosha na wanatarajia kuzigawa kwa wakulima zaidi ya 400 ikiwamo kuwapatia elimu ya kitaalamu ya uzalishaji.

Alisema uzalishaji wa zao hilo bila kuzingatia elimu ya kitaalamu na matumizi ya mbegu bora ni sababu ya wakulima kupata mazao kidogo ambayo yanakandamiza uchumi wao.

Dk. Mongi alisema kuwa wameanzisha mradi wa kuwezesha wakulima katika kilimo cha ngano kwa ufadhili wa Benki ya Afrika baada ya kubaini kuwa kilimo cha zao hilo kina tija katika kuwakwamua wananchi kiuchumi.

# 119 wahitimu Veta ujenzi vyoo bora

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

VIJANA 119 wanaoishi katika mazingira magumu katika Halmashauri tatu za Mkoa wa Mbeya, wamehitimu mafunzo ya wiki tatu ya ujenzi wa vyoo bora katika Chuo ya Ufundi Stadi (VETA).

Vijana hao wanatarajiwa kwenda kujenga vyoo hivyo kwenye wilaya zao ili kunusuru jamii na magonjwa ya mlipuko hasa kipindupindu.

Mafunzo ya vijana hao yamegharimiwa na Shirika lisilo la kiserikali la kusaidia vijana lililo chini ya Kanisa Katoliki la CRS kwa kushirikiana na Halmashauri za wilaya kwa lengo la kulinda afya za wananchi kwenye maeneo husika.

Halmashauri ambazo vijana hao wanaoishi mazingira magumu wamechukuliwa ni Mbarali, Mbeya na Chunya, ambazo zimekuwa zikikumbwa na maradhi ya mlipuko hasa kipindupindu kila mwaka.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmshauri ya Wilaya ya Chunya, Sophia Kumbuli, alisema mradi huo wa ushirikishwaji wa vijana katika biashara ya ujenzi wa vyoo bora, utawasaidia vijana kujiajiri na kujiingizia kipato.

Kumbuli ambaye alizungumza kwa niaba ya wakurugenzi wenzake, aliahidi halmashauri hizo kuwasaidia vijana hao kupata mitaji kwa kuwakopesha kupitia fedha zinazopaswa kukopeshwa kwa vikundi vya vijana ambazo ni asilimia nne ya mapato ya ndani ya Halmashauri.

"Serikali ilishatoa maelekezo na sasa ni sheria kwamba kila Halmashauri itumie asilimia nne ya mapato yake ya ndani kuwakopesha vijana, mimi pamoja na wakurugenzi wenzagu tunaahidi kutumia fedha hizo kuwakopesha ili mpate mtaji wa kuendeshea shughuli zenu za ujenzi wa vyoo bora kwenye jamii yetu," alisema Kumbuli.

Kumbuli aliwataka vijana hao kuunda vikundi ili waweze kupata sifa ya kukopea fedha hizo kwa mujibu wa sheria na miongozo iliyotolewa na Serikali.

Pia Kumbuli alilishukuru shirika la CRS kwa kuwaondoa vijana kwenye mazingira magumu, na hatarishi na kuyataka mashirika mengine yanayojihusisha na masuala ya kijamii kuiga mfano huo.

Aliwataka vijana hao kwa niaba ya wenzao kwenye halmashauri zote tatu kuwa chachu ya maendeleo kwenye maeneo yao na kuwasaidia vijana wenzao kupata ujuzi kama huo ili kufikia malengo ya Watanzania kuwa na vyoo bora.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Uswege Kaminyoge, aliwataka vijana kutumia vizuri fursa za mikopo wanayoipata kutoka kwenye halmashauri ili kutimiza malengo yaliyokusudiwa.

Meneja wa mradi wa CRS, Ephraim Tonya, alisema lengo ni kuongeza msukumo na jitihada za serikali katika kuhakikisha jamii ya Watanzania wanatumia vyoo bora na pia kuwaondoa vijana hao katika makundi yasiyofaa kwa kuwapatia nyenzo za kuajiri na kutoa ajira kwa vijana wasio na ajira nchini.

Mkazi wa kijiji cha Isewe wilayani Chunya, Muone Mkumbo ambaye ni mnufaika kwa mradi huo, alisema alijifunza mbinu mbalimbali za ujenzi wa ujenzi wa vyoo bora katika jamii na kuwa wajasiriamali.



# Jafo amuagiza mkandarasi Suma JKT

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, amemuagiza mkandarasi wa Suma JKT kukamilisha ujenzi wa nyumba wa Mkuu wa Wilaya ya Dodoma Mei 7, mwaka huu.

Akizungumza jana alipofanya ziara ya kukagua ujenzi huo, Jafo aliagiza mkandarasi huyo kuongeza nguvu ili ujenzi wa nyumba hiyo ukamilike kwa wakati kutokana na kasi kuwa ndogo.

"Ukiangalia idadi ya mafundi hapa ukilinganisha na muda uliopangwa kukamilishwa kwa kazi naona kabisa haitawezekana, sasa ngoja nivumilie siku hizi 34, ambazo ziko ndani ya mkataba," alisema.

Aliongeza: "Kinachotakiwa ni kuongeza nguvu kazi na kubadilisha mpango kazi, Mhandisi wa Suma JKT hakikisha ongezeni nguvu kazi, ili nyumba hii ikamilike Mei 7 na Mei 8 Mkuu wa Wilaya abebe vitu vyake aingize ndani maana kwasasa hana nyumba."

Akitoa taarifa ya ujenzi wa nyumba hiyo, Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma, Happiness Mgalula, alisema walitenga kiasi cha Sh. bilioni 1.15 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya Mkuu huyo, lakini waliamua kutumia utaratibu wa 'Force account' ambapo zitajengwa nyumba tatu ikiwamo ya Katibu Tawala wa Halmashauri ya Chemba na Chamwino.

" Tulipompata Suma JKT tulikubaliana wajenge jengo hili la ghorofa moja kwa Sh. milioni 615, hivyo kufanya fedha zingine Sh.milioni 236 kutumika kujenga nyumba ya DAS wa Chemba na Sh. milioni 200 kwa ajili ya nyuma ya DAS wa Chamwino," alisema.

Katika hatua nyingine, Waziri Jafo alikagua ujenzi wa Hospitali ya Uhuru iliyopo Wilaya ya Chamwino, ambapo aliliridhishwa kasi ya ujenzi unaoendelea na utekelezaji wa maagizo yake ikiwamo ya kuongeza nguvu kazi.

Alisema kwa sasa kuna nguvu kazi ya watu 300 ambao wanajenga hospitali hiyo ikilinganishwa na awali ambapo walikuwa 100.

Jafo alisisitiza uongozi wa Suma JKT kuhakikisha wanasimamia ujenzi wa Hospitali hiyo ili ukamilike kwa wakati uliopangwa.

Naye, Mhandisi wa SUMA JKT, Omary Kabalangu, alisema wametekeleza maagizo yake ya kuongeza nguvu kazi kutoka watu 100 wa awali hadi kufikia 300, sambamba na kuongeza muda wa kufanya kazi kwa kujenga usiku na mchana.

Hospitali ya Uhuru inajengwa kwa Sh. bilioni 3.99, zikiwa ni fedha zilizotolewa na Rais John Magufuli baada ya kuahirisha Sherehe za maadhimisho ya Siku ya Uhuru, Desemba, 9 mwaka 2018 na zile zilizotokana na gawio la kampuni ya Airtel.



Mkurungenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa, Dk. Omari Mkulo, akizungumza katika kikao kazi cha kupanga mikakati ya maendeleo ya halmashauri hiyo, wilayani humo, mkoani Dodoma juzi. Wa (pili kulia) ni Mbunge wa Kongwa na Spika wa Bunge, Job Ndugai. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# DC apiga marufuku ukataji miti holela

**Na Paul Mabeja,** BAHI

MKUU wa Wilaya ya Bahi mkoani Dodoma, Mwanahamisi Mkunda, amepiga marufuku ukataji miti kwa wakazi wa eneo hilo bila kibali kutoka katika mamlaka husika.

Mkunda, alipiga marufuku hiyo wakati wa uzinduzi wa vipindi vya Redio uliofanyika katika kijiji cha Mpamantwa, wilayani Bahi.

Vipindi hivyo ambavyo vitakuwa vikiruka hewani katika baadhi ya redio za kijamii mkoani hapa kwajili ya kuelimisha wananchi juu ya mpango wa kutumia Kisiki Hai, kukijijanisha mkoa wa Dodoma chini ya uratibu wa shirika la Lead Foundation.

Mkuu huyo wa Wilaya alisema kuwa kuanzia sasa ni marufuku kwa mwananchi yeyote kukata mti wowote bila kibali kutoka mamlaka husika.

Alisema ukataji miti umekuwa ukichangia katika kupotea viumbe hai lakini pia matumizi ya fedha nyingi katika kurejesha uoto wa asili uliopotea.

"Hapa nimeambiwa katika miaka ya nyuma mlikuwa mnalima mbogamboga katika kipindi cha mwaka mzima, lakini kutokana uharibifu wa mazingira hali imebadilika ikiwemo upungufu wa mvua hali ambayo imesababisha watu kubadili kazi na kwenda kugonga mawe," alisema Mkunda.

Naye Meneja Mradi wa Kisiki Hai, kutoka shirika la Lead Foundation, ambao ndio watekelezaji, Njamasi Chiwanga, alisema mpango huo umesaidia katika kurejesha uoto wa asili katika maeneo ambayo yalikuwa yameharibiwa na shughuli za kibinadamu.

Chiwanga alisema kuwa kwa kutumia mpango wa Kisiki Hai wamezifikia Wilaya zote saba za Mkoa wa Dodoma katika vijiji 300 na kurejesha miti zaidi ya milioni nne na lengo likiwa ni kufikisha miti milioni nane.

Akizungumza juu ya uzinduzi wa vipindi hivyo vya Redio Chiwanaga, alisema vitasaidia kuwafikia watu wengi katika maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Dodoma.

"Vipindi hivi vitasaidia katika kutoa elimu kwa wananchi kutumia mpango huu wa Kisiki Hai kukijanisha Mkoa wa Dodoma njia ambayo haina gharama ambayo itasaidia kurejesha uoto wa asili kama ambavyo mataifa mengine yamefanikiwa," alisema Chiwanga.

Pia alisema vipindi hivyo vitasaidia kufika katika maeneo ambayo hawajayafikia kwani hadi hivi sasa wamefika katika vijiji 300 kati ya 600 vya Mkoa wa Dodoma.

## Askofu: Walemavu waangaliwe corona

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

ASKOFU wa Kanisa la PHAM (T) jijini Dodoma, Julius Bundala, ameiomba serikali kuangalia kwa jicho la tatu makundi maalumu ya watu wenye ulemavu waishio vijijini kwa kuwapatia elimu ya kutosha jinsi ya kujilinda dhidi ya corona.

Aidha, kuhusiana na matumizi sahihi ya vifaa vya kuwasaidia kuepukana na maambukizi ya virusi vya gonjwa hilo.

Alisema wakati serikali ikitilia mkazo mkubwa wa kuwaelimisha watu wa mijini katika mikakati ya kujilinda na virusi vya ugonjwa huo, pia ikumbukwe kuna makundi yaishio vijijini wakiwamo walemavu na wazee wasiojiweza.

Bundala alisema hayo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma na kusema kuwa pamoja na juhudi na mikakati mikubwa inayofanywa na serikali, bado kuna uhitaji mkubwa kwa makundi hayo.

"Naipongeza serikali yetu tukufu, kwa jitihada kubwa zinazofanya kuhusiana na kuondokana na ugonjwa huu kwa elimu na makatazo yanayoelezwa, lakini bado pia huko vijijini wataalamu na viongozi wanajukumu la kuwafikia watu hao wenye mahitaji maalum," alisema.

Katika hatua nyingine, askofu huyo alisema ugonjwa huo unaweze-kana kutokomezwa, lakini ni pale tuu Watanzania watakapotii na kufuata maelekezo yanayotolewa na viongozi.

Alisema kama Watanzania watazingatia maelekezo na kufuata masharti kwa vitendo huku wakimuomba Mungu kwenye nyumba za ibada ugonjwa huo ataondolewa na tutakuwa huru.

Pia askofu huyo aliwataka Watanzania kutouchukulia ugonjwa huo kama vile umekuja kwa maigizo, bali uchukuliwe kuwa ni hatari kwa maisha ya wanadamu.

Alisema tatizo lililopo baadhi ya Watanzania wameufanya ugonjwa huo kama mdori wakati unaonekana una madhara makubwa ya kupoteza maisha ya watu, hivyo ni wakati sasa wakaondokana na dhana hiyo badala yake washirikiane na serikali katika mapambano.



## Waendesha bodaboda walia kukosa wateja

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAFANYABIASHARA wa Bodaboda Zanzibar wamesema ugonjwa wa corona umesababisha biashara hiyo kuwa ngumu kwa kukosa wateja.

Wakizungumza na Nipashe katika maeneo tofauti mjini hapa, walisema kuwa wateja wao zaidi ni wafanyakazi wa hoteli za kitalii na hatua ya kufungwa kwa hoteli hizo kutokana na corona wamekosa wateja wao.

"Wateja wetu zaidi ni wafanyakazi wa hoteli, baa na wanaokwenda katika kumbi za starehe, lakini hivi sasa biashara hizo zimefungwa kutokana na corona na hali zetu za kiuchumi zimekua ngumu," alisema.

Alisema kabla ya ugonjwa huo, kwa siku alikua akipata Sh. 50,000, lakini hivi sasa hata nusu ya kiwango hicho hakipati kutokana na kukosa wateja.

Mfanyabiashara Faki Ali, aliomba ugonjwa huo uondoke kwa sababu kazi yake hiyo ndiyo inayomsaidia kuendesha familia yake kwa mahitaji mbalimbali ikiwamo kununua chakula.

Alisema hivi sasa njaa kali, fedha haipatikani kutokana na ugonjwa huo hivi sasa wateja hakuna watu wapo majumbani mwao.

"Tupo hapa stendi tunapiga stori tu wateja hamna...watu wanaogopa corona, Mungu atuondoshee balaa hili maana tutakufa njaa," alisema.

Hali ngumu ya biashara haipo kwa wafanyabiashara wa boda boda pekee, madereva taksi wanalalamikia ugumu wa biashara kutokana na corona hali ambayo imesababisha wateja kukosekana.

Said Mohamed, ni dereva taksi alieleza kuwa wateja wao zaidi ni wageni, lakini kutokana na hoteli za kitalii kufungwa hali ya biashara imekuwa ngumu.

Alisema kuwa kabla ya ugonjwa wa corona kwa siku alikuwa akipata Sh. 70,000, lakini kwa sasa anapata Sh. 20,000.

Aliwataka madereva wenzake kuchukua tahadhari kubwa kuhusu ugonjwa huo na kuhakikisha katika gari wanakuwa na dawa za kuosha mikono ili mteja kabla ya kuingia katika gari kusafisha mikono yake kwa kitakasa mikono.

# Madaktari 27 wawekwa karantini

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

IDADI ya wananchi waliowekwa karantini Zanzibar imeongezeka na kufikia 324 wakiwamo madaktari 27 kwa ajili ya kufanyiwa uchunguzi wa maambukizi ya virusi vya corona.

Akizungumza na waandishi wa habari, Waziri wa Afya Zanzibar, Hamad Rashid Mohammed, alisema watu 65 wanasubiri majibu na vipimo vyao vimepelekwa Dar es Salaam ili kujua kama wanamaambukizi ya virusi hivyo.

Alisema Zanzibar ina wagonjwa watano wa corona ambao wanaendelea kupatiwa matibabu katika kituo maalumu kilichotengwa huko Kidimni, Wilaya ya Kati Unguja na hali zao zinaendelea vizuri. Alisema, serikali kwa sasa imechukua uamuzi wa kuzifungia baa zote na kumbi za starehe Unguja na Pemba ili kuepusha athari zaidi zisiendelee kutokea.

Waziri Hamad, aliwataka wananchi kufahamu kuwa dawa ya maradhi hayo na chanjo bado haijapatikana hivyo ni vyema kufuata maelekezo yanayotolewa na serikali ikiwamo kukaa nyumbani na kujiepusha na mikusanyiko ambayo ndiyo kichocheo kikubwa cha kuambukizwa.

"Serikali imetoa maagizo ambayo bado utekelezaji wake haujakua mzuri ikiwamo wananchi kuacha kufanya masoko kuwa sehemu ya mazungumzo, kwenda mazikoni, kufanya harusi kama kawaida jambo ambalo ni kwenda kinyume na maagizo ya serikali," alisema.

Pia aliwataka baadhi ya wanaume wenye wake wawili Mombasa - Kenya na Zanzibar, kubaki huko huko nchini Kenya ili kudhibiti maambukizi ya corona.

Alisema wapo baadhi ya wanaume kisiwani Pemba wana wake wawili, mmoja Pemba na mwingine yupo Mombasa - Kenya, hivi sasa wanakimbilia Pemba baada ya kuona hali mbaya ya ugonjwa huo.

Waziri alisema wananchi 710 wamekamatwa kisiwani Pemba wakitokea Mombasa kwa kupita bandari bubu.

Aliwataka wananchi kuepuka mikusanyiko na kuacha tabia ya kwenda kunywa kahawa katika baraza za kahawa.

"Huu si wakati wa kunywa kahawa katika baraza za kahawa, kama unahitaji kahawa pika nyumbani kwako," alisema.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja, Dk. Jamal Adam Kasim, aliiomba vyombo vya habari kuendelea kuelimisha jamii juu ya kujikinga na virusi vya corona ili kuzuia maambukizi nchini.



Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, Hassan Khatib (katikati), akitoa maelezo kwa mfanyabiashara wakati alipofika eneo la Mlandege jana, kukagua uwekaji wa maji na sabuni kwa ajili ya kuosha mikono ili kujikinga na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona katika sehemu za biashara. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wafanyabiashara wakumbushwa vifaa muhimu sokoni

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa mjini Magharibi, Hassan Khatib Hassan, amewataka viongozi wa taasisi zinazotoa huduma na wafanyabiashara katika mkoa huo kuweka huduma maalumu za kunawa mikono na kutumia vitakasa mikono ili kujinusuru na maambukizi ya virusi vya corona.

Akizungumza katika ziara maalumu katika maeneo ya Darajani, Mchangani, Mlandege na Soko la Mwanakwerekwe, Wilaya ya Mjini Unguja, alisema serikali ikiendelea na jitihada za kupambana na maambukizi ya maradhi hayo ni lazima wananchi wakachukua tahadhari ili kujikinga.

Alisema iwapo kila mwanachi atatekeleza wajibu wake kikamilifu, kuna uwezekano mkubwa wa kuzuia kasi ya maambukizo ya ugonjwa huo ambao umeikumba dunia.

"Serikali inapotoa maelekezo yanapaswa kutekelezwa, na kufata elimu na matangazo ya wataalamu wetu wa afya. Hivyo tusiwe wakaidi kwenye mambo haya ya tahadhari masuala ya kuzingatia," alisema Hassan.

Aliwapongeza wafanyabiashara wa maduka ya vifaa vya ujenzi ya maeneo ya Mlandege kwa kuchukua tahadhari ya kuweka dawa na maji ya kusafisha mikono katika maeneo yao ya biashara.

Alitoa elimu ya madhara ya maradhi hayo kwa jamii na kuwataka wananchi kuepuka mikusanyiko huku akiwaagiza viongozi wa soko la Mwanakwerekwe kuendelea kusimamia agizo la kuwataka wafanyabiashara wa soko hilo kufunga biashara zao saa 11 jioni.

Aliwataka wafanyabiashara kuacha kuweka bidhaa zao chini na badala yake kutumia maeneo maalumu yaliyotengwa ili kulinda afya za mlaji na kudumisha usafi.

Kwa upande wao wafanyabiashara wameiomba serikali kuwachukulia hatua za kisheria wafanyabiashara wenzao wanaopandisha bei za bidhaa kwa kisingizio cha corona.

# Wenye ualbino kupunguza changamoto

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

BAADHI ya wanafunzi wenye ualbino wanaofadhiliwa masomo na Taasisi ya The Foundation of Josephat Torner Europe Aid (Fojotea), inayotetea haki za watu walioko pembezoni, wamedhamiria kupunguza changamoto zinazowakabili wenzao.

Waliyasema hayo jijini hapa jana walipozungumza kwa nyakati tofauti na gazeti hili kuhusu mustakabali wao baada ya kuhitimu masomo yao na kuishukuru Fojotea kwa kuwafadhili ili watimize ndoto na malengo yao.

Walisema masomo wanayosoma yamejikita katika falsafa ya uongozi wa jamii, hivyo itakuwa muda muafaka wao kushirikiana na serikali na taasisi zingine binafsi kutokomeza unyanyapaa ambao umekithiri miongozi mwao.

Enock Kusekwa, mwanafunzi wa kidato cha tano katika Shule ya Sekondari ya Longido, mkoani Arusha, alisema anatarajia kusomea sheria ili aweze kuwasaidia watu wenye mahitaji maalumu wakiwamo wenye ualbino ambao wanaporwa haki zao za msingi.

"Watoto wengi wenye ulemavu wakiwamo wenye ualbino wamekosa haki ya kuishi na kupata matunzo kutoka kwa wazazi wao hasa baba kwa sababu tu wamezaliwa na hali hiyo, hivyo wamewakataa wao pamoja na mama zao hata mimi ni muhanga wa hilo," alisema.

"Mimi nimepitia manyanyaso mengi sana kutoka kwa wanajamii na baadhi ya ndugu zangu, tukio ambalo sitalisahau maishani ni siku niliyopewa chakula na bibi yangu wa kambo kilichokuwa kimepikwa kwa ajili ya mbwa nikaambiwa nile kwa sababu sina tofauti na mnyama huyo," alisema Kusekwa.

Pius Boniphace na Yohana Bahame, walisema ndoto zao ni kuwasaidia wengine wenye ulemavu hata kwa mawazo ili waweze kutimiza malengo yao, wakipata nafasi ya kufanyakazi katika ngazi za uamuzi watafurahi zaidi kwa sababu watashiriki kikamilifu kulinda haki na maslahi ya kundi hilo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Fojotea, Josephat Torner, alisema hadi sasa wamekwisha wafadhili masomo wanafunzi 14 kuanzia ngazi ya msingi, sekondari na vyuo vikuu kwa sababu wanaamini mtoto akiwezeshwa kupata elimu bora kinatengenezwa kizazi chenye weledi na uadilifu.

# Wadaiwa sugu kodi ya ardhi matatani

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WIZARA ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, imeanza kutoa elimu kwa wadaiwa sugu wa kodi za ardhi, ili walipe kodi hiyo kwa wakati.

Kodi hiyo inapaswa kulipwa kabla ya kufika Juni mwaka huu, na ambao hawatalipa watachukuliwa hatua kali za kisheria.

Hayo yalibainishwa jana na mkuu wa kitengo cha kodi wa wizara hiyo, Denis Masami, alipofuatana na Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, kutoa elimu kwa wadaiwa sugu wa kodi ya ardhi.

Alisema wizara kabla ya kuanza kuwachukulia hatua wadaiwa sugu wa kodi ya ardhi, wameona ni vyema kuanza kutoa elimu hiyo kwanza ya kulipa kodi kwa hiari, na baada ya hapo watakao kaidi lazima wa wajibishe.

"Wizara tumeanza kutoa elimu ya ulipaji kodi kwa wananchi na wamiliki wa viwanda, ili walipe kodi kwa hiari kabla ya Juni ambao ni mwaka wa fedha, na baada ya hapo tutawachukulia hatua kali za kisheria," alisema Masami.

"Hapa Shinyanga tumetembelea wadaiwa wakubwa wa kodi ya ardhi katika kiwanda cha Wachina cha uchakataji wa nyama ya punda, ambapo wanadaiwa Sh. milioni 63 malimbikizo ya kodi miaka saba tangu mwaka 2013-2020 pamoja na Kampuni ya Ghaki inadaiwa Sh. milioni 120," aliongeza.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Mboneko ,aliwataka wawekezaji na wananchi kufuata sheria za nchi za ulipaji kodi, na siyo kusubili hadi kuanze mvutano na Serikali, kwa kuwa kodi hizo ndio kichocheo kikubwa cha maendeleo ya nchi.

Kwa upande wake Meneja wa kiwanda cha uchakataji wa nyuma ya punda Mjini Shinyanga, Alice Mingyang, alisema hawakujua kama kuna kodi hiyo bali kodi ya nyumba, huku wakiahidi kuilipa kodi hiyo.

Mkurugenzi wa kampuni ya Ghaki Investment, Gaspal Kileo, alisema malimbikizo ya kodi ya ardhi yalitokana na mgogoro, lakini ameshalipa Sh. milioni 10, huku akiahidi kuendelea kulipa madeni yote.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo (katikati), akitoa maelekezo kwa viongozi wa Mkoa wa Dodoma, alipotembelea kukagua ujenzi wa Hospitali ya Uhuru inayojengwa Wilaya ya Chamwino jana. Wa (pili kushoto) ni Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tisa kutoka Sadc wawekwa karantini

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

SERIKALI mkoani Mbeya imesema watu tisa kutoka nchi kadhaa za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (Sadc), wamewekwa karantini katika baadhi ya hoteli za pembezoni mwa mji kwa muda wa siku 14.

Hatua hiyo ni sehemu ya kukabiliana na kusambaa kwa virusi vya ugonjwa wa corona.

Akizungumza na wanahabari jana jijini Mbeya, Mkuu wa Mkoa huo, Albert Chalamila, alisema pamoja na watu hao kuhifadhiwa huko, lakini wako chini ya ulinzi na wanahudumiwa na wahudumu, ambao wamepata mafunzo maalum.

Alisema mkoa huo una kamati maalum ya kupambana na maradhi hayo, na kwamba Kamati hiyo inafanya kazi hasa maeneo ya mipakani.

"Tumewaweka karantini zaidi ya watu tisa kutoka mataifa mbalimbali ambao waliingia nchini sasa kwa kuchukua tahadhari dhidi ya corona... tumeamua kuwaweka kwenye hoteli zilizoko pembezoni mwa Jiji la Mbeya na watajihudumia kwa gharama zao," alisema Chalamila.

Aliwatahadharisha wananchi kuachana na imani potofu zinadai pombe kali zinaweza kuzuia maambukizi ya virusi vya corona badala yake wazingatie ushauri unaotolewa na wataalam wa afya.

Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya, James Kasusura, aliagiza magari yote ya abiria pamoja na pikipiki za magurudumu matatu, maarufu kama bajaji kupuliziwa dawa maalum za kuua virusi kabla ya kutumiwa na wananchi.

Katika hatua nyingine, Chalamila alisema zaidi ya Sh. milioni 150 zimetaifishwa kutoka kwa raia wa nchi jirani ambao waliokuwa wakijaribu kuingia nchini kwa njia za panya.

Alisema fedha hizo zitatumika kwenye shughuli mbalimbali za maendeleo ukiwamo ujenzi wa vyumba vya madarasa na madawati. Chalamila aliongeza kuwa wakuu wote wa mikoa ya Nyanda za juu Kusini wakubaliana kuilinda mipaka ya nchi zinazowazunguka, huku wakiweka ulinzi kuzuia watu kuingia kinyemela nchini.

## HABARI KIMATAIFA

# Ulaji wa mbwa, paka wapigwa marufuku China

**BEIJING,** China

MJI wa Shenzhen umekuwa wa kwanza China kupiga marufuku ulaji wa kitoweo cha nyama za mbwa na paka.

Hii inakuja baada ya mlipuko wa virusi vya ugonjwa wa corona kuhusishwa na ulaji wa wanyamapori, jambo lililowafanya maofisa wa China kupiga marufuku biashara na ulaji wa wanyama hao.

Mamlaka za mji huo zimeeleza kuwa Sheria za ukatazaji wa wanyama hao itaanza kutekelezwa kuanzia Mei, 1. Taarifa iliyotolewa na Shirika la kutetea haki za wanyama, Humane Society International (HSI), ilieleza kuwa Mbwa milioni 30 huuawa kote katika bara la Asia kwa ajili ya nyama,

Hata hivyo, ulaji wa nyama ya mbwa nchini China si wa kawaida sana-wengi wa Wachina hawajawahi kufanya hivyo na wanasema hawataki kufanya hivyo.

"Mbwa na Paka kama wanyama wa nyumbani wameweza kuwa na uhusiano wa karibu sana na binadamu kuliko wanyama wengine wote, na kupiga marufuku ulaji wa nyama za mbwa na paka na wanyama wengine wa nyumbani ni jambo la kawaida katika mataifa yaliyoendelea na kama miji ya Hong Kong na Taiwan," ilisema serikali ya Jiji la Shenzhen na kuongeza:

"Marufuku hii pia inaitaka mahitaji na moyo wa kistaarabu wa ubinadamu.Haya kusema ukweli ni mafanikio makubwa katika juhudi za kumaliza ukatili huu ambao unakadiriwa kuwauwa Mbwa milioni 10 na Paka milioni nne nchini China kila mwaka," alisema Dk. Peter Li, mtaalamu wa sera katika kampuni ya China ya HSI.

**Hata hivyo, hukumu hiyo iliyotolewa China imeidhinisha matumizi ya nyongo ya dubu katika kuwatibu wagonjwa wa virusi vya corona.**

Hata hivyo, hukumu hiyo iliyotolewa China imeidhinisha matumizi ya nyongo ya dubu katika kuwatibu wagonjwa wa virusi vya corona.

Nyongo ya dubu - ambayo ni kiminika kinachosaidia kusaga chakula huchukuliwa kutoka kwa dubu ambao ni hai - imekua ikitumika kwa muda mrefu nchini China kama dawa ya kienyeji.

Nyongo hiyo ambayo ina tindikali ya ursodeoxycholic , hutumiwa kuyeyusha mawe yanayojitengeneza katika kibofu cha mkojo na kutibu ugonjwa wa maini . Lakini hakuna uthibitisho kuwa ina ufanisi dhidi ugonjwa wa virusi vya corona na mchakato wa kuitoa huwasababishia machungu sana wanyama hao.

Msemaji wa wakfu wa Animals Asia Foundation, Brian Daly, aliliambia shirika la habari la AFP kuwa: "Hatupaswi kuwa tunategemea bidhaa za wanyama kama nyongo ya dubu kama suluhu ya kukabiliana na virusi vinavyoua ambavyo vinaonekana kuwa asili yake ni wanyamapori."

Kwa sasa kuna wagonjwa milioni moja walioothibitishwa kuwa na virusi vya corona kote duniani, na zaidi ya vifo 47,000, kwa mujibu wa hesabu za Chuo kikuu cha Johns Hopkins cha Marekani.Nchini China pekee, kuna wagonjwa 81,589 na vifo 3,318.

Wanasayansi na watafiti bado hawajaweza kutambua chanzo hasa cha mlipuko huo wa virusi na kwa namna gani viliwafikia wanadamu. Februari, China ilipiga marufuku biashara na ulaji wa wanyama pori. **BBC**



Ofisa wa afya nchini Uganda akimpima mmoja wa wananchi ili kubaini kama ana maambukizi ya ugonjwa wa virusi vya corona. **PICHA: REUTERS**

# Watumia nyongo ya dubu kutibu wagonjwa wa corona

**BEIJING,** China

CHINA imeidhinisha matumizi ya nyongo ya dubu kutibu wagonjwa wa virusi vya corona hatua iliyowakasirisha wanaharakati na kuibua wasiwasi kwamba huenda ikazorotesha juhudi za kuzuia biashara haramu ya wanyama.

Hatua hiyo inakuja ikiwa zimepita wiki chache tu baada ya China kupiga marufuku biashara ya wanyama wa porini kwa ajili ya kitoweo ikiangazia hatari ya kusambaa kwa magonjwa kutoka kwa wanyama kwenda kwa binaadamu.

Hata hivyo, Tume ya kitaifa ya afya mnamo Machi, mwaka huu ilitoa miongozo inayotaja matumizi ya sindano ya "Tan Re Qing" ambayo huwa na mchanganyiko wa poda ya nyongo ya dubu, pembe ya mbuzi na dawa nyingine za mitishamba katika kuwatibu wagonjwa wenye virusi vya corona ambao wako katika hali mbaya.

Rais wa China, Xi Jinping amekuwa akihamasisha dawa za asili akiziita "hazina za ustaarabu wa China" na kusema zinatakiwa kupewa uzito sawa na tiba nyingine. **DW**

## Ugonjwa wa corona wasababisha vita kusimama

**TRIPOLI,** Libya

WAKATI ulimwengu ukikabiliwa na janga la ugonjwa wa virusi vya corona, Libya kesho inaadhimisha mwaka moja tangu kuzuka kwa mapigano kati ya serikali inayotambuliwa kimataifa jijini Tripoli na vikosi vya upinzani vinavyoongozwa na Marshal Khalifa Haftari anayedhibiti maeneo ya Mashariki mwa nchi hiyo.

Aidha, vita hivyo vilichukua mkondo mpya kufuatia uungaji mkono wa dola ya kigeni kwa pande mbili zinazozozana katika nchi hiyo ya Kaskazini mwa Afrika.

Pamoja na hayo, kusambaa kwa virusi vya corona kulisababisha kujitokeza matukio muhimu katika uwanja huo. Udharura wa kukabiliana na ugonjwa wa virusi vya corona unaotishia pande zote hasimu nchini Libya ni jambo lililomfanya Khalifa Haftar na Serikali ya umoja wa kitaifa ziridhie kusitisha vita.

Hadi sasa kumefanyika juhudi mbalimbali za kimataifa kwa lengo la kuhitimisha vita vya ndani nchini Libya. Moja ya juhudi hizo ni mkutano wa Januari 13 mwaka huu wa wawakilishi wa Uturuki, Urusi na pande hasimu nchini Libya uliofanyika mjini Moscow na kumalizika bila ya tija, ambapo Khalifa Haftar aliondoka katika mji huo bila kusaini hati ya makubaliano.

Wataalamu wa afya wameeleza kuwa Libya ipo kwenye hatari ya kusambaa kwa ugonjwa wa virusi vya corona baada ya miundombinu kwenye sekta ya afya nchini humo kuharibika kutokana na mapigano hayo. **RFI**

## Walioambukizwa corona Hispania wafikia 100,000

**MADRID,** Hispania

NCHI ya Hispania imethibitisha kuwa idadi ya walioambukizwa virusi vya ugonjwa wa corona imefikia 100,000, wakati maofisa wa Wamarekani wamewataka wananchi wajiandae kuwapo kwa uwezekano wa vifo kati ya 100,000 hadi 240,000 vinavyotokana na virusi hivyo.

Hispania ni moja ya nchi zilizo na maambukizi ya virusi hivyo, ikiwa nyuma ya Marekani na Italia kwa idadi ya maambukizi.

Tangazo lililotolewa juzi, lilitoa idadi ya vifo nchini Hispania imefikia 9,000. Takwimu zilizotolewa na Shirika la Afya Duniani (WHO) mwishoni mwa wiki zilieleza kuwa idadi ya maambukizi ya virusi vya corona duniani imefikia 870,000, vifo zaidi ya 43,000, na watu zaidi ya 184,000 wamepona baada ya maambukizi hayo.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa katika bara la afrika, zaidi ya maambukizi 5,000 yameripotiwa katika bara hilo pamoja na vifo 190. **VOA**

# Mpaka wa Namanga sasa wadaiwa kukosa udhibiti

**Na Asraji Mvungi,** NAMANGA

WATENDAJI na wataalamu wa afya katika kituo cha Forodha cha Namanga wameeleza changamoto zinazojitokeza katika udhibiti wa kuenea kwa virusi vya corona ikiwamo ya uhaba wa vifaa vya kujikinga wakati wa kutoa huduma, na tofauti ya sheria na maelekezo ya viongozi wa nchi za Tanzania na Kenya.

Watendaji hao walitoa changamoto hizo kwa wabunge wa Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki waliotembelea kituo hicho kujionea hatua zinazoendelea kuchukuliwa kukabiliana na tatizo la corona.

Kuhusu tatizo la uhaba wa vifaa vya kujikinga, watendaji hao akiwamo mtaalamu wa afya katika kituo teule cha afya cha Oriendeke, kilichotengwa kwa ajili ya huduma kwa watu wanaohisiwa kuwa na dalili za virusi hivyo, amesema licha ya kuwa hawajapata watu wenye matatizo hayo, wana uhaba mkubwa wa vifaa vya kuwawezesha kujikinga, suala linaloweza kuwaathiri kama atatokea mgonjwa.

Tatizo hilo pia limezungumziwa na Ofisa afya mfawidhi wa Kituo cha Forodha cha Namanga, Dk. Gabriel Mdachi, ambaye alisema pamoja na utayari walinao wa kukabiliana na tatizo hilo vifaa vya wao kujikinga bado ni changamoto.

"Tumejipanga vizuri na mpaka sasa tunashukuru kuwa hatujapata watu wenye matatizo, lakini kwa upande wa watendakazi kuna changamoto ya uhaba wa vifaa vya kujikinga kama wagonjwa watatokea," alisema Dk. Mdachi.

Akizungumza na wabunge hao, Katibu Tawala wa Wilaya ya Longido, Toba Nguvila, alisema utaratibu na maelekezo ya serikali ya Kenya wa kuwataka wananchi kufunga shughuli zao ifikapo saa moja za jioni umeongeza changamoto ya wananchi hao kuingia Tanzania tena kwa kutumia njia zisizo rasmi.

"Wananchi wetu huku mpakani wanashirikiana sana, upande mmoja wamewekewa sheria ya kufunga shughuli zote saa moja jioni, wakati huku kwetu tunafunga saa tano usiku, sasa unakuta kule wakifunga, wote wanakuja huku usiku huo na wengi watakuwa wanapitia njia zisizo rasmi, kwa kweli hili ni tatizo," alisema Nguvila.

Aliwaomba wabunge hao kutumia nafasi zao kuzishawishi nchi wanachama kuweka utaratibu wa pamoja wa kuendelea kuchukua tahadhari na pia kuendelea na majukumu yao bila kuongeza matatizo.

Vile vile alisema wanaoishi maeneo ya mpakani wameanza kuelewa na kufuata maelekezo na ushauri unaoendelea kutolewa kwa kukabiliana na ugonjwa huo ikiwa ni pamoja na kuepusha mikusanyiko na pia safari za zisizo za lazima.

Mwakilishi wa wabunge hao, Fancy Nkuy, alisema atafikisha kwenye ngazi zinazohusika na hatua zitachukuliwa.

Nkuy alisema katika hatua za kukabiliana na changamoto zinazojitokeza, wameshazungumza na baadhi ya wadau wakiwamo watendaji wa taasisi ya sekta binafsi ambao wameonyesha nia ya kusaidia upatikanaji wa vifaa vya kujikinga kwa ajili ya watoa huduma.

"Hili tatizo la uhaba wa vifaa sisi kama wabunge wa EALA tumelisikia na tumeanza kushirikiana na wadau wengine kulitafutia ufumbuzi na kwa kuanzia tumeongea na watendaji wa taasisi binafsi na wameonyesha nia ya kutusaidia, na pindi watakapotimiza ahadi kipaumbele kitakuwa maeneo haya ya mpakani," alisema.

Baadhi ya watu waliozungumzia tatizo hilo wamekiri kuvuka mpaka na kuingia upande wa Tanzania kwa kujipatia mahitaji baada ya huduma hizo kusitishwa upande wa pili wa Kenya na kwamba wakati mwingine wanalazimika kulala upande wa Tanzania.

Kuhusu athari za kibiashara zinazochangiwa na tatizo hilo, Mkuu wa Mamalaka ya Mapato (TRA) katika kituo cha Namanga, Paul Kamkulu, alisema pamoja na changamoto hiyo kupunguza idadi ya watu wanaoingia na kutoka nchi moja na nyingine, biashara hasa ya usafirishaji wa mizigo inaendelea.



Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella (wa pili kushoto), akiwa na baadhi ya viongozi wa mkoa huo, wakipata chakula cha mchana kwa mamalishe katika soko la Mirogo jijini humo, juzi, walipokuwa kwenye ziara ya kujionea utayari wa taasisi mbalimbali kupambana na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona. **PICHA: NEEMA EMMANUEL**

## Watatu wahofiwa kufa maji mto Mara

**Na Ambrose Wantaigwa, SERENGETI**

WATU watatu wanahofiwa kufa maji baada ya boti waliyokuwa wakitumia kuvuka mto Mara katika Wilaya ya Serengeti kuzama huku wengine wanne wakijeruhiwa.

Kikosi maalumu cha uokoaji cha Jeshi la Polisi Mkoa wa Mara kinaendelea na juhudi za kusaka miili hiyo ambayo pia inasadikiwa kuwa ilikuwa ya wanawake na ilipotea kwa kusombwa na maji kutokana na mto huo kujaa baada ya mvua kubwa inayoendelea kunyesha ukanda huo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mara, ACP Daniel Shillah, anayeongoza operesheni ya uokoaji katika eneo la tukio, alisema tayari jeshi hilo linawashikilia watu wawili kwa mahojiano.

Alisema wakati wa ajali hiyo jitihada za wananchi kuokoa waathirika hao hazikufua dafu kutokana na kukosekana vifaa na kushindwa kuhimili mwendo kasi wa maji katika mto huo uliofurika.

Aliwataja waathirika hao kuwa ni Nyigai Mahende (25), Matinde Ryoba (15) na Elizabeth Nyambaha (19), wote wakazi wa kijiji cha Borenga, wilayani Serengeti.

Kamanda Shillah alisema ajali hiyo ilitokea wakati watu hao wakiwa miongoni mwa wasafiri wengine waliokuwa wakijaribu kuvuka mto huo kuelekea upande wa Nyamongo na boti waliyokuwa wakisafiri hayo kuzama.

Shillah alisema watu wawili walioshikiliwa wanahusishwa na chanzo cha ajali hiyo kutokana na madai ya kutumia chombo kisicho salama na kujaza watu zaidi ya uwezo, uchunguzi ukikamilika watafikishwa mahakamani.

Kamanda Shillah alitahadharisha wamiliki wanaotumia vyombo visivyo na ubora kusafirisha abiria wakati huu mito imejaa hatua kali zitachukuliwa kwa watakaobainika.

## Tishio la corona lilivyoporomosha bei nyanya Ilula

**Na Francis Godwin,** IRINGA

JANGA la maambukizi ya corona limeendelea kuathiri biashara kadhaa nchini, huku wafanyabiashara wa nyanya mjini Ilula wilayani ya Kilolo mkoani Iringa wakilalamikia hali hiyo.

Wakizungumza jana wakati wa ziara ya Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Kilolo, Yohanes Sarufu, katika soko la nyanya la Tasaf mjini Ilula, walisema awali bei ya nyanya ilikuwa juu kutokana na wageni kutoka Kenya kuja kununua bidhaa hiyo.

Lakini walidai kutokana na hofu ya corona duniani, hivi sasa wafanyabiashara wa nyanya kutoka Kenya na maeneo mengine nje ya Tanzania hawafiki kununua, hivyo kulazimika kuuza kwa hasara.

Wafanyabiashara hao Filix Msola na Chedy Kilongamtwa walisema soko la a nyanya kwa sasa limeyumba sana kutoka bei ya tenga shilingi 75,000 hadi 80,000, sasa wanauza kati ya shilingi 25,000 hadi 30,000 kwa tenga la ujazo wa debe tatu.

"Kabla ya ugonjwa wa corona haujatangazwa kuingia Afrika, tulikuwa tukipata wageni kutoka nchi mbalimbalo ikiwamo Kenya, Ila sasa mipaka imefungwa na wafanyabiashara kutoka nje hawaji tena," alisema Msola.

Alisema wateja wanaowategemea ni kutoka Dodoma, Dar es Salaam na ndani ya mkoa wa Iringa, ambao wengi wao wanapenda bei ya chini zaidi.

Alieleza kuwa hasara wanayoipata ni kubwa kutokana na kutumia gharama kubwa kuwekeza kwenye kilimo lwa matarajio ya kupata fedha zaidi baadae.

Alisema wao wakulima wa nyanya wanatambua mchango mkubwa wa serikali katika kupambana na corona, hivyo wanaamini tatizo hilo ni la mpito na wanaweza kupata pesa zaidi kwa siku za usoni kama ugonjwa utakwisha.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi wa CCM Wilaya ya Kilolo, Yohanes Sarufu, aliwataka wafanyabiashara wa nyanya Ilula kutumia umoja wao kuuza nyanya kwa bei nzuri watakayojipangia badala ya kuwatumia madalali.

Alisema licha ya ugonjwa huo, watajipanga kuuza nyanya kwa pamoja kwa bei nzuri, lakini kila mmoja aliuza kwa bei yake, wataishia kulaliwa bei.

Sarufu alisema lengo la serikali kuwajengea soko la nyanya ni kutaka wote wauzie ndani ya soko ili kuuza kwa bei nzuri.

# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## ELIMU/ MASOMO

**REGISTRATION OPPORTUNITIES KELAND NURSERY AND PRIMARY SCHOOL** located at salasala announces registration opportunities for Nursery and Primary School students. Call: 0713 327613.

## NYUMBA/VIWANJA

**NYUMBA INAUZWA,** Ninauza nyumba ya vyumba vinne vya kulala, kimoja ni master self contained. Ina vyumba vitano vya nyuma kimoja ni self contained, choo, bafu na jiko. Nyumba iko Ntyuka Dodoma karibu na shule ya sekondari Ntyuka. Nyumba iko kwenye kiwanja cha ukubwa wa SQM 2590. Ni nyumba nzuri sana kwa makazi na kupangisha. Kwa maelezo zaidi piga simu no. 0699-210258


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu:


## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MATHIAS MICHAEL MTUI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba ya usajiri **T 400 CD 113 TOYOTA CRUISER.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa Kituo Cha Polisi.

Taarifa ya Polisi

**ARU/ARU/RB/279714/2020.**

215688302

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**EMMANUEL JOSEPH MOSHY** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 557 BRT.** Chassis namba **MD2A21BYXHWA 91467. Engine PFZWHA 82841.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:

**DAR/URA/RB/286059/2020.**

215688502

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BADRUDDIN HABIB HALARI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 742 AGG TOYOTA LANDCRUISER, rangi ya GREY. Chassis namba 7009002184.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**Taarifa ya polisi:**

**DAR/BUG/RB/286472/2020.**

156892


***Uza, Chenye Thamani Kubwa***

***Kwa Kutangaza Nasi Kwa***

***Bei Poa Tupigie***

***0782253676***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe

www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII


**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**

**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# ZLATAN HAJUI HATIMA YAKE MILAN




**MILAN,** Italia

ZLATAN Ibrahimovic amedai hajui majaliwa yake ya baadaye yako wapi baada ya ripoti kubainisha kwamba yupo tayari kuondoka AC Milan ikiwa ni miezi mitatu tu tangu arudi klabuni hapo.

Mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Sweden ameripotiwa kuwa 'amekatishwa tamaa' na uongozi wa klabu hiyo baada ya kumfukuzwa ofisa wa soka, Zvonimir Boban.


Boban ndiye aliyehusika kwenye mpango wa kumleta Ibrahimovic pale Milan, ambapo awali alicheza kati ya mwaka 2010 na 2012, na kulikuwa na matarajio kwamba timu hiyo itajengwa kuwa ya ushindani zaidi msimu ujao pamoja na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 38.

Lakini sasa majaliwa ya Ibrahimovic yapo shakani na kuna uwezekano akaamua kuondoka hapo kwenye dimba la San Siro.

Hata hivyo, fowadi huyo wa zamani wa Manchester United bado hajui chochote kuhusu majaliwa yake, alibainisha kwamba hata hajui wapi atakwenda.

"Tutaona nini kitatokea. Hata sijui wapi natakiwa kwenda, kitu kipya kinatokea kila simu," amesema Ibrahimovic akiliambia gazeti la Svenska Dagbladet."

# Arteta anafuta kiungo Arsenal




**LONDON,** England

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta amesema mpango wake namba moja kwenye dirisha lijalo la usajili wa majira ya joto ni kusajili kiungo wa kati.

Arsenal imepania kuwa na nguvu mpya msimu ujao, Arteta anahitaji kutengeneza timu ambayo itakuwa na uwezo wa kushindania mataji makubwa kama ilivyokuwa miaka ya nyuma.

Wachezaji kadhaa mastaa kwenye safu ya ushambuliaji ikiwamo wakali wa Real Madrid, Luka Jovic na James Rodriguez wanahusishwa na mpango wa kutua kwenye kikosi hicho chenye maskani yake huko Emirates katika dirisha lijalo la uhamisho wa majira ya kiangazi.

Hata hivyo, kwa mujibu wa gazeti la The Sun, miamba hiyo ya London dhamira yao kubwa kwenye dirisha lijalo ni kusajili kiungo wa kati, hasa kwenye eneo la kukaba ili kuimarisha kwenye sehemu ya ulinzi ya timu yake.

Arteta pia amepanga kusajili mchezaji ambaye atakuja kumfanya Mesut Ozil acheze kwa uhuru na kuonyesha yale makali yake ya kupiga pasi za mabao.

Kiungo wa Newcastle United, Matty Longstaff, anatajwa kwenye orodha ya wakali ambao huenda Arteta akafanya kweli kunasa saini zao kwenye kikosi chake.

# Kane anaweza kuondoka Spurs – Redknapp

**LONDON,** England

FOWADI wa Tottenham Hotspur, Harry Kane, hataweza kuendelea kubakia klabuni hapo isipokuwa kama wataanza kupigania kutwaa mataji, kwa mujibu wa kocha Harry Redknapp ambaye alimpa nafasi ya kwanza kucheza.

Kocha huyo wa zamani wa Spurs, Redknapp amesema klabu hiyo ipo kwenye hatari ya kumpoteza nyota wake huyo kwa klabu kama Manchester City kama tu hawataonyesha nia ya kutaka kuleta nyota wapya wa kuwania mataji.

Kumekuwa na mashaka juu ya uwezekano wa Kane kuendelea kubakia kwa klabu hiyo ya jijini London hasa wakati ikiwa inapigania kubakia kwenye nne bora katika msimamo wa Ligi Kuu.

Kikosi hicho kinachonolewa na kocha, Jose Mourinho kipo hatarini kukosa kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

Lakini Redknapp amesema klabu hiyo inatakiwa kuhakikisha wanambakisha Kane na kusajili nyota watakaotoa changamoto ya kuwania mataji.

"Sikiliza, Harry ni mtu kijana mwenye malengo," alisema akiiambia Sky Sports.

"Ni mchezaji kwenye kipaji cha kuvutia na anataka kucheza na kushinda vitu. Hivyo wao kama watanaka kuendelea kuwa nae wanatakiwa kuhakikisha wanakuwa kwenye nafasi ya kushinda mataji."



# United yaendelea kujipanga kwa Haaland

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United itapambana na Real Madrid siku zozote zijazo katika usajili wa mshambuliaji wa Borussia Dortmund, Erling Haaland, kwa mujibu wa Daily Mail.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Norway mwenye umri wa miaka 19 alijiunga na miamba hao wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, wakati wa dirisha la usajili la Januari akiwa mmoja wa washambuliaji hodari zaidi barani Ulaya.

Kocha United, Ole Gunnar Solskjaer, alifanya mazungumzo na Haaland kipindi cha majira ya baridi, lakini maofisa wa Old Trafford hawakuwa tayari kutoa fungu la fedha lililopo kwenye mkataba wake ili kumruhusu kuondoka.

Lakini ESPN imedai kwamba, united bado watamwania Haaland muda utakapofika wa yeye kuondoka Dortmund.

Hata hivyo, watakabiliwa na ushindani mgumu kutoka kwa Real Madrid ambao wanamfikiria Haaland kama mrithi wa muda mrefu wa Karim Benzema.

Miamba hao wa Hispania wanakabiliwa na changamoto ya kufunga mabao msimu huu na hivyo wanamwona Haaland kama ndio mbadala wa mchezaji huyo kwenye safu ya ushambuliaji.







# BALE AJIPANGA KUPIGANIA NAMBA MADRID

**MADRID,** Hispania

GARETH Bale ameripotiwa kwamba, yupo tayari kuweka pembeni tofauti zake za mahusiano na kocha wake, Zinedine Zidane ili kupigania namba ndani ya kikosi cha Real Madrid.

Zidane alibainisha wazi kwamba, yupo tayari kumwachia winga huyo wa kimataifa Wales kuondoka hapo kwenye dimba la Bernabeu kipindi cha majira ya joto na uhamisho wake kwenda Ligi Kuu China ulishindikana dakika za mwisho.

Bale bado ameendelea kuwa na wakati mgumu pale Real Madrid kwa kushindwa kupata nafasi katika kikosi cha kwanza.

Lakini sasa kwa mujibu wa gazeti la Mirror, Bale yupo tayari kumaliza tofauti zake ili aendelee kubakia kwenye klabu hiyo na kupigania nafasi yake.

Nyota huyo wa zamani wa Tottenham ambaye makataba wake wa sasa na klabu hiyo unamalizika Juni 2022, anapokea mshahara wa pauni 600,000 kwa wiki.

Inadaiwa kwamba, Bale hataki kuondoka katika klabu hiyo na anapenda kumalizia mkataba wake ndani ya Real Madrid na anafurahia maisha yake hapo.

# Barcelona kumtoa Griezmann PSG

**BARCELONA,** Hispania

KLABU ya Barcelona imeripotiwa ina matumaini ya kukamilisha usajili wa Neymar kipindi cha majira ya joto, huku Antoine Griezmann akienda upande mwingine.

Mfaransa huyo alijiunga na miamba hao kipindi cha majira ya joto akitokea Atletico Madrid kwa pauni milioni 108, lakini klabu hiyo ya Katalunya ipo tayari kumwachia aondoke ili kupata fedha ya kumsajili Neymar.

Taarifa kutoka nchini Hispania zinadai kwamba, Barcelona imewafanya Neymar na mshambuliaji wa Inter Milan, Lautaro Martinez kama kipaumbele chao cha kuwasajili kipindi cha majira ya joto.

Ousmane Dembele na Philippe Coutinho wamekuwa wakitajwa pia wanaweza kuhusika kwenye usajili huo, lakini kwa mujibu wa Sky Sports Griezmann anaweza kutolewa PSG kama sehemu ya kumpata Neymar.

Sky Sports imedai kwamba, Barcelona imeweka thamani ya Griezmann kuwa ni pauni milioni 90 na wataangalia uwezekano wa kumuuza kwa namna yoyote ile.

Griezmann hajaishi kwenye matarajio ya wengi tangu aliposajiliwa kutoka Atletico na amefunga mabao 14 katika mechi 37 katika mashindano yote.

Hata hivyo, Neymar anatajwa kuwa na thamani ya pauni milioni 135 na hiyo inamaana kwamba Barcelona watalazimika kutafuta fedha zaidi za kumsajili nyota huyo wa PSG.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MEUNIER AKARIBIA KUSAJILIWA UNITED

●●● Beki huyo Mbelgiji wa PSG pia anawindwa na Borussia Dortmund na AC Milan...

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United inajipanga kufanya mchakato wa kumsajili beki wa kulia wa Paris Saint-Germain, Thomas Meunier, ambaye hivi karibuni anatarajiwa kuwa mchezaji huru, imefahamika.

**Taarifa zilizoandikwa na gazeti la Le Quotidien du Foot la jana Alhamisi, liliandika kuwa Ole Gunnar Solskjaer amemtaja nyota huyo wa kikosi cha Timu ya Taifa ya Ubelgiji ni mchezaji sahihi anayefaa kujiunga kwenye timu yake.**

Mbelgiji huyo mwenye umri wa miaka 28, Meunier ametajwa kuwavutia vigogo wa Ujerumani, Borussia Dortmund na AC Milan ya Italia.

Inaonekana kwamba PSG itamwongezea Meunier mkataba mpya wa kuendelea kubakia katika klabu hiyo baada ya kukamilika kwa msimu wa 2019/20.

Lakini kama Meunier atajiunga na kikosi cha Solskjaer anatarajiwa kupeleka mapinduzi ndani ya Old Trafford, na atakuwa na changamoto ya kusaka namba kwenye kikosi cha kwanza.

Mmoja wa wachezaji waliosajiliwa na Solskjaer akiwa ni mchezaji wa kwanza katika majira ya joto mwaka jana alikuwa ni Aaron Wan-Bissaka ambaye aliigharimu United pauni milioni 50 kutoka kwa klabu nyingine inayoshiriki Ligi Kuu England, Crystal Palace.

Inaelezwa endapo mchakato wa Meunier kutua United utakamilika kutasaidia kukiimarisha kikosi hicho kwa kiasi kikubwa.

United ilianza kufuatilia mwenendo wa Meunier baada ya kuona beki huyo na Paris Saint-Germain kushindwa kufikia muafaka katika kusaini mkataba mpya.

Tangu Meunier alipotua PSG amecheza jumla ya mechi 25 kabla ya msimu wa 2019/20 kukumbwa na janga la virusi vya ugonjwa wa corona (COVID 19) na amefunga bao moja.

Gazeti hilo liliendelea kuandika kuwa PSG ina mpango wa kumsajili beki wa kulia wa Juventus, Mattia De Sciglio mara dirisha la usajili lijalo litakapofunguliwa.

Kiuhalisia De Sciglio anacheza nafasi ya beki wa kulia, lakini pia nyota huyo anamudu vizuri nafasi ya beki ya kushoto kwenye idara hiyo ya ulinzi.

## ZISIKUPITE

### ANCELOTTI AMTAKA RODRIGUEZ

KOCHA wa Everton, Carlo Ancelotti, anajipanga kuungana na mshambuliaji wa Real Madrid na Timu ya Taifa ya Colombia, James Rodriguez, 28. ***(Mirror)***

### MARCUS AMKARIBISHA SANCHO

MARCUS Rashford amesema atapenda kuona Jadon Sancho anasaini mkataba wa kujiunga na Manchester United katika majira ya joto kwa sababu ana kila sababu ya kuwa mchezaji wa daraja la juu. Kwa muda mrefu mshambuliaji huyo wa Borussia Dortmund amehusishwa kujiunga na United. ***(Mail)***

### BRAITHWAITE ANUKIA WEST

WEST Ham inajiandaa kuwasilisha ofa ya pauni milioni 15 kwa Barcelona ili kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Norway, Martin Braithwaite (28), ambaye amecheza mechi tatu tu tangu alipojiunga na klabu hiyo ya Nou Camp Januari mwaka huu. ***(Mail)***

### DORTMUND YAJIONDOA

BORUSSIA Dortmund imejiondoa katika mbio za kuwania saini ya kiungo Jude Bellingham (16), anayechezea klabu ya Birmingham City. ***(Bild, via Birmingham Mail)***

### POGBA AITAKA MADRID

KIUNGO wa Manchester United na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Paul Pogba (27), amesema kipaumbele chake ni kuona anajiunga na Real Madrid mara baada ya dirisha la usajili litakapofunguliwa, kwa sababu anataka kuungana na Zinedine Zidane. ***(90min.com)***

### WILLIAN AITAJA LIVERPOOL

KIUNGO wa Chelsea, Willian anafikiria Liverpool ndiyo timu ambayo iko vizuri katika Ligi Kuu England kwa sababu haijabadilisha kocha tangu 2015. ***(ESPN Brazil)***

### WILLIAN KUMFUATA SARRI

NDOTO za kiungo wa Chelsea Mbrazili Willian (31), ni kuungana na kocha wake wa zamani Maurizio Sarri katika kikosi cha Juventus mara baada ya mkataba wake na klabu hiyo ya Stamford Bridge kumalizika kwenye kipindi cha majira ya joto. ***(Tuttosport)***

### FOX ANUKIA MIDDLESBROUGH

BEKI wa kushoto wa Sheffield Wednesday, Morgan Fox (26), ametajwa kuwavutia mahasimu wao katika Ligi ya Championship, Middlesbrough. ***(Yorkshire Post)***

### MESLIER AWEKWA SOKONI

LEEDS United itampa mkataba wa kudumu golikipa Mfaransa Illan Meslier (20), kutoka Lorient ya Ligue 1 kama itafanikiwa kupata daraja na kushiriki Ligi Kuu England msimu ujao. ***(Mirror)***

### NEWCASTLE SOKONI

MIKE Ashley amesema ataiuza Newcastle United kama tajiri kutoka Saudi Arabia Amanda Staveley atakuwa tayari kuinunua klabu hiyo ya kutoa fedha taslimu. ***(Mail)***

### DE BRUYNE AFUNGUKA

KIUNGO wa Manchester City na Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Kevin De Bruyne, amesema muda alioupata wa kukaa nyumbani katika kipindi hiki cha mapambano dhidi ya virusi vya corona kumempa nafasi ya kushauriana na mkewe kuhusu hatima yake kwenye soka. ***(Mail)***

# Lusinde, Nasra wang'ara duniani

**Na Shufaa Lyimo**

CHAMA cha Mchezo wa Kabaddi Duniani kimewateua Watanzania Joseph Lusinde na Nasra Said kuwa Wachezaji Bora katika mchezo huo baada ya kuonyesha viwango vya juu katika mashindano yaliyomalizika hivi karibuni, imeelezwa.

Wachezaji hao wameteuliwa kufuatia kupata idadi ya kura nyingi walizopigiwa mara baada ya taarifa za kiufundi kutumwa katika chama hicho.

Mwenyekiti wa Chama cha Kabaddi Tanzania, Abdallah Mustapha, alisema wachezaji hao wameibuka washindi na kuteuliwa katika tuzo hizo kutokana na juhudi kubwa walizozionyesha.

"Nasra na Joseph ni wachezaji wenye uwezo mkubwa, huwa wanajituma ipasavyo na miongoni mwa wachezaji ambao wamepata tuzo nyingi kutokana na mashindano waliyocheza," alisema Abdallah.

Mwenyekiti huyo alisema mbali na nyota hao, pia viongozi wa benchi la ufundi linaloongozwa na Kocha Mkuu, Abhay Raj, Arun Dagar na Adash Sharma nao wamepongezwa kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kukinoa kikosi cha Tanzania.

Kiongozi huyo amewaomba wadau wa michezo kuwaunga mkono ili kuendelea kufanya vizuri katika mashindano mengine watakayoshiriki.

# Baluna afunguka ushindani Z'bar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KIUNGO wa Malindi FC inayoshiriki Ligi Kuu Zanzibar, Juma Baluna, amesema msimu huu umekuwa na ushindani wa hali ya juu ikilinganishwa na msimu uliopita kutokana na wachezaji kutekeleza vema majukumu yao.

Baluna (pichani) aliliambia gazeti hili jana kuwa ushindani uliopo umepelekea mbio za kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar kuwa wazi kutokana na kila timu kuonyesha ushindani.



Kiungo huyo alisema wachezaji wanajituma ili kuhakikisha wanafanya vizuri na kuzinusuru klabu zao na janga la kushuka daraja.

"Kila mchezaji anataka kuipa timu yake matokeo mazuri, hali inayopelekea wachezaji kujituma katika dakika zote za mchezo na kukaribiana viwango vya uchezaji, kwangu binafsi ninajipanga kuhakikisha ninafikia malengo ya kucheza soka la kulipwa, sitaridhika na kiwango nilichonacho sasa," alisema Baluna.

Aliongeza anahitaji kuona malengo yake yanatimia kwa kuisaidia Zanzibar kufanya vizuri katika mashindano mbalimbali kwa sababu soka ndio mchezo pekee anaoupenda.

Malindi ipo katika nafasi ya sita katika msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar yenye timu 16 ikiwa na alama 30 huku vinara KMKM wakiwa na pointi 46.

# MAYANJA AWASHANGAA KMC KUMFUNGIA 'VIOO'

**Na Faustine Feliciane**

ALIYEKUWA Kocha Mkuu wa KMC FC, Mganda Jackson Mayanja, amesema anashangazwa na kusikitishwa na kitendo cha viongozi wa klabu hiyo kukataa kupokea simu zake kwa ajili ya kujadiliana kuhusu madai ya fedha anazowadai.

**Hata hivyo, waliokuwa wasaidizi wa Mayanja, akiwamo Mlage Kabange, tayari wameshalipwa malimbikizo ya mishahara waliyokuwa wanadai.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Mayanja ambaye alitimuliwa kazi kwenye klabu hiyo amesema viongozi wa KMC ndio walivunja mkataba wake na hivyo wanatakiwa kumlipa stahiki zake kama makubaliano yanavyoeleza.

Mayanja alisema amekuwa akifanya juhudi za kumtafuta kiongozi mkuu wa klabu hiyo ambaye pia ni Meya wa Manispaa ya Kinondoni jijini Dar es Salaam, Benjamin Sitta lakini kiongozi huyo amekuwa hapokei simu.

"KMC walivunja mkataba na mimi.., nilikubaliana nao nikiamini watanilipa stahiki zangu kwa wakati, lakini napata ushirikiano mdogo kutoka kwa uongozi, kila nikipiga simu haipokelewi," alisema Mayanja na kuendelea,

"Nilitaka tumalizane na jambo ili sisi wenyewe bila kufika ngazi ya juu zaidi (Fifa), lakini sipati ushirikiano wowote tangu mkataba wangu ulipovunjwa," Mayanja alisema.

Hata hivyo Mayanja amefurahishwa na kitendo wa kulipwa kwa msaidizi wake Mlage Kabange ambaye naye alikuwa anaidai klabu hiyo.

Aliongeza kuwa anasikia furaha kuona waliokuwa wasaidizi wake wamelipwa na anatarajia kuona klabu hiyo inayafanyia kazi haraka pia madai yake.

"Mimi ndiye niliyemleta Kabange pale KMC na tukaondolewa pamoja, naye walimwangaisha sana juu ya malipo yake, lakini ameniambia tayari wamemlipa, ni jambo jema na naomba wafanye hivyo na kwangu kwa sababu nilifanya kazi yangu pale," alisema kocha huyo wa zamani wa Simba.

Nipashe ilipojaribu kuwasiliana na Sitta ili kupata ufafanuzi juu ya madai haya ambayo pia tayari yameshawasilishwa katika Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kiongozi huyo hakupatikana.

Mayanja ameweka wazi anaidai klabu hiyo inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara kiasi cha Sh. milioni 30.




Wachezaji wa Timu ya Taifa ya Soka ya Wasichana wa umri chini ya miaka 17, wakifanya mazoezi kujiandaa na mechi za kuwania tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia za Vijana (U-17). Timu hiyo inasubiri majibu ya rufani yake dhidi ya Uganda. **PICHA: MAKTABA**

# *Kipa Coastal amtangazia vita Manula*

**Na Saada Akida**

KIPA chaguo la kwanza wa Coastal Union, Sudi Abdallah, amesema anatumia vema mapumziko waliyopata ili kujiimarisha na kuendeleza mapambano dhidi ya mlinda mlango wa Simba, Aishi Manula.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam jana, Sudi alisema anaamini ataingia katika kinyang'anyiro cha kuwania tuzo ya Kipa Bora kwa msimu huu dhidi ya Manula ambaye alishinda tuzo hiyo msimu uliopita.

Sudi alisema katika michezo 27 aliyocheza, hajaruhusu nyavu zake kutingishwa katika mechi 14 rekodi inayofanana na Manula ambaye amecheza michezo 21 ya Ligi Kuu Bara.

Alisema nguvu zake anazielekeza katika mazoezi kwa muda huu ambao wako mapumziko ili kuhakikisha anafanya vizuri katika michezo 10 iliyobakia ya ligi hiyo ya juu Tanzania Bara.

"Kwa sasa jitihada zangu zote naziweka katika mazoezi kwa kuwa naamini mazoezi ndio yatanipa ubora wa kufanya vizuri, sasa najiimarisha vema kumalizia vizuri, malengo makubwa msimu huu ni kuitaka tuzo ya kipa bora," alisema Sudi.

Kipa huyo alisema pia anapambana kuhakikisha anajitolea katika timu yake kufanya vizuri katika michezo iliyobakia ili kutimiza malengo ya pamoja licha ya upinzani uliopo katika kila mechi wanayocheza.

Kipa huyo ameisaidia Coastal Union kukaa kwenye nafasi ya tano ikiwa na pointi 46 baada ya kucheza michezo 28 wakati vinara wa ligi hiyo ni Simba yenye pointi 71 na Singida United yenye alama 15 ikiburuza mkia.

Michezo
Ijumaa Aprili 3, 2020
Nipashe




Meunier akaribia kusajiliwa United UKURASA 30



Golikipa wa KMC na Timu ya Taifa (Taifa Stars), Juma Kaseja, akiwa na zawadi yake ya Sh. milioni 10 aliyokabidhiwa na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda (hayuko pichani), baada ya kuisaidia Stars kuiondoa Burundi. **PICHA: MAKTABA**

## Talib ampigia chapuo Kotei

**Na Saada Akida**

ILI iweze kujiweka katika nafasi ya kufanya vizuri katika mashindano ya kimataifa ya msimu ujao, vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, wametakiwa kuhakikisha hawafanyi makosa kwenye mchakato wa usajili wa wachezaji wa kigeni itakaowanasa, imeelezwa.

Akizungumza na Nipashe jana, aliyekuwa Kocha Mkuu wa Simba, Talib Hilal, alisema kwa sasa Simba inatakiwa kuangalia wachezaji wenye uwezo na uzoefu wa kupambana katika mashindano ya kimataifa.

Talib ambaye anaifuatilia Simba katika mechi zake zote, alitaja nafasi ambazo timu hiyo inatakiwa kuboresha ni ya ulinzi, kati na ushambuliaji. Alisema mabeki wa kati ndio ilikuwa tatizo lao kuu katika msimu uliopita ambapo mechi tatu za ugenini ilifungwa idadi ya mabao mengi.

"Ukiangalia sasa Simba sio ya kushindana au kuangalia zaidi ligi ya ndani, ukiangalia kikosi kilichopo kinaweza kufanya vizuri kwa nyumbani, kikubwa inatakiwa kuangalia zaidi michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, timu inatakiwa kusajili mabeki wawili wa kati, mshambuliaji mmoja na kiungo mkabaji," Talib alisema.

Alisema pia klabu inatakiwa kusajili straika anayejua kufunga ambaye atasaidiana vizuri na Meddie Kagere pamoja na John Bocco ambao nao wana baadhi ya upungufu ukilinganisha na nafasi wanazopata.

"Ikiwezekana nafasi ya kiungo mkabaji pia iboreshwe, asajiliwe mchezaji mwingine au ambaye ni zaidi ya Jonas Mkude au ikiwezekana wamrejeshe James Kotei ambaye msimu uliopita walitengeneza kombinesheni nzuri," alisema kocha huyo.

# Kaseja atambia kiwango chake

**Na Somoe Ng'itu**

## Afunguka silaha pekee iliyomrejesha Stars, asisitiza hakuwahi kucheka wakati timu hiyo...

GOLIKIPA mkongwe nchini, Juma Kaseja, ambaye kwa sasa anaidakia KMC FC ya jijini Dar es Salaam, amesema yeye ndiye mlinda mlango bora hapa nchini na ameweka wazi hakuwahi kufurahia kichapo cha mabao 4-0 ambacho Timu ya Taifa (Taifa Stars) ilichapwa 4-0 dhidi wenyeji Senegal kama ilivyowahi kudaiwa.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Kaseja ambaye ameiongoza Stars kufuzu fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), alisema hakuna kitu kama hicho kilitokea katika mchezo huo ambao golini alisimama, Ivo Mapunda na kikosi kilikuwa chini ya Mbrazili Marcio Maximo.**

Kaseja alisema ilikuwa ni maneno ya "uzushi" ambayo yalisambazwa na baadhi ya watu ambao hawakumtakia mema kwenye safari yake ya soka.

"Yeye (hakumtaja jina), alikuwa Mabibo na mimi nilikuwa Senegal, halikutokea jambo hilo, nadhani hayo ni maneno tu yaliyokuwa yanaongelewa na watu wa mtaani," alisema Kaseja.

Kuhusu kurejea kwake katika kikosi cha Stars, Kaseja alisema sababu pekee iliyomfanya Kocha Mkuu, Etienne Ndayiragije kumrejesha kwenye timu hiyo ni kiwango chake kizuri alichonacho na anaamini mchango wake wa kuisadia timu hiyo bado unahitajika.

"Nirudi nyuma, ndani ya hiyo miaka sita nilikuwa nacheza ligi, na ninaamini nilikuwa bora, sidhani kama ubora wa miaka sita nyuma na ubora wa sasa hivi nikawa sawa, nilikuwa na nguvu, sidhani kama ubora wa wakati huo ni sawa na nilionao sasa hivi, ninaonyesha kiwango kizuri, labda nilikuwa siendani na mifumo," alisema Kaseja.

Aliongeza kwa kudhihirisha hilo, yeye ndio kipa pekee aliyewahi kusajiliwa kwa dau la Dola za Marekani 30,000 kutoka Simba na kuelekea Yanga, kiasi ambacho kilikuwa kikubwa wakati huo.

Kipa huyo alisema pia mchezo wa Ligi ya Mabingwa dhidi ya waliokuwa mabingwa watetezi, Zamalek ulikuwa na 'mafuriko makubwa' lakini siku hiyo ilikuwa na bahati kwa upande wa Simba ambapo waliwavua taji vigogo hao wa Misri.

"Zamalek walikuwa wanashambulia sana, wanakuja kama mafuriko, achana na mipira iliyogonga mwamba, marehemu Christopher (Alex), alijifunga goli lilikataliwa, ndio maana nasema ilikuwa siku yetu," alisema Kaseja, kipa huyo wa zamani wa Moro United.

Alisema pia katika maisha yake ya mpira anajutia goli za 'kizembe' alilofungwa akiwa Simba dhidi ya FC Lupopo katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika baada ya mpira aliokuwa anaupiga mbele kumponyoka na kuingia wavuni.

Aliongeza kuwa anaamini KMC itabakia katika msimu ujao wa Ligi Kuu Bara kutokana na mipango na mikakati waliyonayo wachezaji na viongozi wa timu hiyo ya Kinondoni hapa jijini.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042